# UCHANGANUZI WA KIISIMU KATIKA MASHAIRI HURU YA KITHAKA WA MBERIA NA YA KEZILAHABIA LINQUISTIC ANALYSIS OF FREE VERSE OF KITHAKA WA MBERIA AND KEZILAHABI

**POULINE NANGILA WAFULA**
**C50/CE/28347/2018**

**TASNIFU HII IMETOLEWA KWA MADHUMNI YA KUTOSHELEZA BAADHI YA MAHITAJI YA UZAMILI KATIKA CHUO KIKUU CHA KENYATTA**

**JUNE, 2025**

# UNGAMO

Tasnifu hii ni kazi yangu mwenyewe na haijapata kuwasilishwa kwa mahitaji ya kutuzwa shahada yoyote katika chuo kikuu chochote.

Sahihi: …………………………………… Tarehe: 9/6/2025……………………………

POULINE NANGILA WAFULA

C50/CE/28347/2018

## MSIMAMIZI

Tasnifu hii imetolewa kwa idhini yangu kama msimamizi wa kazi hii ya chuo Kikuu cha Kenyatta.

Sahihi: …………………………………… Tarehe: 9/6/2025……………………………

**DKT. EDWIN W. MASINDE**

Chuo Kikuu cha Kenyatta

Idara ya Kiswahili

## TABARUKU

Naitabaruku tasnifu hii kwa marehemu baba yangu mpendwa Richard Wafula na mama yangu mpendwa Beatrice Wafula kwa kuniwekea msingi bora katika elimu, na kwa kipenzi cha roho yangu, mume wangu, Emmanuel Wanjala, kwa mapenzi yako kwa elimu na kujitolea kwako kuyawekea maisha yangu msingi imara. Kila mara ulinihimiza kutia bidii masomoni. Asante kwa kuniandalia mazingira mazuri yaliyoniwezesha kukamilisha kazi hii.

## SHUKRANI

Kwanza kabisa namshukuru Mwenyezi Mungu kwa kunipa neema, nguvu na afya nzuri ili kuifanya kazi hii tokea mwanzo hadi tamati. Utukuzwe Mola katika mataifa yote.

Pili, nampa shukrani za dhati msimamizi wangu kwa mwongozo wake wa hekima na ushauri alionipa ulinifaa na kuniwezesha kudhibiti na kumudu kazi hii.

Shukrani zangu ziwafikie wahadhiri wangu wote wa Chuo Kikuu cha Kenyatta katika idara ya Kiswahili na Lugha za Kiafrika kwa msaada na motisha walionipa katika kufanikisha kazi hii

Shukrani za kipekee zimwendee mume wangu Emmanuel Wanjala kwa kujinyima kila kitu ili kufadhili elimu yangu hii kila nilipomhitaji kuanzia karo na chochote kile kilichonifaa masomoni. Barikiwa sana mpenzi.

Sina budi kutoa shukrani zangu kwa wanangu wapendwa Hopeclara na Ashley. Asanteni kwa kunivumilia kwa muda huo wote katika kusoma na mlinitia motisha nikaze mwendo wakati nilipokosa tumaini, Mungu awape siha njema wanangu.

Aidha nawashukuru wanafunzi wenzangu Pauline Musyoki, Dorice Gakii, Ruth Moraa, Maurice Igongo, Dancan Abudho, Juma James na wengine wengi. Walinitia moyo na kunichochea wakati nilipotaka kukata tamaa.

Kadhalika nawashukuru wazazi wangu, ndugu zangu na marafiki wote walionitia ari ya kuendelea hadi nikamaliza elimu yangu. Mola awabariki.

## UFAFANUZI WA DHANA

**Isimu:** ni sayansi inayochunguza lugha.

**Fonolojia**: Tawi la isimu linalohusu uchambuzi wa mfumo wa sauti katika lugha.

**Hawaa:** Hamu ya kutaka kufanya kitu.

**Kiambajengo**: Kipashio ambacho ushirikiana na vipashio vingine katika kuunda kipashio kikubwa zaidi katika sentensi.

**Kikonyo:** Ni kipande kinachoshikilia tawi.

**Kiwizani**: Ni mapigo asilia ya mawimbi ya sauti.

**Matini:** Maandishi yanayohusu jambo lolote yaliyo katika umbo la kitabu au makala.

**Mizani:** Silabi za mishororo au mistari ya shairi.

**Mkazo:** Mkazo ni hali ambayo neno au silabi katika neno husikika kwa nguvu na kuwa na nguvu nyingi zaidi kuliko silabi zingine.

**Mpangilio msonge:** Mfumo wenye kupanga maneno au silabi kwa kutilia mkazo silabi zenye mkazo au nguvu.

**Mtindo**: Njia ya utekelezaji wa maana.

**Mizani**: Ulinganifu wa idadi ya silabi katika kila kipande au mshororo wa ubeti

**Uchanganuzi wa kiisimu:** Ni uhakiki wa kazi za fasihi kwa kuzingatia mbinu za kisayansi.

**Ujumi:** Kanuni zinazohusu ubora na ubaya wa kazi ya sanaa.

**Ushairi huru:** Huu ni ushairi ambao hauzingatii kanuni za utunzi wa mashairi ya kimapokeo

**Uwiano:** Hali ya kuwa vitu viwili au zaidi kuwa sawa au kulingana.

## ORODHA YA VIFUPISHO

**FM:** Fonolojia mizani.

**NACOSTI:** National Commission for Science, Technology and Innovation**.** Baraza la Taifa la Sayansi na Teknolojia.

**TUKI:** Taasisi ya uchunguzi wa Kiswahili.

**Uk:** Ukurasa.

## YALIYOMO

**YALIYOMOUNGAMO** ..... ii
**TABARUKU** ..... iii
**SHUKRANI** ..... iv
**UFAFANUZI WA DHANA** ..... v
**ORODHA YA VIFUPISHO** ..... vi
**IKISIRI** ..... x
**ABSTRACT** ..... xi
**SURA YA KWANZA** ..... 1
**UTANGULIZI** ..... 1
1.0 Usuli wa Mada ..... 1
1.1 Suala la Utafiti ..... 5
1.2 Malengo ya Utafiti ..... 7
1.3 Maswali ya Utafiti ..... 7
1.4 Sababu za Kuchagua Mada ..... 7
1.5 Umuhimu wa Utafiti ..... 9
1.6 Upeo na Mipaka ..... 9
1.7 Yaliyoandikwa Kuhusu Mada ..... 10
1.8 Misingi ya Nadharia ..... 14
1.8.1 Historia ya Nadharia ya Fonolojia Mizani ..... 15
1.8.2 Misingi ya Nadharia ya Fonolojia Mizani ..... 17
1.8.3 Mihimili ya Nadharia ya Fonolojia Mizani ..... 18
1.9 Mbinu za Utafiti ..... 19
1.9.1 Muundo wa Utafiti ..... 20
1.9.2 Mahala pa Utafiti ..... 20
1.9.3 Sampuli na Usampulishaji ..... 21
1.9.4 Ukusanyaji wa Data ..... 22
1.9.5 Uchanganuzi wa Data ..... 22
1.9.6 Uwasilishaji wa Matokeo ..... 23
1.9.7 Maadili ya Utafiti ..... 23
1.10 Hitimisho ..... 23

**SURA YA PILI..........24**

**KUBAINISHA VIPENGELE VYA KIISIMU NA JINSI VINAVYOTUMIKA KATIKA MASHAIRI HURU YA KITHAKA WA MBERIA ..........24**

2.0 Utangulizi .......... 24

2.1 Aina za Sentensi .......... 24

2.1.1 Sentensi/Mishororo Mishata .......... 25

2.1.2 Sentensi zenye Urefu Tofauti katika Beti .......... 28

2.1.3 Sentensi Ndefu .......... 32

2.2 Uakifishaji .......... 34

2.3 Kipengele cha Nafsi.......... 38

2.3.1 Nafsi ya Kwanza .......... 39

2.3.2 Nafsi ya Pili.......... 40

2.3.3 Nafsi ya Tatu .......... 42

2.4 Hitimisho .......... 45

**SURA YA TATU..........46**

**KUBAINISHA VIPENGELE VYA KIISIMU NA JINSI VINAVYOTUMIKA KATIKA KUENDELEZA KAZI YA MASHAIRI HURU YA KEZILAHABI ........46**

3.0 Utangulizi .......... 46

3.1 Aina za Sentensi .......... 46

3.1.1 Sentensi/Mishororo Mishata.......... 47

3.1.2 Sentensi zenye Urefu Tofauti katika .......... 50

3.1.3 Sentensi Ndefu .......... 54

3.2 Uakifishaji .......... 56

3.3 Kipengele cha Nafsi.......... 60

3.3.1 Nafsi ya Kwanza .......... 61

3.3.2 Nafsi ya Pili.......... 63

3.3.3 Nafsi ya Tatu .......... 65

3.4 Hitimisho .......... 67

**SURA YA NNE ..........68**

**UMUHIMU WA VIPENGELE VYA KIISIMU KATIKA KUENDELEZA KAZI YA MASHAIRI HURU..........68**

4.0 Utangulizi .......... 68

4.1 Umuhimu wa Aina za Sentensi katika Ushairi wa Kiswahili................................. 69
4.1.1 Umuhimu wa Sentensi za Mishata katika Ushairi Huru...................................... 69
4.1.2 Umuhimu wa Sentensi zenye Urefu Usiolingana katika Ushairi Huru............. 72
4.1.3 Umuhimu wa Matumizi ya Sentensi Ndefu katika Mashair Huru .................... 78
4.2 Umuhimu wa Uakifishaji katika Mashairi ya Kiswahili ........................................ 80
4.2.1 Uakifishaji kama Mbinu ya kujenga Uhuru katika Usarifu wa Lugha ............. 80
4.2.2 Uakifishaji kama Mbinu ya kuwasilisha Mawazo ........................................... 82
4.2.3 Uakifishaji kama Chombo cha kuchochea Usaili wa Utafakari wa Ujumbe .... 83
4.2.4 Uakifishaji kama Njia ya Kuelekeza Toni katika Mashairi na Kudhibiti Mwendo wa Usomaji ........................................................................................ 84
4.2.5 Viakifishi katika Kusaidia Kuifanya Matini Kueleweka Kisarufi .................... 85
4.3 Umuhimu wa Kipengele cha Nafsi katika Kuendeleza Ushairi Huru ..................... 87
4.3.1 Umuhimu wa Nafsi ya Kwanza katika Ushairi Huru....................................... 87
4.3.2 Umuhimu wa Nafsi ya Pili katika Ushairi Huru .............................................. 89
4.3.4 Umuhimu wa Matumizi ya Nafsi ya Tatu katika Ushairi Huru ........................ 90
4.4 Hitimisho ............................................................................................................ 91
**SURA YA TANO ...........................................................................................92**
**MUHUTASARI, MATOKEO NA MAPENDEKEZO YA UTAFITI ........................92**
5.0 Utangulizi ............................................................................................................ 92
5.1 Muhtasari wa Utafiti ............................................................................................ 92
5.2 Matokeo ya Utafiti ................................................................................................ 95
5.3 Changamoto za Utafiti ......................................................................................... 97
5.4 Hitimisho ............................................................................................................. 97
5.5Mapendekezo ........................................................................................................ 98
**MAREJELEO ...................................................................................................99**

# IKISIRI

Lengo kuu la utafiti huu ni kuonyesha jinsi ushairi unavyoweza kuchanganuliwa kiisimu. Tasnifu hii inahusu uhakiki wa kiisimu wa ushairi wa Kiswahili katika mashairi huru ya Kithaka wa Mberia na ya Kezilahabi kwa mtazamo wa nadharia ya Fonolojia Mizani. Utafiti huu umejikita katika diwani teule za watunzi waliotajwa ambazo ni *Doa, Msimu wa Tisa, Mvumo wa Helikopta, Kichomi* na *Karibu Ndani.* Uteuzi wa diwani hizi ulifanywa kimakusudi kwa kuwa zina aina data iliyodhamiriwa kuchanganuliwa kiisimu ambayo ilitosheleza mahitaji ya utafiti huu. Mashairi sitini yalihakikiwa kutoka katika diwani teule. Vipengele vya kiisimu vilivyochanganuliwa ni: Aina za sentensi, kipengele cha nafsi na uakifishaji. Utafiti huu uliongozwa na nadharia ya Fonolojia Mizani iliyoasisiwa na Liberman (1975) ambayo ina madai kuwa mkazo katika lugha uko katika mfumo wa mfuatano wiani wa kimsonge ambao hupanga silabi, maneno na virai katika sentensi. Tasnifu hii ina sura nne: Sura ya kwanza imeangazia utangulizi unaojumulisha vipengele vifuatavyo: mada, suala la utafiti, maswala ya utafiti, malengo ya utafiti, umuhimu wa utafiti, sababu za kuchagua mada, upeo na mipaka ya utafiti, yaliyoandikwa kuhusu mada, misingi ya nadharia, mihimili ya nadharia na mbinu za utafiti. Sura ya pili imeshughulikia vipengele vya kiismu vilivyobainishwa na jinsi vinavyotumika katika kuendeleza kazi ya mashairi huru teule ya Kithaka wa Mberia. Sura ya tatu imebainisha vipengele vya kiisimu na kuonyesha jinsi vilivyotumika katika kuendeleza mashairi huru ya Kezilahabi. Sura ya nne imeshughulikia umuhimu wa vipengele vya kiisimu kisha sura ya tano imeshughulikia muhtasari wa utafiti, matokeo ya utafiti, changamoto za utafiti na mapendekezo ya taifi zaidi. Data iliyotumika katika utafiti huu ilikusanywa kutoka maktabani. Maktabani ndiko usomaji ulifanywaa wa diwani za mashairi teule, tasnifu na vitabu vingine vinavyohusiana na mada ya utafiti na nadharia ya utafiti huu. Uchanganuzi wa data ulifanywa kwa kutumia mbinu ya uhakiki matini kwa kuongozwa na pengo la utafiti, maswali na malengo ya utafiti na kwa kuongozwa na mihimili ya nadharia ya Fonolojia Mizani. Kwa kufanya hivi, utafiti uligundua kwamba mbinu za kiisimu zinaweza kutumiwa katika uhakiki wa mashairi huru ya Kiswahili.

## ABSTRACT

The main aim of this research is to show how poetry can be analyzed using linguistic tenets. The thesis is about linguistic analysis of Kithaka Wa Mberia and Kezilahabi's free verse using Metrical phonology theory. The study focuses on selected anthologies; *Doa, Msimu wa Tisa, Mvumo wa Helikopta, Karibu Ndani* and *Kichomi.* The texts were purposefully sampled due to the fact that they had the data required for this study. Sixty poems were analysed. The linguistics tenets used included types of sentences, personalizations and punctuations. This research was guided by the principles of metrical phonology which was formulated by Liberman (1975). This theory is a syllable based multi-linear theory of Phonological description and analysis. In Metrical phonology, the utterance is broken into segments in a hierarchical order. Basic units of metrical organization are the syllables, stress foot, phonological word and intonation phrases. The thesis has five chapters. The first chapter contains the following sections: background information, problem of the study, objectives of the study, research questions, literature review, significance of the study, theoretical framework and research methodology. Chapter two contains analysis of linquistic elements and how they are used in free verse of Kithaka wa Mberia. Chapter three contains analysis of linquistic elements and how they are used in the free verse of Kezilahabi. Chapter four analyses the significance of the linquistic elements in free verse in Kiswahili poetry. Chapter five has the summary and conclusions of the whole thesis. Data collected for this study was library based where selected texts were analysed. Also, it is in the libray where literature review was done. Further, the theory undergirding the study was selected. Data collection was done through indepth reading and selection of areas that had the required data. Data analysis was done through critical analysis guided by the gap to be filled, research objectives, research questions and the tenetss of the theory. Generaly the study found that linguistic approaches can favourably be used in the analysis of Kiswahili free verse

# SURA YA KWANZA

# UTANGULIZI

## 1.0 Usuli wa Mada

Kazi za kifasihi zina njia au namna teule ambazo huwasilishwa, tanzu za fasihi mathalani: riwaya, tamthilia na ushairi na tanzu nyingine zina namna ya kipekee ya matumizi ya lugha na hivyo kila moja hujitofautisha na utanzu mwingine katika uwasilishaji. Halikadhalika wasanii mbalimbali wa kazi za fasihi wana namna zao za kipekee za kutumia lugha kwa kila utanzu. Hali hii huweza kumtofautisha msanii mmoja kutoka kwa mwingine kutokana na mitindo yao tofauti ya matumizi ya lugha. Hata hivyo, matumizi ya lugha katika ushairi hujitofautisha zaidi na tanzu zingine za kifasihi kama vile riwaya na tamthilia. Ushairi unajitenga zaidi na tanzu nyingine kwa jinsi unavyotumia lugha ya maneno machache, lugha ya mkato na teule yenye uwezo wa kuibua hisia na ujumi katika kuelezea fikra pana na za ndani kama ilivyo kazi nyingine za kifasihi Leech na Short (1989). Watalaam kama vile Graham (1968), Easthope (1983) na Besha (1993), wanaeleza kuwa "viambajengo mbalimbali vya lugha ndivyo vinavyojenga maana na pia vinavyojenga ujumi katika ushairi wa Kiswahili."

Ushairi ni utanzu mmojawapo katika fasihi ambao una mvuto zaidi. Ushairi umegawika katika mashairi huru ambayo hayazingatii arudhi katika utunzi wake na mashairi ya kijadi ambayo yanazingatia arudhi. Namna mashairi ya aina hizi mbili yanavyoonekana kwa umbo la nje ni tofauti. Utafiti huu ulilenga kuchanganua mashairi huru kwa kuzingatia mbinu za kiisimu za kifonolojia.

Ingawa kuna kaida za kijadi zinazoongoza utunzi, watunzi wa mashairi-huru wametumia mbinu kadhaa katika kusawiri maudhui na kuibua dhamira zao.  Mashairi huru hutumia ubunifu wa kipekee katika kuyatunga mashairi ya Kiswahili. Uhuru wa utunzi wa ushairi huru umekita tu katika kule kutozingatia arudhi ambazo ndizo kaida za utunzi wa mashairi ya kimapokeo. Hii ina maana kuwa "uhuru wa mashairi huru si tu uhuru bali ni uhuru wa busara unaoshikana na hisia na ufundi wa utunzi" (Mohammed, 2002:09).

Ushairi huru ni hatua ya maendeleo ya kimuundo katika utunzi wa ushairi ambao una usuli wake katika mapigo ya nyimbo. Mapigo ya nyimbo hizi yaliibua muundo wa vina na mizani ambayo huzingatiwa kama umbo la shairi. Ushairi wa jadi ulithaminiwa sana kwa namna ya kuwasilisha ujumbe kwa kuzingatia umbo ili ujumbe upatikane kama anavyosema Mazrui (1987) hapana shaka kwamba umbo la mashairi daima litakuwa na umuhimu mkubwa katika kuwasilisha maudhui. Aidha, Arege (2016) anaongeza kuwa, licha ya uhuru katika aina hii ya mashairi, tungo hizi si nathari bali ni ushairi kwa sababu zina sifa nyingine za ushairi kama vile lugha teule, lugha ya mkato na yenye uwezo wa kuibua hisia na ujumi wa kuridhisha kishairi.

Wasomi mbalimbali wametoa fasiri kuhusu ushairi huru. Arege (1998:1). Ushairi huru ni ushairi ambao haufuati kanuni za kijadi katika utunzi wake. Kulingana na yeye katika ushairi huru mshairi hajifungi katika kanuni za mtirirko wa vina, ulingalifu wa mizani na hata idadi sawa ya mishororo katika kila ubeti. Wangari (1988:51). Ushairi huru ulikwepa kanuni ya ujitoshelezi wa ubeti hivyo kufanya shairi kuonekana kama mkusanyiko wa mistari tu, iliyokusanywa pamoja bila sababu maalaum wala umoja wa maudhui".

Lampert (1946) anasema kuwa “mashairi huru huwa ni mkusanyiko wa tungo zenye anuwai za ufundi wa kisanaa.” Anaeleza kuwa mashairi huru ni mashairi yasiyogawika katika mikondo ambazo ndizo kanuni za utunzi katika mashairi ya kimapokeo.

Wamitila (2002:96) anaeleza kuwa badala ya kutegemea mizani na vina kuzua maana, inafaa kutegemea mbinu zingine kama vile mpangilio wa maneno, unyambuaji wa maneno na mpangilio wa sentensi katika kuzua hisia nzito katika utungo wa kishairi. Kwa mujibu wa maoni yake, vipengele hivi ndivyo vya kimsingi vya kutambulisha ushairi kwa vile ni vipashio zaidi ya vina na mizani. “Ushairi huru huwa na usambamba wa kimawazo pamoja na kimatumizi ya urudiaji katika kiwango cha neno, virai na hata sentensi.”

Mitazamo ya baadhi ya wasomi hawa inadhihirisha kuwa ushairi huru husisitiza zaidi vigezo vinavyodhibiti maana na fahiwa na kupuuza umaarufu wa umbo kama kitambulisho kikuu cha tungo. Hii ni kwa vile ushairi huru ni sehemu ya utamaduni wa jamii na umbo lake limekuzwa kupitia vipindi mbalimbali kulingana na tamaduni za jamii husika. Ushairi huru kama utanzu mmoja wapo wa tanzu za fasihi andishi unaweza kuchanganuliwa kiisimu matini ili kudhihirirsha kuwa ni matini. Uchanganuzi wowote wa matini kama kipashio cha lugha huzingatia muala na a kwani ni miongoni mwa viambajengo muhimu sana vya matini.

Ni muhimu kumakinika katika sifa mbalimbali za kiisimu ili uweze kuyachambua mashairi huru vilivyo. Viwango mbalimbali vya lugha kama vile aina za sentensi, uakifishaji na vinginevyo vingi hutumiwa kwa lengo maalum na kwa njia maalum. Kwa mfano, katika ushairi huru washairi wanaweza kuunda midundo mbalimbali kwenye ushairi kwa kuzingatia viwango mbalimbali vya lugha mathalani sarufi, mofolojia na mantiki badala

ya kuzingatia mizani na vina ambazo ni sifa kuu za kifonolojia katika kujenga mdundo. Kuzingatia viwango hivi katika utunzi wa mashairi huru kunaweza kuzua muwala na mtiririko mzuri wa habari. Katika mashairi huru pia mpangilio wa herufi, silabi, mofimu, maneno na sentensi huoana na maudhui ya mtunzi kwa madhumuni maalumu katika kubainisha namna ya kujenga midundo katika ushairi huru (Masinde, 2007).

Ushairi huru hujikita katika sifa za kiisimu ambazo humfanya msomaji aweze kuliona jambo fulani kwa uwazi zaidi. Mara kwa mara jambo hili husababishwa na ukiushi wa kiisimu mathalani mpangilio ambao si wa kawaida wa vipashio mbalimbali licha ya kuwa hii sio njia pekee Wamitila (2002: 106) katika kutokeza kwa njia ya mpangilio wa utungo; yani tunapoliangalia shairi tunaona limechukua muundo fulani.

Kahigi (1975) anatoa maelezo kuwa ushairi wa Kiswahili unafaa kutazamwa kisayansi. Mtazamo huu wa kisayansi ni wa kihalisia unaoangalia historia yote ya ushairi kijumla kulingana na mabadiliko ya mfumo na tamaduni za jamii na kuzingatia lengo na maendeleo ya jamii husika. Mtazamo wa kisayansi huweza kukiangalia kitu jinsi kilivyo maishani mathalani sehemu ya mchangamano wa vitu vingi kwenye maumbile na kama kitu kilicho na mabadiliko mara kwa mara hutegemea mazingira yaliyokizunguka.

Uhusiano wa fasihi na isimu ni wa kimsingi kwa kiwango kikubwa, kwa kuzingatia nadharia na njia za utafiti wa kiisimu zinaweza kutumika katika uchambuzi wa kazi za kifasihi. Isimu hueleza ni kwa nini msomaji hupata hisia fulani anaposoma kazi ya kifasihi. Uchanganuzi wa aina hii humwezesha mhakiki kutathmini ujuzi wa mwandishi kuhusu lugha anayotumia Traugott na Pratt (1980).

Matumizi ya lugha na vipengele vya kiisimu katika kazi ya ushairi huru hulenga usanifu na ubunifu ambacho ndicho kipengele kinachotofautisha fasihi na taaluma zingine. Uhakiki unaozingatia lugha katika kazi ya fasihi aghalabu hutumia isimu ambayo ni taaluma inayochambua lugha kisayansi. Viwango vya lugha yafaa vichunguzwe katika kuhakiki ushairi kifasihi ndipo kiwango cha uelewaji wa kazi hii kiinuke.

Kazi za Kithaka Wa Mberia: *Msimu wa Tisa* na *Mvumo wa Helikopta* pamoja na diwani za Kezilahabi: *Kichomi* na *Karibu Ndani* ni baadhi ya diwani za hivi punde zinazofuata mkondo huu. Kazi hizi zinaonesha mpangilio unaoenzi ushairi huru kando na kupiga hatua katika matumizi ya maumbo kama vile michoro, jambo ambalo ni geni kwenye ushairi wa Kiswahili. Tafiti ambazo zimefanywa kuhusu uchanganuzi wa kiisimu katika ushairi huru wa Kiswahili hazijafanywa kwa misingi na mkabala wa nadharia ya Fonolojia Mizani. Ni kwa msingi huu ndipo utafiti ulifanywa kushughulikia uhakiki wa kiisimu katika ushairi huru wa Kiswahili.

### 1.1 Suala la Utafiti

Utafiti huu umehakiki mashairi huru ya Kithaka wa Mberia na ya Kezilahabi. Mashairi huru ni yale mashairi yasiyozingatia kanuni za utunzi kama yalivyo mashairi ya kiarudhi

Taaluma za isimu haziwezi kutenganishwa na taaluma za kifasihi kwa vile zina uhusiano na hutegemeana na kukamilishana. Kwa kuzingatia nadharia na njia za uhakiki wa kiisimu, ni Dhahiri kwamba mbinu za kiisimu zinaweza kutumika katika uchambuzi wa kazi za kifasihi, hii inatokana na sababu ya kwamba isimu hueleza kwa nini msomaji hupata hisia fulani anaposoma kazi za kifasihi (Traugott na Pratt 1980:20). Uchanganuzi wa aina hii humwezesha mhakiki kutathmini ujuzi wa mwandishi kuhusu lugha aliyoitumia.

Matumizi ya lugha na vipengele vya kiisimu katika kazi ya ushairi huru hulenga usanifu na ubunifu wa mtunzi. Hiki ndicho kipengele kinachotofautisha utanzu wa fasihi na taaluma zingine. Hivyo, uhakiki unaozingatia lugha katika kazi ya fasihi aghalabu hutumia isimu ambayo ni taaluma inayochambua lugha kisayansi. Kwa mantiki hii, viwango vya lugha katika ushairi huru wa Kiswahili vinafaa kuchunguzwa ili kuinua viwango vya uelewaji wa mashairi husika.

Kila mtafiti huwa na ujumbe wa kuwasilisha kwa hadhira yake anapoandika kazi yake ya kifasihi. Hivyo, mwandishi hana budi kubuni njia ya kutumia kuwasilisha kazi yake.
Utafiti wa ushairi huru wa Kiswahili unaweza kuhakikiwa kiisimu kama kazi zingine za kifasihi.

Kazi za awali ambazo zimefanywa katika fasihi ya Kiswahili kwa kuongozwa na nadharia za kiisimu zimejikita katika tanzu za riwaya. Kwa mfano Osore (1994) alishughulikia uhakiki wa kiisimu wa fasihi kwa kurejelea riwaya za Suleiman Mohamed. Alipata kwamba taaluma za isimu haziwezi kutenganishwa na taaluma za kifasihi kwa vile zina uhusiano, hutegemeana na kukamilishana. Hivyo, uhusiano wa fasihi na isimu ni wa kimsingi kwa kiwango kikubwa. Naye Okuku (2010) alifanya uchanganuzi wa kiisimu katika baadhi ya matini za Kiswahili akitumia mtazamo wa kipragmatiki Leksia. Katika kazi yake pia, amerejelea riwaya ya Kiza Katika Nuru. Alipata kwamba nadharia ya pragmatiki Leksia inaweza kutumika kuchanganua matini za kiswahili, semi katika matini za Kiswahili ambazo huzua maana ambazo ni pana katika misingi ya Pragmatiki Leksia na pia uhusiano wa usemi na muktadha ni muhimu katika kufasiri maana.  Tofauti na tafiti za

awali zilizotumia mkabala wa kiisimu katika utanzu wa riwaya, utafiti huu ulitumia mkabala wa kiisimu katika utanzu wa ushairi wa Kiswahili amabao ni tafauti

## 1.2 Malengo ya Utafiti

Utafiti huu utaongozwa na malengo yafuatayo:

1. Kubainisha vipengele vya kiisimu katika mashairi huru na jinsi vinavyotumika katika kuendeleza mashairi huru ya Kithaka wa Mberia.
2. Kubainisha vipengele vya kiisimu katika mashairi huru na jinsi vinavyotumika katika kuendeleza mashairi huru ya Kezilahabi.
3. Kueleza umuhimu wa vipengele vya kiisimu katika kuendeleza kazi ya mashairi huru teule.

## 1.3 Maswali ya Utafiti

Utafiti huu utalenga kujibu maswali yafuatayo:

1. Ni vipengele gani vya kiisimu vinavyobainika katika mashairi huru na ni kwa jinsi gani vinatumika katika kuendeleza mashairi huru ya Kithaka wa Mberia?
2. Ni vipengele gani vya kiisimu vinavyobainika katika mashairi huru na ni kwa jinsi gani vinatumika katika kuendeleza mashairi huru ya Kezilahabi?
3. Vipengele vya kiisimu vina umuhimu gani katika kuendeleza kazi ya mashairi huru teule?

## 1.4 Sababu za Kuchagua Mada

Ushairi wa Kiswahili umekuwa ukichanganuliwa kwa kuzingatia vipengele vya fani, mtindo na maudhui. Utafiti huu ulionelea kuwa kuna haja ya kuzingatia pia kipengele cha isimu katika uhakiki wa mashairi ya Kiswahili. Tafiti hizi ni pamoja na: Nyamai (2015) aliyechunguza mtindo katika mashairi ya Kiswahili, Kemuntho (2016) aliyechunguza

mtindo katika utenzi wa katirifu. Mikondo hii ni tofauti na ule ambao utafiti huu ulichukua katika kubaini jinsi ushairi huru wa Kiswahili unavyoweza kuchanganuliwa kiisimu.
Pili, kuna baadhi ya tafiti zilizofanywa ambazo zilichunguza vipengele vya kiisimu ila zilifanywa katika tanzu nyingine za fasihi, mathalani riwaya na tamthilia. Hawa ni pamoja na Osore (1994) aliyechunguza uhakiki wa kiisimu katika riwaya za Suleiman. Isitoshe, Mohamed na Makanga (2008) waliochunguza uhakiki wa kiisimu kwa kujikita katika vipengele vya muwala na mshikamano katika mashairi huru ya Kithaka Wa Mberia.

Hata hivyo tafiti zilizofanywa haswa kuhusu uchanganuzi wa kiisimu katika kazi za kifasihi hazikuhakikiwa kwa misingi ya nadharia ya Fonolojia Mizani ambayo iliasisiwa na Liberman (1975). Nadharia hii inadai kuwa mkazo katika lugha umewekwa kwenye mfumo wa mfuatano wiani wa kimsonge ambao kwa kawaida hupanga maneno, silabi na virai katika sentensi.

Ushairi huru una upekee wake kutokana na vile ambavyo umetungwa pasi kuzingatia kanuni za utunzi, hauna mpangilio wa kiarudhi kama yalivyo mashairi ya kiarudhi. Kutokana na sababu hii ndipo utafiti huu ulifanywa kwa kuchanganua mashairi huru teule hasa kwa kutumia vipengele vya kiisimu.  Pengo hili lilitoa nafasi ya uchunguzi ili kubaini na kuainisha vipengele vya kiisimu vinavyotumika katika utunzi wa mashairi huru ya Kiswahili.

Utafiti huu utakuwa wa manufaa sana kwa wahakiki, walimu wa Kiswahili na fasihi, wakuza mitalaa ya Kiswahili na fasihi. Pia, watanufaika kwa kuelewa jinsi ya kufanya uchanganuzi wa mashairi huru kwa kutumia mbinu za kiisimu.

### 1.5 Umuhimu wa Utafiti

Kila utafiti wowote ule una manufaa yake mahususi kulingana na kile kinachotafitiwa. Inatarajiwa kwamba matokeo ya utafiti huu yatakuwa na mchango mkubwa katika taaluma ya ushairi kwa kuonyesha namna mashairi ya Kiswahili yanavyoweza kuchanganuliwa kiisimu. Utafiti huu utakuwa na umuhimu kama rejeleo katika tafiti za baadaye. Aidha inatarajiwa kwamba utafiti huu utakuwa na manufaa kwa wahakiki, walimu wa Kiswahili na fasihi, wakuza mitalaa ya Kiswahili na fasihi na hata kwa wanafunzi wa Kiswahili katika viwango mbalimbali. Isitoshe, watanufaika kwa kuelewa jinsi ya kuchanganua mashairi huru kwa kutumia mbinu za kiisimu.

### 1.6 Upeo na Mipaka

Utafiti huu umejikita katika diwani teule za Kithaka wa Mberia ambazo ni: *Mvumo wa Helikopta*, *Doa* na *Msimu wa Tisa* pamoja na diwani za Kezilahabi ambazo ni *Kichomi* na *Karibu Ndani*. Kwa jumla mashairi sitini yalishughulikiwa kutoka kwenye diwani teule zilizotajwa awali.

Utafiti huu ulihakiki vipengele vya kiisimu ambavyo ni: aina za sentensi, kipengele cha nafsi, na uakifishaji. Diwani hizi ziliteuliwa kimakusudi kwa vile zina aina ya data iliyokidhi mahitaji ya utafiti huu.

Data hiyo ilihusu vipengele vya kiisimu na jinsi vinatumika katika kuendeleza kazi ya mashairi huru ya Kiswahili, namna vipengele hivyo husaidia katika uendelezaji wa mashairi huru ya watunzi.

Watunzi Kithaka Wa Mberia na Kezilahabi waliteuliwa kimakusudi kwa vile mashairi yao yamejikita katika mashairi huru. Halikadhalika, mashairi yao yana aina ya data iliyohitajika na ni data teule iliyotosheleza mahitaji ya utafiti huu.

### 1.7 Yaliyoandikwa Kuhusu Mada

Tafiti nyingi zimechunguza ushairi wa Kiswahili kwa kuangazia dhima, fani, maudhui na mtindo ila tafiti zilizofanywa kuhusu uchanganuzi wa matini ya kifasihi hazijangazia kazi za ushairi huru. Dhamira ya utafiti huu ilikuwa ni kuangazia uchunguzi wa kiisimu katika mashairi huru ya Kezilahabi na ya Kithaka wa Mberia. Katika usomaji wa tafiti mbalimbali ambazo zimefanywa, ilibainika kuwa zinakaribiana, kuchangiana na kuhusiana na utafiti huu. Hata hivyo, hakuna utafiti ambao unafanana moja kwa moja na huu lakini kazi hizo zilitufaa katika marejeleo.

Kahigi (1975) anaeleza kuwa “mashairi ya Kiswahili yanafaa kutazamwa kisayansi.” Mtazamo huu ni wa kihalisia unaotazama historia yote ya ushairi kijumla unapohusishwa na mabadili ko ya mfumo katika jamii kwa kuzingatia nia na maendeleo yake. Kwa kunukuu maelezo ya Kahigi (1975) mtazamo huu hukiangalia kitu kilivyo katika maisha kama sehemu ya mchangamano wa mambo mengi katika maumbile na kama kitu kinachobadilika kila wakati hutegemea mazingira ambayo yamekizingira. Maoni haya yalisaidia sana katika utafiti kwa kuelewa jinsi ya kuchanganua ushairi wa Kiswahili kwa kutumia mbinu za kiisimu.

Chacha (1980) amehakiki ushairi wa Abdilatif katika kiwango cha maudhui akizingatia uhakiki wa diwani ya *Sauti ya Dhiki* na *Uteuzi wa Hawaa*. Utafiti wake ni tofauti na huu kwa sababu, utafiti wa awali umejikita katika kibwagizo ilhali utafiti huu umeangazia

uchanganuzi wa ushairi huru kiisimu katika mashairi huru ya Kezilahbi na Kithaka. Utafiti huu uliongozwa na nadharia ya Fonolojia Mizani ambayo ni tofauti na ile iliyotumikizwa na Chacha.

Osore (1994) alichunguza uhakiki wa kiisimu wa fasihi katika riwaya teule za Suleiman Mohamed. Mtafiti huyu alijikita katika riwaya ya *Kiu* na *Nyota ya Rehema*. Vipengele vya kiisimu alivyovahakiki ni: Aina za sentensi, wahusika, taswira na methali. Alizingatia viwango vitatu vya isimu ambavyo ni:  semantiki, isimu miundo na sintaksia katika kuchanganua kazi yake. Kazi hii ni tofauti na utafiti huu kwa vile, mtafiti wa awali alihakiki riwaya ilhali utafiti huu umeangazia mashairi. Pia, alihakiki vipengele tofauti na utafiti huu. Hata hivyo, kazi ya awali ilimpa mtafiti uelewa wa kuhakiki matini za kifasihi kiisimu.

Isitoshe, Nzuki (2003) alishughulikia mwingiliano wa fani na maudhui katika ushairi wa Kithaka wa Mberia. Katika utafiti wake, mtafiti alichunguza aina mpya za fani ambazo zinatumika katika ushairi huru na jinsi ambavyo zimechangia katika kukuza maudhui. Kazi yake imechangia utafiti huu kwa vile, imeshughulikia mtindo mpya wa uandishi ambao ni sifa mojawapo ya ushairi huru wa mwandishi ambaye mashairi yake yanashughulikiwa katika utafiti huu. Hata hivyo, kazi yake ni tofauti na utafiti huu kwa sababu yeye amejikita katika fani na maudhui katika mashairi ya Kithaka wa Mberia lakini utafiti huu ulichunguza uhakiki wa kisimu wa kazi ya ushairi huru.

Vilevile, Makanga (2008) katika utafiti wake ameangalia uchanganuzi wa kiisimu katika matini ya *Msimu wa Tisa*. Katika kazi yake ameshughulikia muala na mshikamano katika mashairi huru ya Kithaka wa Mberia kwa mtazamo wa nadharia ya Muala na Mshikamano. Kazi hii ilifaa utafiti huu sana kwa vile imehakiki kitabu ambacho ni mojawapo wa vile

ambavyo vilichanganuliwa, isitoshe, amechanganua baadhi ya vipengele vya kiisimu katika kazi yake. Hata hivyo, kazi yake ni tofauti na hii kwa sababu utafiti huu umejikita katika vipengele vya kiisimu lakini yeye ameangazia muala na mshikamano, halikadhalika nadharia aliyoitumia ni tofauti na yetu.

Utafiti wa Nyamai (2015) ulichunguza mtindo katika mashairi kwa kuangazia vipengele vya dhima na kibwagizo katika diwani ya "*Sauti ya Dhiki* ya Abdilatif Abdalla (1973), *jicho la Ndani* ya Said A Mohamed (2002) na *Dhifa* ya Kezilahabi (2008)." Baadhi ya mashairi yalizingatia kanuni za kiarudhi bali mengine yalikaidi arudhi. Aidha, ushairi wake ulizingatia nadharia ya Mtindo. Utafiti wake ulifaa kazi hii kwa vile umechanganua diwani ya Kezilahabi ambayo utafiti huu umeihakiki, hivyo iwezesha kuelewa namna ya kuchanganua baadhi ya vipengele vya kiisimu katika kazi ya ushairi huru. Hata hivyo, utafiti wa awali ni tofauti na huu kwa vile utafiti huu ulichanganua fasihi kiisimu kwa kutumia nadharia ya Fonolojia Mizani.

Okuku (2010) alishughulikia uchanganuzi wa kiisimu wa baadhi ya matini za Kiswahili kwa kutumia mtazamo wa pragmatiki leksia. Katika kazi yake ameshughulikia tamathali za semi akirejelea riwaya ya Kiswahili. Kazi hii ilifaa utafiti huu kwa kuelewa jinsi ya kuchanganua baadhi ya matini au vipengele vya ushairi huru kiisimu. Utafiti wa Okuku ni tofauti na huu kwa vile unaangazia uchanganuzi wa mashairi huru kiisimu kwa kuzingatia mtazamo wa Fonolojia Mizani.

Utafiti wa Gicuka (2011) ulichunguza usawiri wa maudhui ya ndoa katika ushairi wa Kezilahabi na wa Kithaka wa Mberia. Alitumia nadharia ya Umuundo-Utekelezi inayoonesha kuwa, jamii ni mfumo unaochangiwa na vipengele vyake vyote ili kuwe na

mshikamano. Utafiti wa Gicuka ni tofauti na huu kwa kuwa, alishughulikia maudhui kwa kuchanganua mashairi ya Kezilahabi na Kithaka wa Mberia. Halikadhalika, alitumia nadharia ya Umuundo na mtindo tofauti na huu utafiti ambao umechanganua mashairi huru kwa mtazamo wa nadharia ya Fonolojia Mizani.

Aidha, Shavinya (2015) aliangazia uchanganuzi wa kiisimu wa baadhi ya semi katika matini za kidini kwa mtazamo wa kipragmantiki. Kazi ya Shaviya ni tofauti na hii kwa vile kazi hii imechanganua ushairi huru kwa kuzingatia mtazamo wa nadharia ya Fonolojia Mizani. Utafiti huu ulifaa kazi hii kwa kusaidia kuelewa jinsi vipengele vya asihi vinavyoweza kuchanganuliwa kiisimu.

Kitsao (1975) ameangalia uhakiki wa miundo ya kazi za fasihi ya Kiswahili. Kwa kufuatilia mwongozo wa Crystal na Davy (1969) anachambua mitindo ya aya za kazi alizochagua katika viwango vitatu vya kiisimu: Semantiki, sarufi na mofolojia. Katika utafiti wake alijaribu kuoanisha matumizi ya lugha na maudhui lakini hakuzingatia ushairi mzima bali beti moja tu. Hata hivyo, kazi yake ilisaidia utafiti huu kwa kuelewa namna ya kuchanganua kazi ya kifasihi kwa mtazamo wa kiisimu haswa tukiangazia kipengele cha sarufi ambacho naye alikihakiki katika utafiti wake.

Leech (2008) amechunguza mashairi ya Kiingereza *Ode to the west wind*. Mtafiti wa awali alilenga kudhihirisha umuhimu wa kuchunguza lugha katika uchunguzi wa maana ya shairi. Pia, ameonesha jinsi uhakiki wa mtindo unavyosaidia msomaji katika kuelewa dhana za kilele, mtiririko na taharuki. Katika utafiti wake, ameonyesha umuhimu wa uhakiki wa sifa za kiisimu katika fasihi ambapo zinasaidia mhakiki wa fasihi kuifahamu

kazi husika, hivyo uchanganuzi wa fasihi kiisimu unaohusu fasihi unadhihirika katika mashairi huru.

Pia, Nofal (2011) alichunguza sintaksia katika ushairi kwa mtazamo wa kipragmantiki kwa kulinganisha lugha ya kawaida na lugha ya kishairi jinsi zinavyotofautiana. Kazi yake imeangazia ngazi mbalimbali za lugha kama vile maumbo, sauti na vikundi vya maneno vinavyojenga ushairi. Kazi hiyo imeonesha kuwa lugha ya kishairi hailingani na lugha ya kawaida kwa vile lugha ya kishairi ina kanuni za kubadilisha sarufi kwa mfano katika mnyambuliko wa maneno, virai, vishazi au sentensi. Aidha, amefafanua kuwa lugha ya kishairi ina kaida ya kutofuata mpangilio wa maneno wa kawaida. Kazi hii ilitoa mchango mkubwa kwenye utafiti huu katika kuchambua sintaksia katika mashairi huru teule yaliyoshughulikiwa.

Ni bayana kuwa kazi hizi ambazo tumezitaja hazijashughulikia ushairi huru kwa malengo kama tuliyo nayo. Baadhi ya wahakiki ambao wamejaribu kutumia mtazamo huu wa kiisimu katika kuchanganua kazi za kifasihi hawakuingilia kwa undani wake. Kwa mfano kuna wale walihakiki tu kwa kuchunguza vipengele vichache, wengine wamehakiki tu sehemu ya beti au mishororo katika kazi husika. Utafiti huu umeziba mapengo haya kwa kuhakiki ushairi huru kiisimu ili kuthibitisha uhusiano uliopo kati ya isimu na fasihi haswa katika utanzu wa ushairi huru wa Kiswahili.

### 1.8 Misingi ya Nadharia

Utafiti huu uliongozwa na nadharia ya Fonolojia Mizani (FM). Fonolojia Mizani ni nadharia iliyoasisiwa na Liberman (1975) katika tasnifu yake ya uzamili ya “The intonation system of English.” Nadharia hii ilipendekezwa kwa malengo kutaka kujaribu kusuluhisha

matatizo yaliyojitokeza katika kuchanganua mkazo katika lugha ya Kiingereza. Nadharia ya Fonolojia Mizani baadaye iliendelezwa na Liberman na Prince (1977) na hatimaye ikafafanuliwa zaidi kwa upana na Halle na Vergnaud (1987).

### 1.8.1 Historia ya Nadharia ya Fonolojia Mizani

Nadharia ya FM inatoa maelezo kuwa mkazo katika lugha uko katika mfumo wa mfuatano wiani wa kimsonge ambao hupanga silabi, maneno na virai katika sentensi. Fonolojia Mizani ni nadharia ya mtazamo wa kuchanganua mfumo wa sauti za lugha uliojikita katika mfumo sauti mathalani kitu kilichojengeka kimsonge kwa kufuata misingi ya silabi lakini chenye mahusiano ya viwango tofauti kati ya vipengele vyake (Massamba, 2004). Nadharia hii inahusika na utayarishaji wa vijenzi kwa vikundi vyenye hadhi sawa. Vijenzi hivi kwa kawaida vinaungana na kuwa silabi kisha silabi kuwa tamko na tamko kuwa neno ambacho ndicho kipashio kikubwa.

Nadharia ya Fonolojia Mizani iliasisiwa ili kuwezesha kuafikiwa kwa kifonetiki katika semi mbalimbali na wizani na mizani. Ililenga kushughulikia hali ya kubadilika kwa shadda katika irabu swia na ukadiriaji wa usemi (Clair, 2006). Ilizinduliwa na Liberman (1975) na kuendelezwa na Liberman na Prince (1977). Katika Fonolojia Mizani mkazo huchukuliwa kama kihusishi kati ya vijenzi unaowakilishwa kwa matawi mizani kama uhusiano pigo kati ya vifundo umbu vilivyoonyeshwa kama vyenye nguvu na dhaifu. Baadaye nadharia hii iliendelezwa na: Hayes (1980), Prince (1983), Halle na Vergnaud (1987).

Liberman na Prince (`1977) wanadhihirisha uwakilishi wa mkazo kwenye lugha katika viwango vikuu vya neno na tungo. Uwakilishi huu unatumia miti ya mizani katika jozi uwilikinzani kwa kuziweka alama ya nguvu na alama isiyokuwa na nguvu kwenye kila mwisho wa tawi. Walitumia gridi ili kuonyesha tofauti za sauti zenye nguvu msikiko katika kila silabi zinazounda maneno ambayo yanajenga tungo.

Nadharia hii ya Fonolojia Mizani ilichaguliwa kwa sababu tulihakiki mashairi huru ya Kiswahili kutumia vipengele vya kiisimu katika mashairi teule ya Kithaka Wa Mberia na Kezilahabi.

Kwa kiasi kikubwa, utafiti huu ulijikita katika vipengele vifuatavyo vya kiisimu ambavyo ni:

a. Aina za sentensi.
b. Kipengee cha nafsi
c. Uakifishaji.

Nadharia ya Fonolojia Mizani hutoa muundo unaowakilisha mkazo kama kipengele kinachotumika kwa vijenzi husika au silabi kwa urejeleaji wa silabi zingine katika kifungo. Hushikilia kuwa kila neno au kishazi kina silabi mkazo moja. Mkazo husambazwa kiwizani kwa vile ni wa kimsonge na haulasimishwi. Lengo ni kuwa mkazo hudhihirisha muundo wa kiwizani wa kiisimu na kuwa sifa za kifonolojia za kipekee za mkazo zaweza kuelezwa kwa msingi huu. Fonolojia Mizani hueleza masharti ya mizani ya shairi kimfanano na sheria za sintaksia. Hadhi ya kijenzi hufafanuliwa kulingana na vijenzi vingine katika kishazi kimoja. Mkazo unaofikiriwa wa silabi hutokana na sehemu yake katika matawi mizani ya solo mizani.

Ujitokezaji wa kiisimu katika nadharia ya Fonolojia Mizani hubainishwa kwa kiwango na uhusiano kati ya vifundo katika ugawaji kiuwili. Kifundo kimoja huwa chenye nguvu (N) na kingine huwa dhaifu (D). Ubainishi wa kilicho na nguvu au dhaifu hauna uafikiaji wowote wa kifonolojia bali huwa na maana tu kuhusiana na vibainishi vingine katika matawi. Katika neno na mgao wa neno (N) na (D) huonyesha mkazo wenye msikiko zaidi na (D) huonyesha mkazo ulio na msikiko hafifu. Muundo wa ndani wa silabi huwakilishwa na pembe tatu.

Tangulo na fungio huwakilisha msikiko usio na nguvu huku kilele kikiwakilisha msikiko wenye nguvu. Katika Fonolojia Mizani kipashio cha neno kilicho na nguvu zaidi ni kile kilichotawaliwa na (N) kutoka chini hadi juu mwa matawi. Katika uwakilishi wa mizani matawi na ujitokezaji wa kiisimu katika Fonolojia Mizani hubainishwa kwa kiwango na uhusiano kati ya vifundo katika ugawaji kiuwili ambapo kimoja ni chenye nguvu na kingine dhaifu.

### 1.8.2 Misingi ya Nadharia ya Fonolojia Mizani

Nadharia ya Fonolojia Mizani ambayo inatazamiwa kutumiwa katika uchanganuzi wa kazi hii yetu ina misingi ifuatayo:

1. Mfumo na mfuatano wiano wa kimsonge ambao hupanga silabi, maneno na virai katika sentensi kwa kawaida silabi ndicho kiambajengo muhimu, maneno hupangika katika utaratibu wa lugha maalum inayohusika, kwa hivyo silabi zina umuhimu mkubwa sana kwa vile mkazo kwa kawaida huwekwa kwenye kilele cha silabi.

2. Kubainisha uwakilishi wa mkazo katika lugha kwenye viwango vya neno na tungo. Uhakiki wa sauti umejikita katika kigezo cha nguvumsikiko kinachoweza kutofautisha silabi zenye mkazo dhidi ya silabi zisizo na mkazo wa mawimbi ya sauti wakati wa utamkaji. Hii husaidia kujua silabi huanzia wapi na kuishia wapi kwa kutofautisha silabi zenye msikiko mkubwa dhidi ya silabi zisizo na msikiko mkubwa katika neno au kirai.
3. Uhusiano wa matawi. Matawi ya kimizani huwa na uwiani wa kimsikiko ambapo tawi moja huwa na msikiko zaidi kuliko tawi jingine. Tawi lenye msikiko zaidi huwa na nguvu zaidi na hupewa alama ya 'N'ambayo inasomeka kuwa ina nguvu kuliko alama 'H' wakati tawi lile lisilo na msikiko zaidi huwa hafifu kuliko 'N' (Liberman na Prince 1977:257).

### 1.8.3 Mihimili ya Nadharia ya Fonolojia Mizani

Mihimili iliyoongoza utafiti huu ni kwa mujibu wa Prince na Liberman (1977). Nadharia ya Fonolojia Mizani ina mihimili mitatu ambayo tulitumia katika kuafiki malengo ya utafiti huu:

1. Mhimili wa kwanza ambao unasema kuwa "mpangilio msonge ambapo vipengele vya kifonolojia huwakilishwa katika ruzu zilizo katika uhusika wa kimsonge" (Massamba, 2009:208), yaani kuanzia katika vipengele vikubwa zaidi kisha kumalizia katika vipengele vidogo zaidi. Mhimili huu ulisaidia katika kubainisha vipengele vya kiisimu na kuonyesha jinsi vipengele hivyo vinatumika katika kuendelezakazi ya mashairi huru ya Kiswahili ya Kithaka wa Mberia na ya Kezilahabi. Mhimili huu umetumikizwa katika sura ya pili na ya tatu.

2. Pili, mhimili unaosema kuwa kubainisha uwakilishi mkazo katika lugha kwenye viwango vya neno na vilevile katika viwango vya tungo ambapo uchanganuzi wa sauti umejikita katika kigezo cha nguvu-msikiko kinachoweza kutofautisha silabi zenye mkazo dhidi ya silabi zisizo na mkazo kwa mawimbi ya sauti wakati wa utamkaji. Hii husaidia kujua pale ambapo silabi huanzia na pale zinapomalizikia katika kiwango cha neno au kirai. Mhimili huu ulisadia kuonyesha jinsi vipengele vya kiisimu vinavyotumika katika mashairi huru teule ya Kiswahili
3. Mhimili wa tatu unaosema kuwa "uhusiano wa ndani wa silabi huonyeshwa kwa kutumia mizani" (Massamba (2001:207). Aidha Liberman na Prince (1977) walisistiza kauli hii katika kuonyesha uhusiano wa ndani wa silabi mbalimbali zilizomo katika neno au kirai. Mhimili huu ulitusaidia kuonyesha umuhimu wa vipengele vya kiisimu katika kuendeleza kazi ya mashairi huru ya Kiswahili. Mhimili huu umetumikizwa katika sura ya nne.

### 1.9 Mbinu za Utafiti

Kulingana na Kothari (2008) anafafanua kuwa utafiti wowote ule wa kitaaluma ni sharti ufanywe kwa kuongozwa na mbinu mbalimbali za utafiti kwa madhumuni ya kutoa matokeo yasiyo na shaka ndani yake.

Huu ni utafiti wa kimaelezo. Data iliyotumika katika utafiti huu ilikusanywa kutoka kwenye diwani za mashairi zilizoteuliwa. Diwani hizo ni *Msimu wa Tisa*, *Doa*, *Mvumo wa Helikopta*, *Karibu Ndani* na *Kichomi*. Uteuzi wa diwani hizo ulifanywa kwa kutumia mbinu kusudio kwa sababu zinadhihirisha sifa za kiisimu katika kiwango kikubwa.

### 1.9.1 Muundo wa Utafiti

Muundo wa utafiti ni mpango au mkakati wa kiuchunguzi unaokusudiwa kutumiwa ili kupata majibu ya maswali ya utafiti. Aidha, muundo wa utafiti ni seti ya mbinu na hatua ambazo hutumiwa katika kukusanya na kuchanganua vipimo vya vitengo vilivyo maalum kwa suala la utafiti. Muundo kwa jumla ndio utaratibu wa utafiti. Muundo hubainishwa kwa muhtasari wa mambo yatakayoshughulikiwa na mtafiti hatua kwa hatuaa. Muundo wa utafiti hujibu maswali kama; nini? Wapi? Lini? Mbinu zipi?

Utafiti huu ulichukua muundo wa kimaelezo ambapo, maelezo muhimu kuhusu vipengele vya kiisimu ambavyo vilichanganua kazi ya ushairi huru vilivyoshughulikiwa. Kwa mujibu wa Murray (2003) muundo wa utafiti wa kimaelezo ni ule ambao data yake haijachanganuliwa kitakwimu bali huchunguza sifa zinazobainika katika jambo linalochunguzwa. Sifa za kiisimu kama vile aina za sentensi, kipengele cha nafsi na uakifishaji vilishughulikiwa kwa kuyahakiki mashairi kutoka diwani teule.

Maelezo kuhusu wataalamu mbalimbali yalitolewa ili kujenga misingi ya utafiti huu. Vilevile, maelezo kuhusu utafiti kwa ujumla yalitolewa ili kutosheleza mahitaji ya utafiti huu. Mbinu za ukusanyaji data zilizotumika ni uchambuzi matini ambayo yaliwezesha katika kupata data za msingi ambazo zinapatikana maktabani kwa kusoma matini mbalimbali zilizohusiana na mada ya utafiti huu. Halikadhalika kulikuwa na matumizi ya mtandao kwa sababu ya mengi yaliyoandikwa kuhusu mada ya utafiti huu.

### 1.9.2 Mahala pa Utafiti

Utafiti huu ulifanywa kupitita usomaji wa kina maktabani. Ni katika maktaba ndipo tulisoma kuhusu nadharia ya utafiti, mbinu za utafiti, yaliyoandikwa kuhusu mada ya utafiti

na kupata data iliyohitajika ili kuboresha pengo la utafiti, nadharia ya utafiti na mbinu za utafiti. Tulisoma kuhusu nadharia iliyoongoza huu. Data za kimsingi zilitokana na uchanganuzi wa vipengele vya kiisimu katika kazi teule ya mashairi huru yaliyohakikiwa

Vilevile, data ilikusanywa kutokana na tafiti za awali kuhusu uchanganuzi wa kiisimu katika kazi za kifasihi haswa zile zinazohusiana na ushairi huru kutoka katika tasnifu mbalimbali, vitabu, tahakiki mbalimbali kupitia mtandaoni na maktabani.

**1.9.3 Sampuli na Usampulishaji**

Ogula (2005) anaeleza kuwa sampuli ni hali ya kuchagua kikundi kidogo cha watu kutoka kwa idadi kubwa ya watu ambao wanakusudiwa kushiriki katika utafiti.

Sampuli lengwa katika utafiti huu zilikuwa diwani teule za mashairi ya Kithaka wa Mberia na Kezilahabi.

Uteuzi wa watunzi wa mashairi pamoja na diwani zilizoshughulikiwa ulifanywa kwa kutumia mbinu za kimaksudi. Mashairi yaliyoteuliwa kimakusudi yalikuwa na vipengele vifuatavyo: aina za sentensi, uakifishaji na kipengele cha nafsi. Usomaji wa diwani teule za mashairi ulibainisha kuwa diwani zilizoteuliwa zilitosheleza mahitaji ya utafiti huu kwa kuwa na data iliyochanganuliwa kiisNaye Milroy (1987) anaeleza kuwa sampuli kusudio huwa mwafaka pale kundi fulani la watu linaaminiwa kuwa na data inayohitajika katika kuyaafiki malengo ya utafiti

Mashairi sitini yalichanganuliwa kutoka katika diwani teule kwa hivyo jumla mashairi sitini yalishughulikiwa. Uteuzi wa watunzi wa mashairi huru ulifanywa kimaksudi kwa vile ni watunzi maarufu hasa kwa vile wao ni miongoni mwa watunzi na waasisi wa tapo la ushairi huru.

### 1.9.4 Ukusanyaji wa Data

Data ilikusanywa kwa kusoma kwa kina na kwa umakinifu mashairi teule kutoka kwenye diwani za Kithaka wa Mberia na Kezilahabi kwa kunukuu sehemu zenye data iliyohitajika. Diwani teule zilizosomwa ni: *Doa, Mvumo wa Helikopta, Msimu wa Tisa, Karibu Ndani* na *Kichomi*. Vipengelele vya kiisimu ambavyo vilizingatiwa katika usomaji wa kina wa mashairi teule ni: Uakifishaji, aina za sentensi na kipengele cha nafsi. Maneno na mishororo iliyozingatia sifa za kiisimu yalizingatiwa na kuteuliwa ili yafanyiwe uchanganuzi.

Kwa kuongozwa na mihimili ya nadharia ya Fonolojia Mizani, maneno na mishororo iliyozingatia sifa za kiisimu yaliteuliwa na kuchanganuliwa kutegemea aina ya vipengele vilivyobainisha sifa za kiisimu. Vipengele vya kiisimu vilivyodhihirika katika mashairi teule vilielezwa kutegemea wingi wake na kufafanuliwa kwa kuvihusisha na muktadha wa mishororo na shairi nzima.

### 1.9.5 Uchanganuzi wa Data

Kulingana na Kombo na Tromp (2006) wanaeleza kuwa uchanganuzi wa data hutegemea iwapo ni utafiti wa kimaelezo au utafiti wa kihesabu. Data iliyokusanywa ilipangwa kimfumo kulingana na malengo ya utafiti haswa kuanzia katika lengo la kwanza hadi lile la mwisho.

Aidha data iliyokusanywa ilichanganuliwa kwa njia ya kimaelezo kwa kuongozwa na malengo pamoja na maswali ya utafiti, vilevile iliongozwa na mihimili ya nadharia ya Fonolojia Mizani na kwa kuzingatia pengo la utafiti huu. Halikadhalika utafiti huu ulichanganuliwa kwa kuzingatia mbinu ya uhakiki matini

### 1.9.6 Uwasilishaji wa Matokeo

Matokeo ya utafiti huu yaliwasilishwa kwa njia ya kimaelezo na utoaji mifano kwa kuzingatia vipengele teule vya kiisimu vilivyochanganuliwa. Uchanganuzi ulizingatia vipengele vya kiisimu katika kazi ya ushairi huru wa Kiswahili.

Katika kubainisha vipengele vya kiisimu na kuonyesha jinsi vinatumika katika kuendeleza kazi ya mashairi huru katika sura ya pili, utafiti ulitumia mashairi ishirini kutoka katika diwani teule za Kithaka wa Mberia. Aidha, katika kubainisha vipengele vya kiisimu na kuonyesha jinsi vinavyatumika katika kuendeleza mashairi huru ya Kezilahabi katika sura ya tatu, utafiti ulitumia mashairi kumi na manane. Utafiti huu ulitumia mashairi ishirini na mawili katika kueleza umuhimu wa vipengele vya kiisimu kutoka katika diwani teule katika sura ya nne.

### 1.9.7 Maadili ya Utafiti

Kabla ya kufanya utafiti, mtafiti aliomba ruhusa kutoka Chuo Kikuu cha Kenyatta na vilevile, kutoka katika baraza la Taifa la Sayansi na Teknolojia, NACOSTI. Aidha, kazi zozote ambazo zilitajwa kutoka katika tafiti za awali zilirejelewa vilivyo.

## 1.10 Hitimisho

Sura hii imeshughulikia utangulizi wa utafiti ambao unajumuisha vipengele kama usuli wa mada, suala la utafiti, maswala ya utafiti, malengo na maswali ya utafiti, umuhimu wa utafiti, sababu za kuchagua mada, upeo na mipaka ya utafiti, yaliyoandikwa kuhusu mada, misingi na mihimili ya nadharia na mbinu za utafi

# SURA YA PILI

# KUBAINISHA VIPENGELE VYA KIISIMU NA JINSI VINAVYOTUMIKA KATIKA MASHAIRI HURU YA KITHAKA WA MBERIA

## 2.0 Utangulizi

Katika sura hii tumebainisha vipengele vya kiisimu katika mashairi huru ya Kithaka wa Mberia na kuonyesha jinsi vinavyotumika katika kuendeleza kazi ya mashairi huru teule ya Kiswahili. Katika kuchanganua mashairi huru ya Kithaka wa Mberia, tumebainisha vipengele vifuatavyo vya kiisimu: Aina za sentensi, kipengele cha nafsi na uakifishaji. Katika kuchanganua mashairi teule ya Kithaka wa Mberia ambayo ni *Msimu wa Tisa, Doa* na *Mvumo wa Helikopta*. Lengo kuu ni kubainisha vipengele vya kiisimu na kuonyesha jinsi vinavyotumika katika kuendeleza kazi ya mashairi huru ya Kiswahili.Na katika kufanya hivyo, uchunguzi uliongozwa na mihimili miwili ya nadharia ya fonolojia mizani inayosema kuwa: Kwanza, mpangilio msonge ambapo vipengele vya kifonolojia huwakilishwa katika ruzu zilizo katika uhusika wa kimsonge, yaani kuanzia katika vipengele vikubwa zaidi kisha kumalizia katika vipengele vidogo zaidi. Pili, kubainisha uwakilishi mkazo katika lugha kwenye viwango vya neno na pia katika viwango vya tungo ambapo uchanganuzi wa sauti umejikita katika kigezo cha nguvu msikiko kinachoweza kutofautisha silabi zenye mkazo dhidi ya silabi zisizo na mkazo kwa mawimbi ya sauti wakati wa utamkaji.

## 2.1 Aina za Sentensi

Mishororo katika mashairi huru ya Kiswahili hutofatiana kutoka katika ubeti mmoja hadi mwingine. Sentensi katika ushairi tunarejelea kama mishororo au mistari katika lugha ya kishairi. Beti za shairi huundwa kwa kuzingatia aina mbalimbali za mishororo mathalani:

sentensi fupi, sentensi ndefu na sentensi ambazo mishororo haitoshani. Kunazo aina nyingi za mishororo au sentensi kutegemea ujumbe na wazo ambalo linawasilishwa katika ubeti husika. Katika kazi hii, tumejikita kwenye aina tatu za sentensi kama zifautazo:

1. Sentensi ya mishata
2. Sentensi zenye mishororo isiyotoshana
3. Sentensi ndefu

### 2.1.1 Sentensi/Mishororo Mishata

Mishata ni mistari ambayo haijitoshelezi kimaana katika beti za mashairi, mistari hii huwa inategemea mistari mingine inayofuata katika ubeti ili kukamilika kimaana. Sentensi au mishororo mishata katika mashairi huru mara nyingi huwa haikamiliki katika kuleta dhana ya maana pale inapoishia kwenye ubeti. Hii ni kusema kuwa, mishororo ya aina hii haijitoshelezi kimaana katika ubeti. Ili msomaji aweze kupata maana kamili, analazimika kuisoma sentensi inayofuata katika ubeti au hata asome ubetu mzima ili apate maana iliyokusudiwa na mtunzi (Lutomia, 2017).

Mishata inapotumika katika mashairi inaonyesha hali iliyo halisi ya mazungumzo ingawa kwa kutumia njia ya mkato na yenye kunata wasomaji wa kazi husika. Mshairi hupanga mistari yake kwa namna itakayokuwa rahisi kwa hadhira katika kuufasiri ujumbe ambao unakusudiwa na mtunzi wa kazi husika. Kwa kawaida, mistari mishata katika mashairi ya Kithaka wa Mberia imetumika kwa wingi ili kuwasilisha masimulizi yaliyo katika akili yake mtunzi badala ya kutumia lugha ya nathari ambayo inatumika katika tanzu nyingine za kifasihi kama vile hadithi fupi, riwaya na tamthiliya.

Aidha, aina za sentensi hizi bila shaka huanza kwa herufi kubwa. Kwa sababu ya kutokamilika kwa sentensi hizi, humpa msomaji hamu ya kutaka kufahamu maana iliyokusudiwa na mshairi. Kwa mfano, katika diwani hizi mishata imejitokeza kama ifuatavyo:

**Shairi la Hasidi Kijijini:**

*Alipovishwa kofia ya nembo ya mamlaka*
*Waajiri walimtarajia awe dira katika jamii*
*Njiani awaongoze wananchi kwa maadili*
*Wafike nyanda za mwangaza na bashasha*
*Alitazamiwa kuchangia kuleta sura mpya*
*Ili kata ndogo aliyoiongoza isiachwe nyuma*
*Kumbe badala ya kuleta taa katika jamii*
*Angeishi kwa miaka mingi katika utawala*
*Na kisha kuachia kijiji harufu isiyopendeza*
*Kutoka uozo uliokwamiza ndoto za Watoto*
(Kithaka wa Mberia; *Mvumo wa Helikopta* Uk. 48)

Sentensi ya kwanza inadokeza kauli ambayo haikamilishwi papo hapo, lazima sentensi hii iambatanishwe na sentensi ya pili ama ya tatu, ya nne, ya tano na hata na sita ili kukamilisha wazo lililo kamili lililokusudiwa na mshairi. Sentensi au mshororo wa kwanza katika ubeti huu ni mshata kwa sababu haukamilishi wazo isipokuwa lazima uambatanishwe na mishororo inayofuata ndipo ulete maana inayotarajiwa na ya kisarufi.

Aidha, sentensi ya nne, tano, sita na ya saba zinasaidia kukamilisha wazo la kwanza. Vilevile, unaposoma sentensi ya nne, tano, sita na ya saba, unagundua kuwa hazijakamilika kimaana bila kufungamanishwa na sentensi ya kwanza. Kwa mfano, inafaa sentensi ya kwanza ikamilike hivi: “Alipovishwa kofia ya nembo ya mamlaka, waajiri walimtarajia

awe dira katika jamii, njiani awaongoze wananchi kwa maadili ili wafike nyanda za mwangaza na bashasha". Kwa kufanya hivi, ndipo maana inakamilika kisarufi.

Mfano mwingine:

**Shairi la Ardhi yenye Siha na Uchangamfu wa Rutuba**

*Ardhi yenye siha na uchangamfu wa rutuba*
*Imelala usingizi katika kitanda cha maumbile*
*Tukinongenezana. 'Anga linaonea nchi'*
*Tambarare zenye uwezo wa kuhimili mamilioni*
*Zimeachiwa nguchiro, panya, mchwa na nyenze*
*Katika taifa linalotapatapa katika dimbwi la njaa*
(Kithaka wa Mberia; *Msimu wa Tisa*)

Kutokana na ubeti huu kauli ya mshairi katika sentensi ya kwanza na ya pili imekamilika kimaana katika sentensi ya tatu, aidha sentensi ya nne na ya tano maana imekamilika katika sentensi ya mwisho ya ubeti. Unaposoma ubeti mzima ambapo ardhi iliyotarajiwa kuwanufaisha wananchi dhidi ya janga la njaa, badala yake imeachiwa wadudu kama vile mchwa, nguchiro, panya na nyenze ambao ndio wanatawala na kusababishia wananchi ukame na njaa. Sentensi ya kwanza na ya pili ikiambatanishwa kwa mfano: "ardhi yenye siha na uchangamfu wa rutuba imelala usingizi katika kitanda cha maumbile".

Sentensi hii sasa imekamilika kimaana. Sentensi ya kwanza ikiwa pekee yake haina maana na hivyo ni mshata kama ilivyo sentensi ya pili ambayo pia haiwezi jisimamia kimaana isipokuwa pale inapombatanishwa na ya kwanza.

Mfano mwingine:

**Shairi la 20**

*Katika mitaa walimoishi watu kwa amani*
*Jirani alisaka Jirani wa miaka na mikaka*
*Na kwa upanga kumkatakata bila huruma*

*Wanawake walivamiwa na watu waliowajua*
*Waliteswa kwa jinsi isiyoelezeka kwa lugha*
(Kithaka wa Mberia; *Doa* Uk. 80)

Katika utunzi huu, maana ya mshairi katika sentensi ya kwanza na ya pili inapatikana katika sentensi ya tatu ambayo maana ya sentensi ya kwanza na ya pili inaleta ule ukamilifu wake ni kwamba jirani alimsaka jirani ili amkatekate kwa upanga bila huruma. Hii inamlazimu msomaji kusoma ubeti mzima ndipo apate maana inayowasilishwa na mshairi.

Hali kadhalika, sentensi ya nne katika ubeti huu inasaidia kutambua jinsi wanawake walivyoteswa katika sentensi ya tano baada ya kuvamiwa na watu waliowajua. Sentensi ya tano imetumika kama kielezi cha sentensi ya nne kwa sababu imetupa taarifa zaidi kuhusu namna wanawake walivyoteswa kwa kuvamiwa na watu waliowajua.

### 2.1.2 Sentensi zenye Urefu Tofauti katika Beti

Sifa bayana inayodhihirika katika diwani zote za Kithaka wa Mberia ambazo tumezihakiki mathalani: *Msimu wa Tisa*, *Doa* na *Mvumo wa Helikopta* ni kutumia urefu usiotoshana katika sentensi. Watunzi wengi wa mashairi huru katika kazi zao hutumia mishororo au sentensi zisizotoshana katika beti za mashairi yao. Lengo kuu haswa la mtunzi kama huyu ni kujenga ridhimu ambayo ni tofauti toka shairi moja hadi lingine. Ridhimu yenyewe inatokana na jinsi mawazo ya mtunzi yanavyotiririka katika akili yake na jinsi mapigo na muziki vinavyojengeka. Mawazo katika akili ya Kithaka wa Mberia yanathibiti urefu wa mistari katika tungo zao.

Mchanganyiko wa mishororo mirefu na mifupi inasaidia katika kubadilisha kasi na mwendo wa usomaji wa shairi, aidha, mchanganyiko huu hutumika na mtunzi ili kujenga ridhimu na hisia mahususi katika hatua mbalimbali za shairi. Kwa mfano, mistari mifupi katika mashairi huru ya Kiswahili hutumika kwa lengo la kupunguza kasi ya usomaji wa shairi kwa sababu ya kuleta mapumziko katika ubeti wa shairi ambacho ndicho kipengele muhimu cha kiisimu.

Nayo mistari mirefu katika mashairi huru ya Kiswahili inatumika kimakusudi katika kusaidia kuongeza kasi ya usomaji wa shairi na hutoa hisia na fikra nzito zenye utulivu. Mistari mirefu husomwa kwa kasi ikilinganishwa na mistari mifupi ambayo inaelekea kupunguza kasi ya usomaji. Mistari mirefu inaweza ikaunda athari ya kukosa pumzi au uharaka wa shairi haswa pale ambapo viakifishi havijatumika katika kuleta mtuo.

Kwa mfano:

**Shairi la**: **Kikaragosi**

*Ulijikweza angani na kujieka baina ya binadamu na nyota (silabi 24)*
*Uliona dunia kama kinyago katika mkono wako imara (silabi 23)*
*Watu walipopaza sauti ya kite uliwavunja mafuvu kwa rungu (silabi 23)*
*Kama Malaika wa mauti hufurahia nyimbo za Matanga (silabi 21)*
(Kithaka wa Mberia; *Msimu wa Tisa* Uk. 79)

Katika kifungu hiki, urefu wa sentensi unatofautiana kutoka mshororo mmoja hadi mwingine. Hii inadhihirika kupitia idadi ya silabi katika kila mshororo. Hii inaonyesha mtiririko wa mawazo katika fikra za mshairi ambayo hawezi kujifunga katika kanuni za utunzi zinazoweza kumfanya asiwasilishe mawazo yake anavyokusudia.

Kwa mfano, mshairi ametumia mstari wa kwanza mrefu mbao una silabi nyingi kuliko sentensi zingine bila kipumuo ili kuibua hisia nzito zinazokusudiwa na mtunzi anapozungumzia kuhusu mhusika aliyejikweza na kujieka baina ya binadamu na nyota.

Vilevile, mtunzi ametumia mstari mfupi katika sentensi ya nne anaposema “kama Malaika wa mauti hufurahia nyimbo za Matanga”. Mstari huu mfupi umedokeza kauli ya huzuni kubwa ambayo haieleweki moja kwa moja.

Kwa jumla Kithaka wa Mberia ametumia urefu wa sentensi ambazo hazilingani kwa kuzingatia mizani au silabi katika kila sentensi. Hii imempa mtunzi huyu kuiwasilisha kazi yake kwa njia iliyo huru bila kujifinya kwa sheria za kiarudhi kama vile utoshelezi wa mizani katika kila mshororo au mistari inayotoshana katika kila ubeti n.k.

Mfano mwingine*:*

**Shairi la 25**

*Kwa wafichwao chini ya mivungu ya vitanda (silabi 15)*
*Kufurahia kucheza juani na Watoto wenzao (silabi 18)*
*Linaonekana jambo lililo mbali isiyofikika (silabi 19)*
*Kupata tajriba iwe dira ya kuwaongoza maishani (silabi 21)*
*Ni njia iliyozibwa kwa kuchimbwa mtaro wa kina (silabi 18)*
(Kithaka wa Mberia; *Doa* Uk. 101)

Kithaka wa Mberia ametumia mchanganyiko wa sentensi ndefu na fupi katika ubeti huu kama ilivyo kwenye shairi hili. Ametumia sentensi fupi katika sentensi ya kwanza “kwa wafichwao chini ya mivungu ya vitanda”, sentensi hii ni fupi ikilinganishwa na sentensi ya nne, mtunzi huyu amefanya hivi kimakusudi ili kuwafanya wasomaji wa kazi hii kuhisi uwepo wa mambo yasiyoweza kuelezwa akirejelea watu ambao hajawataja moja kwa moja.

Aidha, Kithaka ametumia sentensi ndefu ambayo ni: “kupata tajriba iwe dira ya kuwaongoza maishani”. Ameeleza sentensi hii kwa mapana ili kuwasilisha maudhui yenye hisia nzito na kuwawezesha wasomaji wa kazi hii waelewe fungu hili bila kutatizika.

Mtunzi wa kazi hii ametumia urefu wa sentensi ambazo hazilingani katika ubeti kwa kuzingatia mizani au silabi katika kila sentensi. Hii imempa mtunzi uhuru kuiwasilisha kazi yake kwa njia iliyo huru bila kujifinya kwa sheria za kiarudhi kama vile utoshelezi wa mizani katika mishororo na nyinginezo nyingi.

Mfano mwingine:

**Shairi la Hatima ya Masahibu**

*ilisimama kwa afya iliyochangamsha macho (silabi 17)*
*kwa ujasiri ambao haukuhitaji ufafanuzi (silabi 19)*
*ilikaribiana na kuta za mawe, vioo na vyuma (silabi 18)*
*ikazilainisha na kuleta utuvu kwa mpita-njia, (silabi 20)*
*kwenye matawi, ndege waliishi kwa amani (silabi 15)*
*wadudu walishangilia ukarimu uliowazingira (silabi 20)*
*chini vivulin iambavyo havikujua ubahili (silabi 18)*
*barubaru na mabanati walifinyanga urafiki (silabi 18)*
*baadhi walifumiana hadithi za rangi pendezi (silabi 19)*
*nyoyo zikang’ara kabla ya kuingia masomo (silabi 17)*
(Kithaka wa Mberia; *Mvumo wa Helikopta* Uk. 15)

Katika ubeti huu wa shairi, mtunzi ametumia urefu wa sentensi usiolingana pale anapozingatia idadi ya mizani au silabi katika mishororo ambayo ni tofauti toka mshororo mmoja hadi mwingine kwa mfano katika sentensi ya kwanza mshairi ametumia silabi 17, ikilinganishwa na sentensi ya pili ambayo ina silabi 19 kisha sentensi ya tatu ina silabi 18. Huenda mtunzi alifanya hivyo kimakusudi ili kuwasilisha maudhui yake katika shairi hili linalohusu hatima ya mashahibu, mtunzi alikusudia kuchanganya sentensi ndefu na fupi

katika ubeti wa shairi hili ili aweze kutimiza lengo lake la kuwasilisha maudhui yake kwa njia iliyo huru bila kujifunga kwa sheria za kiarudhi. Kwa ufupi tumebaini kuwa Kithaka wa Mberia ametumia sentensi zisizotoshana katika kuendeleza maudhui ya kazi yake bila kuzingatia kanuni za kiutunzi.

### 2.1.3 Sentensi Ndefu

Sentensi ndefu zinapotumika katika mashairi huru ya Kiswahili, huwa zinalenga kuafiki mtetemo unaodorora kwa sababu ya toni kama vile; toni ya huzuni, toni ya unyonge au hata toni ya furaha. Kwa kawaida, sentensi ndefu huchukua nafasi kubwa na ndefu katika ukurasa. Sentensi ndefu zinapotumika katika shairi huongeza kasi ya shairi. Mara nyingi, sentensi ndefu hutoa vizuri hisia zenye utulivu na fikra pana. Sentensi ndefu katika shairi lenye hisia nzito huwekwa vipumuo ili kupunguza kasi na hivyo huweza kuibua hisia zinzazokusudiwa, hata hivyo kuna baadhi ya sentensi ndefu katika mashairi ambazo haziwekwi vipumuo.

Kwa mfano:

**Shairi la Wakala wa Kaburi**

*Milioni kwenye siri haramu, furaha kwa waporao mashirirka ya walipaji kodi*
*Kusambaratika kwa huduma za umma, kuporomoka miradi ya taifa, machozi*
*Kwenye akaunti za makuwadi wa serikali, milioni zisizohesabika, ujenzi wa makasri*
*Milioni zisizohesabika zilizofichwa katika nchi za nje, mijengo Ulaya na Marekani*
(Kithaka wa Mberia; *mvumo wa Helikopta* Uk. 26)

Katika ubeti wa shairi hili, mshairi ametumia sentensi ndefu ndefu hasa katika beti zote, sentensi hizi ndefu zina vipumuo katikati na mtunzi amekusudia kufanya hivyo ili kumwezesha msomaji kutua anaposoma kazi yake na pia kuwasilisha hisia nzito kuhusu walioshika doria ya uongozi wanavyotumia mamlaka mali ya umma kujinufaisha naa

kuekeza mamilioni ya fedha kwenye nchi za Ulaya na Marekani. Mtunzi huyu alieleza hayo kwa upana kwa kutumia sentensi ndefu ili msomaji asipate changamoto za kuelewa ujumbe uliokusudiwa kuwasilishwa tofauti na vile ambavyo labda angetumia sentensi fupi zilizojaa lugha ya mkato.

Mfano mwingine:

**Shairi la Waharifu Huru**

*Bila kutarajiwa, onyo za mashambulizi dhidi ya wageni*
*Zilipaa na kuchafua anga kama harufu ya amonia*
*Vilifuata vijinga vikipulizwa na pumzi hatari za wanasiasa*
*Taya za miako zilitafuna mbao, fenicha, nguo na vyeti*
*Maghala ya vyakula na matumaini ya kesho yenye shibe*
*Yalifutiliwa mbali na upepo wa wendawazimu wa kupangwa;*
*Kutoka mikononi mwa fukara walioleweshwa kwa chuki*
*Mishale ilipiga mbizi katika miili ya wakazi wa makabila mengine*
*Panga za ghadhabu zilishuka baina ya vichwa na viwiliwili*
*Vituo vya biashara vilivyonawirishwa kwa Maisha ya heshima*
*Vilichomwa na kubakia magofu yenye mwangwi wa huzuni;*
(Kithaka wa Mberia; *Msimu wa Tisa* Uk. 30)

Katika utunzi huu, mshairi amekamilisha wazo alilolianza katika sentensi ya kwanza kwenye sentensi ya pili na hivyo kuifanya iwe sentensi moja ndefu yenye vipumuo na iliyokamilika kimantiki na kisarufi kwa mfano, “bila kutarajiwa, onyo za mashambulizi dhidi ya wageni zilipaa na kuchafua anga kama harufu ya amania”. Mshairi ametumia sentensi ndefu katika ubeti huu kusimulia jinsi wenyeji walivyoshambulia watu wa makabila mengine na kuchoma maghala yao na vibanda vyao vya biashara na kuwaacha wakiwa hawana pa kuenda. Ametumia hizi sentensi ndefu ili kumwezesha msomaji wa

kazi yake kupata ujumbe kwa mapana na kwa njia inayoeleweka rahisi bila kutazika kama alivyokusudia mtunzi.

Mfano wa mwingine:

**Shairi la 18**

*Wanyonge ni adui wakubwa wa wanyonge*
*Kwa kuchochewa kwa kauli bila mashiko*
*Huwageukia wenzao walioloa uchochole*
*Huwatumbukiza katika bwawa la madhila*
(Kithaka wa Mberia; *Doa* Uk. 71)

Katika utunzi huu, mshairi amekamilisha wazo alilolianza katika sentensi ya kwanza na ya pili kwenye sentensi ya tatu na hivyo kuifanya iwe sentensi moja ndefu yenye vipumuo na iliyokamilia kimantiki na kimaana. Kwa mfano, sentensi uinaunganishwa na kusomeka kama: "wanyonge ni adui wakubwa wa wanyonge kwa kuchochewa kwa kauli bila mashiko, huwageuka wenzao walioloa uchochole." Mshairi ametumia sentensi hii ndefu katika kuelezea jinsi wanyonge walivyo adui wa wanyonge wenzao kwani wakiwa katika shida ata wanyonge wenzao hawana uwezo wa kuwaokoa. Mshairi huyu ametumia sentensi ndefu katika ubeti huu ili kumwezesha msomaji wa kazi yake kupata ujumbe aliokusudiwa kwa mapana na kwa njia inayoeleweka rahisi.

## 2.2 Uakifishaji

Katika sehemu hii, tumeangalia baadhi ya viakifishi mbalimbali katika mashairi huru teule na jinsi viakifishi vyenyewe vinavyotumika katika kuendeleza mshairi teule. Mifano mahususi imetolewa kutoka katika mashairi ya diwani teule za Kithaka wa Mberia mathalani*: Msimu wa Tisa, Doa* na *Mvumo wa Helikopta*.

Jambo muhimu katika kuelewa ni kwamba mashairi huru yametopewa sana falsafa. Hii inatokana na sababu kuwa watunzi wa mashairi huru ya Kiswahili hudadisi mambo kwa njia ya kitaaluma, hivyo mashairi yao aghalabu hutumia viakifishi mbalimbali ili kusistiza mambo kama vile maudhui na vilevile katika kuunganisha fikra na mawazo ili kuleta muwala na mshikamano katika kazi zao na kuwezesha wasomaji wa kazi zao kuelewa wanachokusudia.

Watunzi wengi wa kazi za kifasihi wanatumia viakifishi mbalimbali katika kuwasilisha kazi zao, hii ndiyo kanuni muhimu katika utunzi wowote ule. Lengo kuu la kufanya hivi ni kunasa hisia za wasomaji na kudhibiti mwendo wa usomaji wa kazi husika.

Kwa mujibu wa Maitaria (2012) viakifishi hutaka usomaji na upokezi wa ujumbe ubainike zaidi kwa kuzingatia uelekezi wa ishara hizo. Hadhira inaweza kusoma mashairi kwa mwendo unaoafiki matarajio ya mshairi. Aidha, matumizi ya viakifishi mbalimbali katika kazi ya mashairi huru hutumiwa ili kuvunja mfululizo wa kauli.

Katika ushairi huru wa Kiswahili aghalabu watunzi huwasilisha kazi zao kwa lugha iliyoakifishwa kama tu zilivyo tanzu zingine za fasihi. Uwasilishaji wa kimantiki huzingatiwa ili kubainisha matini zilizotumika na kuondoa utata haswa katika kufasiri ujumbe uliokusudiwa. Watunzi hutumia viakifishi mbalimbali kama mtindo na mbinu ya kibinafsi katika kuwasilisha kazi zao za ushairi.

Katika usomaji wa mashairi huru, njia ya kuupokea ujumbe ni kupitia kwenye matini zilizoakifishwa na mtunzi wa kazi husika. Viakifishi mbalimbali vimeshirikishwa katika kubainisha ujumbe kwa malengo ya kuwasiliana na hadhira vizuri. Miongoni mwa

viakifishi ambavyo vimetumiwa na watunzi wa kazi za mashairi huru ni pamoja na: Nukta (.), nukta mbili nukta mkato, koma, mabano, herufi kubwa, alama za mtajo, alama za hisi, alama za viulizi miongoni mwa viakifishi vingine. Viakifishi hivi vinaweza kutumiwa ndani kwa ndani katika beti za shairi au kwenye kingo au mwishoni mwa beti na mishororo.

Mfano wa kwanza:

**Shairi la Gamba la Mtu**

***Ku**mbe udhaniacho kimekutana na mboni za macho*
***S**i sharti kiwe maji ya kukufaa; labda ni mazigazi:*
***N**iliyemwona kuwa mwaminifu, nikataja tuliyopanga*
***N**i maarufu wa kuahidi kumbe kwa ahadi za uzandiki!*
(Kithaka wa Mberia; *Mvumo wa Helikopta*, Uk. 72)

Katika ubeti wa shairi hili, mtunzi ametumia viakifishi kama vile: herufi kubwa, koma, alama za kunukuu na alama za hisi ipasavyo. Ametumia herufi kubwa katika kila mwanzoni mwa mshororo kama ilivyo katika sarufi ya lugha pale ambapo sentensi hupaswa kuanza kwa herufi kubwa.

Aidha, mshairi ametumia alama ya hisi (!) mwishoni mwa ubeti kutekeleza kimalizio katika ubeti, hoja iliyokamilika na kama mbinu ya kuleta utaharuki ili kumpa msomaji hamu ya kuendelea kusoma beti nyingine za shairi hilo. Halikadhalika mshairi ameweza kutumia koma (,) katika mstari wa tatu ili kudokeza kauli ya ukinzani pale ambapo tunaona sehemu ya kwanza ya sentensi ambayo ni “niliyemwona kuwa mwaminifu” inaonyesha hali ya mtunzi alivyokuwa amemwamini mwenzake na hivyo akampa siri zake, kisha sehemu ya pili ya sentensi inaleta kinyume na matarajio ya mtunzi (Wamitila, 2002).

Aidha, mtunzi ametumia koma kumwezesha msomaji kupunguza kasi ya usomaji wa sentensi hiyo ndefu kwa kutua baada ya kusoma sentensi au kishazi kilichotangulia.

Mfano mwingine:

**Shairi la 11**

*Kwa wasichana na wanawake makamo*
*Ni sawa na kuvuka mto wa mamba:*
*Askari wa jeshi la malkia wa Buckinam*
*Huwapiga kumbo na kuwabwaga chini*
*Dhuluma inayofuata, haitajiki kwa lugha!*
(Kithaka wa Mberia*; Doa* Uk. 46)

Katika shairi hili mshairi ametumia viakifishi vichache katika kukidhi mahitaji yake ya uwasilishaji. ibainike kuwa wakati viakifishi viwili ambavyo ni (: na!) vinatumika hurejelea sehemu mbili muhimu. Katika mshororo wa pili "ni sawa na kuvuka mto wa mamba:" na katika mshororo wa mwisho: "dhuluma inayofuata, haitajiki kwa lugha." Mtunzi amefanya hivi kimakusudi ili kumfanya msomaji wa kazi hii asome shairi lote kwanza na kisha kufuatilia matukio yaliyojiri huko Buckinam huku akisaili na kutafakari kila kauli katika mshororo hadi pale ukingoni au mwisho wa ubeti.

Mfano mwingine:

**Shairi la Msumbuji**

*Maisha ya kutemewa mate ya dharau*
*Miongo ya miiba mikali nyonyoni*
*Majira ya vibunga vichwani*
*Uamuzi wenye mashiko:*
*Dawa ya moto ni moto!*
(Kithaka wa Mberia; *Msimu wa Tisa* Uk. 71)

Katika ubeti wa shairi hili, mshororo wa mwisho unaosema “dawa ya moto ni moto!” kuna matumizi ya alama ya hisi ambayo imetumiwa na mshairi kudhihirisha toni na hali ya huzuni na machozi. Alama hii ya hisi imetumika na mtunzi katika shairi hili ili kutilia mkazo ujumbe anaotaka ufikie hadhira yake kwa njia ya msisitizo, kwa mfano walichukua silaha na kupigana na maadui wao.

Ukizingatia shairi lenyewe unaona kuwa linahusu ulipizaji wa kisasi haswa baada ya wahusika kufanyiwa madhila na wenzao na hivyo wanapanga njama ya kulipiza mabaya na hii inaonekana kupitia huo mshororo wa mwisho. Huu ni mfano wa shairi la kiharakati ambalo kwa namna fulani linataka watu wazinduke na wachukue hatua inayostahili ili kupigana na maadui kusudi wapate uhuru na mali zao zilizonyakuliwa.

Aidha kuna matumizi ya koloni katika sentensi ya nne inayodokeza hivi “uamuzi wenye mashiko:”, kauli hii ya mtunzi inaonyesha toni yenye huzuni ya msimulizi baada ya kufanyiwa madhila. Kwa jumla, tuseme kuwa viakifishi vilivyotumika katika ubeti huu vinaashiria toni ya huzuni na machozi miongoni mwa warejelewa wanaoazimia kulipisha kisasi kwa dhuluma walizofanyiwa.

### 2.3 Kipengele cha Nafsi

Tumezingatia nafsi katika sehemu mbili ambazo ni nafsi neni na nafsi nenewa kisha tukachanganua nafsi hizi kuzingatia usarufi wake kwa kuangazia nafsi tatu za Kiswahili ambazo ni nafsi ya kwanza, nafsi ya pili na nafsi ya tatu.

Nafsineni pia inarejelewa kama pasona ama yule mzungumzji katika shairi au kazi yoyote ile ya fasihi. Nafsineni sio mtunzi wa kazi husika bali ni mhusika ambaye huteuliwa na

mwandishi ambaye anapewa jukumu la kuwasilisha ujumbe. Mshairi anaweza kutumia nafsi ya mtu yeyote kutoa ujumbe wake. Haijalishi umri, jinsia, cheo au hali ya kiuchumi (Arege, 2016).

Nafsineni inamwezesha mtunzi kuweka msomaji katika hali na hisia fulani ili kuweka wazi kile kinazungumziwa. Mwandishi anaweza kuzungumzia janga la virusi fulani na athari zake, hii haimanishi kuwa huenda mtunzi ameathirika na virusi hivyo mwenyewe bali kuna uwezekano huenda mtunzi aliathirika na hali hiyo kama waandishi wengine wa kazi za kifasihi, mtunzi huyu ana uhuru na haki ya kubadilisha yaliyomkumba na kuyapa sura nyingine yenye ubia kusudi aweze kutoa funzo kwa watu wengine ili wasije wakakumbana na hali kama hiyo aliyokuwa nayo mtunzi. Katika kazi zingine unaweza kupata mtunzi anataja jina lake au mahali na mazingira anamoishi yeye mwenyewe. Katika hali ya uhalisia ya maisha huonyesha sauti katika shairi husika.

### 2.3.1 Nafsi ya Kwanza

Katika kiwango cha simulizi hizi, mshairi anatumia kiwakilishi cha nafsi ya kwanza kwa kutumia mofu ‘ni’ au ‘na’katika umoja na mofu ‘tu’ katika wingi kisha viwakilishi ‘mimi na sisi’ katika umoja na wingi kurejelea nafsi na njeo mtawalia ya msemaji.

Mfano wa shairi:

**Shairi la Roshani**

*Sitembei na kupanda ngazi kuitafuta rafiki yangu Roshani*
*Nifunguapo mlango, nakaribishwa kwa pepezi za sahibu*
*Ndilo agizo nililoweka mikononi mwa msarifu nyumba*
*Akatekeleza vyema, mjenzi akatimiza hadi maridhiko*

(Kithaka wa Mberia; *Mvumo wa Helikopta* Uk. 62)

Katika shairi hili, nafsineni ni sauti ya msimulizi, huenda mtunzi akawa anarejelea nafsi ya kwanza akiwa anajirejelea yeye mwenyewe wakati anaisifu Roshani yake ambayo ndiye rafiki yake wa kumkaribisha kila siku afunguapo mlango wa nyumba yake. Maneno kama hayo: 'sitembei', 'nifunguapo', 'nakaribishwa' yanabainisha wazi viambishi vya nafsi ya kwanza katika umoja kupitia usimulizi wake. Aidha, nafsi ya kwanza katika wingi inabainika kupitia shairi lifatalo;

**Shairi la Kimbunga cha Misiba**

*Matembeleano yangali kwenye kumbukumbu*
*Familia zetu zilikutana na kuchangamkiana*
*Tulikula mezani moja tukijenga utangamano*
*Tulikunjua hadithi tukimulika sura za maisha*
*Ukawepo urafiki mbali na uhusiano wa damu*
*(*Kithaka wa Mberia; *mvumo wa Helikopta)*

Katika ubeti wa shairi hili, mtunzi amerejelea wanenaji au sauti ya wasemaji kwa kutumia nafsi ya kwanza katika wingi. Amefanya hivyo kwa kutumia mofu 'tu' kupitia maneno kama vile; "tulikula, tulikunjua" ambayo yanaashiria nafsi ya kwanza katika wingi. Kwa hivyo, wasomaji wa kazi hii wanaposoma wanatambua kuwa warejewa ni wahusika katika miongoni mwa wengine ndio wanenaji katika ubeti huu na mtunzi wa shairi hili ni mmoja wao.

### 2.3.2 Nafsi ya Pili

Kwa kawaida inaporejelea nafsi ya pili, huwa na matumizi ya mofu 'u' na 'm' katika umoja na wingi au viwakilishi 'wewe' na 'nyinyi' kurejeleo njeo. Nafsi ya pili katika ushairi ina athari kubwa kwa wasomaji kwa kuwa inanuia kuwaleta wasomaji hao karibu kwa kuwahusisha na matukio yanayorejelewa. Tazama mfano ufuataο:

**Shairi la Rose**

*Mkasa katika jiji lililozoea ulaini wa amani*
*Msimu wa vita baina ya hilali na mwewe*
*Kwa siku tano chini ya kandamizoza mawe na chuma*
*Rose, ulijisatiti katika uwanda utengao hai na wafu*
*Ukipigana vita kwa nguvu imara za mwili na akili*
*Sauti yako ya shujaa ilipopanda na kufikia waokoaji*
*Ilichanganya machovu na dhamira thabiti ya kuishi*
*(*Kithaka wa Mberia; *Msimu wa Tisa uk 33)*

Katika shairi hili limeonyesha wazi matumizi ya nafsi ya pili katika umoja. Rose ndiye mhusika ambaye alijisatiti kupigana vita kwa nguvu imara kwa mwili na akili hadi kupaza sauti iliyowafikia waokoaji na hivyo akaokolewa kutoka katika mauti yaliyokuwa yamemwandama.

Rose ametumiwa na mtunzi huyu kuwasilisha kipengele hiki cha nafsi ya pili. Haya yanadhihirika kupitia mofu au viambishi vya viwakilishi vifuatavyo katika maneno yafuatayo: 'ulijisatiti' 'ukipigana', katika maneno haya, mofu 'u' imetumika kuonyesha nafsi ya pili katika umoja. Halikadhalika, mtunzi wa kazi hii amedhihirisha matumizi ya nafsi ya pili katika wingi kupitia mfano wa shairi lifuatalo;

**Shairi la Firimbi**

*Kwa ujasiri kama tumba la jua*
*Mlipanda kilimani mkapiga mbiu*
*Kwa maneno wazi kama firimbi*
*Mkaarifu umma kwa angani*
*Kunapepea bendera nyekundu*
*Kitambaa chenye nembo ya fuvu*
*Ishara ya mamlaka ya virusi sugu*

(Kithaka wa Mberia; *msimu wa Tisa* Uk. 83)

Mshairi anawarejelea kundi la watu waliokuwa na ujasiri kwa kupanda milima na kupiga firimbi kwa kuarifu watu wengine kuhusu janga la virusi sugu vilivyokuwa vimezuka katika mazingira yao. Nafsi ya pili katika wingi imedhirishwa kupititа mofu 'm' kwenye maneno kama vile "mlipanda, mkaarifu". Msomaji wa kazi hii anapoisoma atabaini kuwa bila shaka warejelewa ni watu zaidi ya mmoja walio katika nafsi ya pili wingi kwa kurejelea mofu 'm'.

### 2.3.3 Nafsi ya Tatu

Katika nafsineni ya tatu, mtunzi ametumia mofu 'a' katika umoja na mofu 'wa' katika wingi kuelezea matukio mbalimbali kuwahusu wahusika warejelewa.

Kwa mfano:

**Shairi la 7**

*Alikuwa mtu Madhubuti kimawazo*
*Aliposhika wadhifa muhimu serikalini*
*Alihudumu kwa mafanikio yaliyon'gara,*
*Alikuwa mahiri katika kuzalisha mali*
*Biashara zake za kitalii na shule*
*Zilikuwa za kuonewa Fahari na wananchi*
(Kithaka wa Mberia; *Doa* Uk. 31)

Mshairi katika shairi hili anarejelea sifa nzuri za maendeleo ya mrejelewa ambaye amefanyia wananchi maendeleo katika kata yake pindi tu aliposhika hatamu ya uongozi. Mtunzi ametumia mofu 'a' kuonyesha kuwa nafsi inayorejelewa ni ya tatu katika umoja, hii inabainika kupitia viambishi vya viwakilishi katika maneno kama 'alikuwa',

‘aliposhika’, ‘alihudumu’ na kadhalika. Halikadhalika, matumizi ya nafsi ya tatu pia yamebainika vizuri kupitia mfano wa shairi lifuatano:

Aidha, nafsi ya tatu katika wingi imedhihirika kupitia mfano ufuatao:

**Shairi la 15**
*Wakubwa waliopambwa kwa nembo mabegani*
*Wangepunguza sinzio kazini na kuamsha akili,*
*Wangetilia maanani jukumu la kuhifadhi uhai*
*Wangetuma kazini wanasare waliokolea ujuzi*
*Maisha ya vijana bila tajriba ya kujenga mauko*
*Hayangemezwa na mchanga dudumizi wa mauti*
*(*Kithaka wa Mberia; *Doa uk 64)*

Mshairi katika ubeti huu ameweza kuonyesha kuwa warejelewa katika ubeti huu ni watu zaidi ya mmoja ambao walipopata madaraka walisinzia kazini na kutotilia maanani jukumu la uhai kwa kujenga mauko katika maisha ya vijana yaliyosalia yenye dhiki na uchochole. Mtunzi ametumia mofu ‘wa’ kupitia maneno kama vile “waliopambwa, wangepuuza, wangetilia” kuonyesha nafsi ya tatu katika wingi ya warejelewa katika ubeti huu.

Mfano mwingine:

**Shairi la Hasidi Kijijini:**
*Alipovishwa kofia ya nembo ya mamlaka*
*Waajiri walimtarajia awe dira katika jamii*
*Njiani awaongoze wananchi kwa maadili*
*Wafike nyanda za mwangaza na bashasha*
*Alitazamiwa kuchangia kuleta sura mpya*
*Ili kata ndogo aliyooingoza isiachwe nyuma*
*Kumbe badala ya kuleta taa katika jamii*
*Angeishi kwa miaka mingi katika utawala*
*Na kisha kuachia kijiji harufu isiyopendeza*

*Kutoka uozo uliokwamiza ndoto za Watoto*
*(*Kithaka wa Mberia; *Mvumo wa Helikopta)*

Shairi hili linalohusu mrejelewa ambaye alikuwa amechukua hatamu ya uongozi katika kata ndogo, tunaona wananchi wakiwa na matumaini tele kuwa huenda angewakopoa ama kuwakomboa kutoka katika lindi la ufukara, mambo ambayo yalitimia kinyume na matarajio yao. Nafsi ya tatu imejitokeza vizuri kupitia mofu 'a' katika maneno kama 'alipovishwa', 'alitazamiwa' na 'angeishi'.

Aidha, mtunzi pia amedhihirisha nafsi ya tatu katika wingi kupitia mfano ufuatao:

**Shairi la Wasomi wa Jana 11**
*Walimwaga jasho wakapata vyeti vya umahiri*
*Waliweka usingizi kando wakikimbiza uzamivu*
*Wakishangiliwa walipiga magoti wakavishwa*
*Walivishwa kofia mviringo umma ukiwaajabia*
*Kwa miaka walitia wanafunzi mwanga vyuoni*
*Walipoona mishahara ya angani ya wanasiasa*
*Walijitosa katika vumbi la mieleka mikali ya kura*
*Wakabwaga washindani, wakabebwa wakiimbiwa.*
*(*Kithaka wa Mberia; *Mvumo wa Helikopta uk 88)*

Katika kuendeleza kazi hii ya ushairi huru, mtunzi ametumia nafsi ya tatu katika wingi kuonyesha kuwa wanaorejelewa ni watu wengi, watu hawa ni wasomi waliotia bidii katika masomo yao hadi kupata shahada ya uzamivu kisha baadaye wakajitosa kwenye siasa na kunyakua viti vya uongozi. Watu hawa wanarejelewa kama wengi kupia mofu 'wa' katika maneno kama "walimwaga", "waliweka", "wakishangiliwa" n.k".

Kwa jumla, ni bayana kuwa Kithaka wa Mberia amezingatia usarufi au isimu katika kurejelea kipengele cha nafsi katika wingi na umoja kama ilivyo katika sarufi ya Kiswahili.

## 2.4 Hitimisho

Katika sura hii utafiti umebainisha vipengele vya kiisimu katika mashairi huru ya Kiswahili kutoka katika diwani za Kithaka wa Mberia ambazo ni: *Msimu wa Tisa, Doa* na *Mvumo wa Helikopta*. Aidha, kwa kubainisha vipengele hivi vya kiisimu, tuliweza kuonyesha jinsi vipengele vyenyewe vinatumika katika kuendeleza kazi ya mashairi huru ya Kiswahili. Vipengele vya kiisimu vilivyobainishwa ni: Aina za sentensi, uakifishaji na kipengele cha nafsi.

Katika uchanganuzi huu, mtafiti alibaini kuwa, vipengele vya kiisimu vinatumika sana katika kazi za mashairi jinsi ambavyo vinategemeana na kushirikiana pakubwa. Huru kwa kiwango kikubwa. Hii imedhihirisha kuwa huwezi kutenganisha isimu na fasihi kwa

# SURA YA TATU

# KUBAINISHA VIPENGELE VYA KIISIMU NA JINSI VINAVYOTUMIKA KATIKA KUENDELEZA KAZI YA MASHAIRI HURU YA KEZILAHABI

## 3.0 Utangulizi

Katika sura hii utafiti umebainisha vipengele vya kiisimu katika mashairi huru ya Kezilahabi ambayo ni *Kichomi* na *Karibu Ndani* na kuonyesha jinsi vinavyotumika katika kuendeleza kazi ya mashairi huru teule ya Kiswahili. Katika kuchanganua mashairi huru ya Kezilahabi, mtafiti amebainisha vipengele vifuatavyo vya kiisimu: Aina za sentensi, kipengele cha nafsi na uakifishaji. Katika kuhakiki mashairi huru teule ya Kezilahabi, lengo kuu ni kubainisha vipengele vya kiisimu na kuonyesha namna vinavyotumika katika mashairi huru ya Kiswahili. Uchanganuzi huu uliongozwa na mihimili miwili ya nadharia ya fonolojia mizani inayosema kuwa: Kwanza, mpangilio msonge ambapo vipengele vya kifonolojia huwakilishwa katika ruzu zilizo katika uhusika wa kimsonge, yaani kuanzia katika vipengele vikubwa zaidi kisha kumalizia katika vipengele vidogo zaidi. Pili, kubainisha uwakilishi mkazo katika lugha kwenye viwango vya neno na pia katika viwango vya tungo ambapo uchanganuzi wa sauti umejikita katika kigezo cha nguvu msikiko kinachoweza kutofautisha silabi zenye mkazo dhidi ya silabi zisizo na mkazo kwa mawimbi ya sauti wakati wa utamkaji.

## 3.1 Aina za Sentensi

Kiisimu kuna aina tatu za sentensi ambazo ni: sentensi sahili, sentensi ambatani na sentensi changamano. Na katika uhakiki wa mashairi, aina hizo za sentensi huwa na umuhimu tofauti. Kwa hivyo utafiti huu umehakiki aina zingine za sentensi zinazopatikana katika

ushairi ambazo ni: sentensi ndefu, sentensi za mishata na sentensi zenye urefu unaotofautiana katika beti.

Mishororo katika mashairi hutofautiana kutoka ubeti mmoja hadi mwingine. Tunaposema sentensi katika ushairi tunarejelea mishororo au mistari katika lugha ya kishairi. Beti za shairi huundwa kwa kuzingatia aina mbalimbali za mishororo.

Kunazo aina nyingi za mistari au sentensi kutegemea ujumbe na wazo ambalo mtunzi wa kazi husika anawasilisha katika ubeti husika. Katika utafiti huu, mtafiti amejikita kwenye sentensi mbalimbali kama vile; sentensi za mishata, sentensi zenye urefu usiotoshana katika beti na sentensi ndefu kama zifautazo:

### 3.1.1 Sentensi/Mishororo Mishata

Sentensi za mishata katika mashairi huru ni sentensi ambazo huwa hazikamiliki katika kuleta maana pale inapoishia kwenye ubeti, hii ni kusema kuwa sentensi za aina hii hazijitoshelezi kimaana katika ubeti. Ili msomaji aweze kupata maana kamili, matumizi ya sentensi ndefu katika ubeti aghalabu mizani huwa mirefu kama ilivyo katika mashairi ya mtunzi huyu.

Mizani ikiwa mirefu, shairi katika mtetemo wake hudororа yaani linakwenda taratibu. Mara nyingi shairi likiwa la furaha, mizani au mapambano huenda kwa mtetemo wa haraka na yale ya msiba na huzuni hudororа (Mohamed, 1990). Aidha, matumizi ya sentensi fupi fupi katika mashairi huru huwa na kauli fupi fupi kwa kuzingatia mizani michache Sentensi zikiwa fupi, shairi linapata mtetemo wa haraka haraka. Kwa kawaida, msomaji wa mashairi yenye mshororo mifupi na mirefu katika ubeti huwa analazimika kuzisoma sentensi zinazofuata katika ubeti ili apate maana iliyokusudiwa na mshairi.

Kwa kawaida, aina za sentensi hizi aghalabu huanza kwa herufi kubwa. Kwa sababu ya kutokamilika kwa sentensi hizi, humpa msomaji hamu ya kutaka kufahamu maana iliyokusudiwa na mshairi kwa kuendelea kuusoma hata ubeti mzima wa shairi. Kwa kawaida sentensi za mishata hujenga taharuki. Kwa mfano, katika diwani hizi mishata imejitokeza kama ifuatayo:

Mfano wa Shairi:

**Wimbo wa Kunguni**

*Mwanadamu kama hajui*
*Ndoa ni mkono karibu na goli*
*Na firimbi imelia*
*Golini hamna mtu*
*Lakini goli upana fupi moja*
*Viatu vimechanika na mpira na tofali*
*Uwanja kijiji ndani ya nyumba*
*Washangiliaji na wazomeaji wengi sana*
(Kezilahabi; *Kichomi,* Uk. 20)

Sentensi ya kwanza imedokeza wazo ambalo halijakamilika kimaana. Sentensi hii ya kwanza ni mshata kwa kuwa haijakamilisha wazo ila imedokeza tu kauli inayosema: “mwanadamu kama hajui”. Kwa hivyo, lazima msomaji asome sentensi ya pili na ya tatu ili apate wazo kamili. Sentensi ya pili imekamilisha wazo lilidokezwa katika sentensi ya kwanza na hivyo inasaidia kuziba pengo kwa vile inaeleza kile ambacho mwanadamu hajui katika sentensi ya kwanza ambacho kinafafanuliwa katika sentensi ya pili kuwa ndoa ni mkono karibu na goli.

Aidha, sentensi ya tatu ni mshata kwa sababu maana yake inakamilika kupitia sentensi ya nne hadi ya mwisho ndipo tunapata wazo kamili. Hivyo basi, sentensi hizi ni mishata kwa

sababu haziwasilishi wazo lililokamilika kimaana zikiwa pekee yake ila lazima ziunganishwe na zingine katika ubeti. Maana inakamilika baada ya kusoma hata kifungu chote.

Mfano mwigine:

**Shairi; Chai ya Jioni**

*Wakati tunywapo chai hapa upenuni*
*Na kuwatazama Watoto wetu*
*Wakicheza bembea kwa furaha*
*Tujue Kamba ya bembea yetu*
*Imeshalika na imeanza kuoza*
*Na bado kidogo tutaporomoka*
(Kezilahabi; *Karibu Ndani* Uk. 3)

Katika ubeti wa shairi hili, maana inayokusudiwa na mtunzi inapatikana katika sentensi ya nne na ya tano. Hii ni kusema kuwa sentensi ya kwanza, ya pili na ya tatu haziridhishi kwa vile hazileti maana yoyote isipokuwa katika sentensi ya nne na ya tano. Sentensi ya kwanza ni mshata kwa vile haikamiliki kimaana. Hakuna wazo kamili kwa kudokeza tu kuwa wakati warejelewa wanywapo chai ya jioni pale upenuni. Msomaji anatarajia kujua ni nini kilichofuata wakati watu hawa walipokuwa wakinywa chai pale kwenye upenu, hii inambidi msomaji kuendelea kusoma sentensi zinazofuata ili ajue kilichotendeka.

Aidha, sentensi ya pili na tatu vilevile ni mishata kwa sababu hazijabainisha wazo lililo kamili hadi pale katika sentensi ya nne na ya tano ambazo zinakamilisha maana iliyodokezwa katika sentensi ya pili na ya tatu. Sentensi ya nne na tano zinasaidia wasomaji kujua kwamba bembea ya warejelewa imeshalika na kuoza na kisha kuporomoka ukirejelea sentensi ya mwisho.

Mfano mwingine:

**Shairi la Hatumwoni**

*Kateni yote misitu, fimbo tuenee*
*Na vinyago tuwachomge Watoto wachezee.*
*Kausheni yote maziwa maji tuwalowanishe*
*Kukipambazuka wasiweze ruka angani.*
*Kokeni mioto, mashujaa wa uonevu tuwabanike.*
*Kamwe hapatakuwa na kilio wala Matanga*
*Bali hoi za ushindi na Madaraka kwa umma.*
(Kezilahabi; *Karibu Ndani* Uk. 31)

Katika ubeti huu wazo la mtunzi katika sentensi ya kwanza linakamilika katika sentensi ya pili. Sentensi hii ya kwanza ni mshata kwa sababu mtunzi anaposema "kateni yote msitu, fimbo tuenee", msomaji anaposoma mstari huu, hawezi kuelewa haswa baada ya misitu kukatwa ni nini kingetokea. Sentensi ya pili, ya tatu, ya nne, ya tano na ya sita ndipo yale yaliyofanyika yanaelezwa kupitia sentensi hizi, kwa mfano, watoto walifaa kuchongewa vinyago vya kuchezea miongoni mwa vitu vingine. Kwa hivyo, msomaji lazima asome sentensi zingine zote baada ya kusoma ya kwanza ili aweze kujua maana ya mtunzi kwa sababu sentensi hizi zinatupa majibu ya sentensi ya kwanza haswa kwa kueleza sababu za kwa nini misitu ikatwe

### 3.1.2 Sentensi zenye Urefu Tofauti katika

Sifa muhimu inayodhihirika katika diwani zote ambazo tumezichanganua mathalani: Kichomi na Karibu Ndani ni kutumia urefu usiolingana wa sentensi. Watunzi wengi wa mashairi huru katika kazi zao hutumia mishororo au sentensi zisizotoshana katika beti za mashairi yao. Nia kuu la mtunzi kama huyu ni kuazimia kujenga ridhimu ambayo ni tofauti

kutoka shairi moja hadi lingine. Ridhimu yenyewe inatokana na jinsi mawazo ya mtunzi yanavyotiririka katika akili yake na jinsi mapigo na muziki yanavyojengeka. Hivyo, urefu wa sentensi usiotoshana katika beti ndicho kigezo cha kipekee cha kuabainisha ridhimu katika usomaji wa mashairi huru ya Kiswahili.

Mawazo katika akili ya Kezilahabi yanathibiti urefu wa mistari katika tungo zake.

Kwa mfano:

**Shairi la Bikira mwenye Huzuni**

*Miaka kumi ya uchovu (silabi 10*

*Mapenzini na msichana (silabi 9)*

*Aliyeishi pangoni (silabi 8)*

*Ilikuwa imepita kwa huzuni (silabi 12)*

*Halafu buibui, kanisa, alikuwa (silabi 14)*

*Amekwisha wasomea kitabu cha zamani (silabi 15)*

*Na kusema aliweza kumwoa: lakini (silabi 14)*

*Bila, kwa nguvu (silabi 5)*

*Za shetani, kwanza (silabi 6)*

*Kuvunja ule wavu wa uchawi. (silabi 11)*

(Kezilahabi; *Kichomi* Uk.3)

Katika ubeti huu wa kwanza wa shairi hili, urefu wa sentensi unatofautiana kutoka mshororo mmoja hadi mwingine. Katika ubeti huu, mshairi ametumia mchanganyiko wa sentensi ndefu na fupi kwa mfano: sentensi ya tatu inayosema "aliyeishi pangoni" ni mfano wa sentensi fupi zaidi ikilinganishwa na sentensi zingine katika ubeti husika ambayo ina silabi sita, katika sentensi ya mwisho, nayo ni ndefu sana kuliko zingine zote katika ubeti huu. Hii inadhihirika kupitia idadi ya silabi kwenye mistari katika kila mshororo.

Matumizi ya sentensi fupi katika ubeti huu inasaidia kupunguza kasi ya usomaji wa shairi lenyewe. Hii ni kwa sababu wasomaji wanalazimika kuweka vipumuo kila baada ya sentensi kama hizi fupi katika usomaji wao. Katika ubeti huu, matumizi ya mistari mifupi imefungamana vizuri na shairi hili ambalo lina uzito wa hisia. Matumizi ya sentensi fupi katika ubeti huu inaonyesha mtiririko wa mawazo katika fikra za mshairi.

Katika ubeti wa pili wa shairi hili, vilevile sentensi zinatofautiana kutoka sentensi moja hadi nyingine. Kwa mfano, sentensi ya pili ina silabi kumi na tano (15) tofauti na sentensi zingine zilizo na idadi fupi ya siilabi kama vile sentensi ya tano iliyo na silabi tano (5) ambazo ni chache mno. Mtunzi ametumia sentensi ndefu zenye vipumuo ili kuongeza kasi ya usomaji wa ubeti huu. Kwa mfano, sentensi ya tatu inayosema: "na kusema aliweza kumwoa; lakini", sentensi hii ni ndefu na imetumika pamoja na kipumuo ambacho ni nukta mkato (;). Kwa hivyo, msomaji anaposoma ubeti huu, anatua kwa kuongozwa na nukta mkato. Kwa hivyo, sentensi hizi ndefu zimetumika ili kusaidia kuzitoa hisia zenye utulivu, fikra pana na mawazo kwa njia iliyo huru.

Kwa jumla matumizi ya sentensi zenye urefu usiolingana katika beti za shairi hili zinaashirira mtiririko wa mawazo katika fikra za mtunzi huyu. Hivyo, mtunzi anapata uhuru wa kuwasilisha kazi yake kwa hadhira kwa njia ilyo huru bila kujifinya kwenye sheria za utunzi.

Mfano mwingine:

**Shairi la Kifo cha Mende Wekundu**

*Na ujenge yako nyumba, jingi jasho likuoshe (silabi 16)*

*Ufyeke, upime na uweke nguzo (silabi 12)*

*Kisha paa uweke na ukandike (silabi 12)*

*Siku nyingi bila kuingiliwa na mgeni hutakaa (silabi 19)*

*Wataanza kutalii mipaka mende usiku,*
*Nje na ndani ya nyumba watazunguka*
*Bila woga, bila ruhusa ulichonacho watakula,*
*Masalia yatakuwa yako, ijaranya kaziyo.*
(Kezilahabi; *Karibu Ndani* Uk. 33)

Halikadhalika, katika ubeti wa shairi hili mtunzi ametumia urefu wa sentensi ambazo hazilingani kwa kuzingatia mizani au silabi katika kila sentensi. Kwa mfano, mshairi ametumia sentensi ya nne yenye silabi kumi na tisa (19), ambayo ni ndefu zaidi kuliko sentensi zote katika ubeti huu. Mshairi amefanya hivi kimakusudi ili kutoa mawazo yake mapana akimwonya mrejelewa kuhusu umuhimu wa kuua mende ili asije kupata aibu endapo angetembelewa na mgeni. Urefu wa sentensi hii unayafanya mapigo ya mizani yadorore na kwa hivyo, limechukua mtetemo wa utaratibu ambao unawiana vizuri na ujumbe kuhusu mashaka yaliyoletwa na mende wekundu kwa mhusika.

Aidha, mtunzi wa kazi hii ametumia mistari mifupi miwili wa pili na wa tatu yenye silabi kumi na mbili katika kila mstari, amefanya hivi katika kuorodhesha hatua ambazo mrejelewa anastahili kuchukua ili kuwaua mende kama vile kufyeka, apime, aweke paa na nguzo na akandike.

Jambo linalodhihirika katika beti hizi mbili ni kuwa urefu huu unakaribiana sio tu katika beti hizi mbili bali katika shairi lote. Kwa mfano, ukiangalia ubeti wa pili una silabi kumi na nane katika sentensi ya tatu kisha silabi kumi na saba katika sentensi ya mwisho. Hii ni njia moja ya kudumisha wizani na muwala katika shairi lote kwa kulifanya shairi lisomeka au liimbike.

Urefu usiolingana katika ubetI umejitokeza kimakusudi kwa kufuata utaratibu maalum wa mtunzi. Katika kutumia mistari isiotoshana katika beti hizi mbili imempa mtunzi huyu kuiwasilisha kazi yake kwa njia iliyo huru bila kujifinya kwa sheria za kiarudhi kama vile utoshelezi wa mizani katika kila mshororo katika ubeti.

### 3.1.3 Sentensi Ndefu

Kwa kawaida, sentensi ndefu huchukua nafasi kubwa na ndefu katika ukurasa. Sentensi ndefu zinapotumika katika shairi huongeza kasi ya shairi. Mara nyingi sentensi ndefu hutoa vizuri hisia zenye utulivu na fikra zilizo pana. Sentensi ndefu katika shairi lenye hisia nzito huwekwa vipumuo ili kupunguza kasi na hivyo huweza kuibua hisia zinzazokusudiwa. Hata hivyo, kuna baadhi ya sentensi ndefu katika mashairi ambazo haziwekwi vipumuo.

Kwa Mfano:

**Shairi la Watoto Wawili**

*Mtoto wa tajiri akilia hupewa mkate*
*Mtoto wa tajiri akilia hupewa picha kuchezea*
*Akiendelea kulia hupanda mgogngo wa yaya*
*Akikataa kunyamaza ulimwengu mzima hulaumiwa*

*Mtoto wa maskini akilia hula mchanga*
*Mtoto wa maskini akilia hupewa mti kuchezea*
*Akilia mtoto wa maskini huvutwa kashani*
*Akiendelea kulia hupanda mgongo wa mama ulio uchi*
*Akikataa kunyamaza wazazi husikitika kimya kimya*

(Kezilzhabi; *Kichomi* Uk. 63)

Huu ni mfano wa shairi lenye sentensi ndefu zisizo na vipumuo. Mtunzi ametumia mistari au sentensi ndefu bila vipumuo ili kuwasilisha ujumbe kuwahusu watoto wawili wanaotoka katika matabaka mawili tofauti ili kuelezea jinsi watu walio na uwezo maishani wanavyoishi maisha mazuri tofauti na wale wa tabaka la chini wanaoishi maisha ya taabu na dhiki.

Mfano mwingine:

**Shairi la Kujifunza Kuendesha**

*Nilijiona simba nimepanda, na manyoya nimeshika*
*Nikachomoka kundi kuelekeala vitungi-tumbo*
*Nikaviona vinatapatapa na vingine vikijililia:*
*Nitakupa pesa! Nipe Maisha mwaka! Sitanyonya!*

*Nilijiona angani, tai nimepanda, miguu nimeshika.*
*Tai akiranda akinyonyoa manyoya ya waliotakata*
*Wengine nikiwakatakatakwa makali ya yangu kalamu*
*Vichwa vikidondoka, ndimi bado zikijikililia: Ya Rabi!*

(Kezilahabi; *Karibu Ndani* Uk. 29)

Vilevile, hili ni shairi lenye mfano wa matumizi ya sentensi au mishororo mirefu, mshairi ametumia alama ya kuakifisha ya koloni baada ya sentensi ya tatu ‘Nikaviona vinatapatapa na vingine vikijililia:’ katika kudokeza sentensi kama hii mwandishi alikuwa na nia ya kuendeleza sentensi yake na kwa kufanya hivyo sentensi hiyo inakamilika kwa sentensi ya nne, alifanya hivi kimakusudi ili kuwasilisha ujumbe kwa hadhira kwa mapana na kurahisisha kuelewa.

Aidha, katika ubeti wa pili mshairi ametumia sentensi ndefu ndefu zenye vipumuo vinavyosaidia katika kupunguza kasi ya usomaji wa ubeti huu na hivyo kuibua hisia nzito kwa mapana kama zilivyokusudiwa na mtunzi. Ametumia sentensi hizi fupi kumrejelea msimulizi ili kuwasilisha ujumbe wake wenye hisia, fikra na mawazo mapana kuhusu mrejelewa aliyejiona akiwa angani amepanda kama tai akirandaranda akiwanyanyasa wengine kwa kuwakatakata kwa makali ya kalamu yake.

Mtunzi alitumia sentensi hizi ndefu katika ubeti huu kimakusudi ili aweze kuwasilisha maudhui ya kazi yake kwa hadhira kwa njia iliyo na uhuru bila kujikita kwenye kanuni za kiutunzi na alikwepa kujikita kwenye lugha ya mkato kama ilivyo katika mashairi ya kimapokeo.

### 3.2 Uakifishaji

Matumizi ya viakifishi ni moja wapo ya sheria muhimu katika utunzi wa mashairi ya Kiswahili. Lengo kuu la kutumia viakifishi katika utunzi wa mashairi ya Kiswahili ni kuwezesha katika uwasilishaji wa ujumbe kwa jinsi inayonasa na kunata akili na hisia za hadhira ili kudhibiti kasi ya usomaji wa mashairi huru ya Kiswahili.

Kulingana na Maitaria (2012), viakifishi huutaka usomaji na upokezi wa ujumbe ubainike zaidi kwa kuzingatia uelekezi wa ishara hizo mbalimbali za uakifishaji. Kwa hivyo, wasomaji wa kazi husika huweza kuyasoma mashairi kwa mwendo ambao unaafiki matarajio ya mtunzi. Aidha, viakifishi hutumika ili kuvunja mfululizo wa kuusoma ujumbe unaowasilishwa na mtunzi.

Katika ushairi huru wa Kiswahili mara nyingi watunzi huwasilisha kazi zao kwa lugha ilyoakifishwa kama tu zilivyo tanzu zingine za fasihi kama vile; riwaya, tamthiliya na

hadithi fupi. Uwasilishaji wa kisiimu huzingatiwa ili kubainisha matini zilizotumika na kuondoa utata katika kufasiri ujumbe uliokusudiwa na mtunzi wa kazi husika. Watunzi hutumia viakifishi mbalimbali kama mtindo na mbinu ya kibinafsi katika kuwasilisha kazi zao za ushairi. Matumizi ya alama za uakifishaji ni mapana na kutokana na nia ya kuwasilisha maudhui kwa ukamilifu.

Katika sehemu hii, tumeangalia baadhi ya viakifishi mbalimbali vilivyotumika katika utunzi wa mashairi huru teule ya Kezilahabi na jinsi viakifishi vyenyewe vinavyotumika katika kuendeleza kazi ya mshairi Kiswahili. Mifano imetolewa kutoka kwa mashairi ya diwani teule za Kezilahabi mathalani: *Karibu Ndani* na *Kichomi.*

Katika usomaji wa mashairi huru, njia ya kuupokea ujumbe ni kupitia kwenye matini zilizoakifishwa na mtunzi wa kazi husika. Viakifishi mbalimbali vimeshirikishwa katika kubainisha ujumbe kwa malengo ya kuwasiliana na hadhira vizuri. Miongoni mwa viakifishi ambavyo hutumia na watunzi wa kazi za mashairi huru ni pamoja na: Nukta, nukta mbili, nukta mkato, koma, mabano, herufi kubwa, alama za mtajo, alama za hizi, alama za viulizi n.k. viakifishi hivi vinaweza kutumiwa ndani kwa ndani katika beti na mishororo za shairi au kwenye kingo/mwishoni mwa beti na mishororo.

Mfano wa kwanza*:*

**Shairi la Mwamba Ziwani**

***H**autingisiki, hauzungumzi**:** umekufa**;***

***L**akini ninaweza kuusikia ukizungumza**:***

***"**Kijana mimi sciheki, uwe hivyo na wewe.*

***T**azama jinsi ndege walivyokifanya kichwa changu*

***C**heupe kama mchwa na fuvu, mimi nimetulia,*

***S**ina wasiwasi ingawa naonekana mjinga*

***M**awimbi yananigusa na kuvunjika*

***K**ama upanga wa muuwaji ushindwavyo kwa roho.*

***M**imi ni imara na sihamishiki*

***N**a mtu mwovu siumiziki**."***

(Kezilahabi; *Kichomi: mwamba ziwani* Uk. 6)

Ubeti wa shairi hili umetumia viakifishi mbalimbali ambavyo vinasaidia kuifanya matini ya shairi hili kueleweka kisarufi na msomaji. Mfano: katika mstari wa kwanza "Hautingisiki, hauzungumzi…." Mshairi ametumia viakifishi vingi ambavyo ni: herufi kubwa. Herufi kubwa zimetumika katika kila mwanzoni mwa mshororo kuonyesha mianzo ya sentensi. Pili, ametumia ishara ya mkato (,) kuonyesha uorodheshaji na kutenganisha mfululizo na mfuatano wa matukio, tatu, ametumia koloni (:) kuashirira kutenganishwa kwa hoja kuu ya kwanza kabla ya dondoo na maelezo yanayohitajika. Nne, ametumia nusu koloni (**;)** kuonyesha hoja nzito na kuu inayohusiana na ile iliyotangulia na pia inaashiria kinachounganisha hoja hizo mbili zinazofuatana. Tano, kuna matumizi ya nukta (.) ambayo imetumika kuashiria miisho ya vifungu na kukamilika kwa wazo katika sentensi. Sita, mshairi ametumia alama za mtajo ("") kuashiria maneno au kauli ambayo sio ya mtunzi yani maneno ya mtu mwingine. Katika ubeti wa shairi hili, mtunzi anadokeza kuwa hiyo

sio kauli na huenda anawataka wasomaji kukabiliana na matini hizo kwa nafsi ya mtu mwingine. Mfano mwingine:

**Shairi la Chai ya Jioni**

*Kulikuwa na wakati ulinisukuma juu*
*Nikaenda zaidi ya nusu duara;*
*Kulikuwa na wakati nilikudaka*
*Ulipokaribia kuanguka,*
*Na kulikuwa na wakati tulibebwa kwa zamu*
*Mmoja wima akisukuma mwingine amekaa.*
*Wakati huo, japo tulipaa mbele na nyuma*
*Tulicheka kwa matumaini yaliyotiwa chumvi.*
*Na kisha tukaongozana jikoni kupika chajio;*
*Ilikuwa adhuhuri yetu.*
*(*E. Kezilahabi; *Karibu Ndani, uk 3)*

Kwa kuzingatia viakifishi vilivyotumika ambavyo ni: herufi kubwa, kikomo, koma na nusu mkato, mshairi amepania kuwasilisha mawazo yake hatua baada ya hatua kwa utaratibu. Mishororo imejitokeza kuzingatia awamu. Herufi kubwa imetumika kuashiria mianzo ya mishororo kwa mfano kila mshororo umeanza kwa herufi kubwa kwa mfano kupitia maneno kama “Kulikuwa, Nikaenda, Ulipokaribia, Mmoja, Wakati, Tulicheka”.

Nacho kitone kimetumika kuonyesha mwisho wa sentensi au mstari. Kwa mfano, baada ya sentensi ya mwisho “ilikuwa adhuhuri yetu”, kuna kitone mwishoni mwa sentensi ili kuoyesha kukamilia kwa wazo ama kuonyesha mwisho wa sentensi ilikamilika kimaana. Koma (,) imetumika kuorodhesha matukio na mawazo ya mtunzi haswa pale anapodokeza mishororo kwa kusema “kulikuwa na wakati.” Katika sentensi ya kwanza, ya tatu na ya tano.

Nukta mkato imetumika kutoa ufafanuzi zaidi haswa baada ya sentensi ya pili "Nikaenda zaidi ya nusu duara;" mtunzi amefanya hivi kimakusudi ili kuonyesha kuwa kuna ufafanuzi wazo alilolitanguliza na hivyo, analifafanua katika sentenzi zinazofuata ili kutoa hisia za mshairi alivyokusudia. Katika ubeti huu msomaji anapofikia kiakifishi hiki, anafaa kutua kidogo kisha aendelee kusoma sentensi zingine kwa malengo ya kutaka kujua yaliyotokea baadaye.

### 3.3 Kipengele cha Nafsi

Utafiti huu umezingatia nafsi tatu za Kiswahili ambazo ni nafsi ya kwanza, nafsi ya pili na nafsi ya tatu. Nafsineni pia inarejelewa kama pasona ama yule mzungumzji katika shairi au kazi yoyote ile ya fasihi. Nafsineni sio mtunzi wa kazi husika bali ni mhusika ambaye huteuliwa na mwandishi ambaye anapewa jukumu la kuwasilisha ujumbe. Kwa mujibu wa Arege (2016) mshairi anaweza kutumia nafsi ya mtu yeyote kutoa ujumbe wake. Haijalishi umri, jinsia, cheo au hali ya kiuchumi.

Nafsineni inamwezesha mtunzi kuweka msomaji katika hali na hisia fulani ili kuweka wazi kile kinachozungumziwa. Mwandishi anaweza kuzungumzia janga la virusi fulani na athari zake, hii haimanishi kuwa huenda mtunzi ameathirika na virusi hivyo mwenyewe bali kuna uwezekano huenda mtunzi aliathirika na hali hiyo kama wandishi wengine wa kazi za kifasihi, mtunzi huyu ana uhuru na haki ya kubadilisha yaliyomkumba na kuyapa sura nyingine yenye ubia kusudi aweze kutoa funzo kwa watu wengine ili wasije wakakumbana na hali kama hiyo aliyokuwa nayo mtunzi.

Katika kazi zingine unawezapata mtunzi anataja jina lake au mahali na mazingira anamoishi yeye mwenyewe. Katika hali ya uhalisia ya maisha huonyesha sauti katika shairi

husika. Katika kazi hii tumeweza kuangazia nafsi katika viwango vitatu: kiwango cha kwanza ni nafsi ya kwanza, nafsi ya pili na nafsi ya tatu mtawalia.

### 3.3.1 Nafsi ya Kwanza

Katika kiwango cha simulizi hizi, mshairi anatumia kiwakilishi cha nafsi ya kwanza kwa kutumia mofu 'ni' au 'na'katika umoja na mofu 'tu' katika wingi kisha viwakilishi 'mimi na sisi' katika umoja na wingi mtawalia kurejelea nafsi na njeo mtawalia ya msemaji. Nafsi ya kwanza katika umoja imedhihirika kupitia mfano wa ubeti ufuatao:

**Shairi la Kujifunza Kuendesha**

*Nilijiona tembo nimepanda, na masikio nimeshika*
*Mkonga ukifyeka vyao vikwazo vya siri*
*Vingine vikikanyagwa vikijililia:*
*Nitakupa pesa! Nipe mwaka Maisha! Sitanyonya!*
(Kezilahabi; *Karibu Ndani* Uk. 29)

Katika ubeti wa shairi hili, mtunzi ametumia nafsi ya kwanza katika umoja kuashiria kuwa msemaji wa maneno huenda akawa mtunzi ama ametumia mtu mwingine lakini katika nafsi ya kwanza, huyu ni mtu mmoja na amewasilishwa kwa kutumia mofu 'ni' katika maneno kama vile "nilijiona, nikatupa" msomai wa kazi hii ataweza kufahamu kuwa mrejelewa katika ubeti huu ni mtu mmoja aliye katika nafsi ya kwanza. Halikadhalika, mtunzi ametumia nafsi ya kwanza katika wingi wakati anapowaonya au kuwatahadhari wenzake kuhusu hatari iliyowakodolea macho katika ubeti wa shairi lifuatalo:

**Shairi la Chai ya Jioni**

*Wakati* ***tu****nywapo chai hapa upenuni*
*Na kuwatazama Watoto wetu*
*Wakicheza bembea kwa furaha*

***Tu**jue Kamba ya bembea yetu*

*Imeshalika na imeanza kuoza*

*Na bado kidogo **tu**taporomoka*

(Kezilahabi*; Karibu Ndani uk 3*)

Katika shairi hili, nafsi ya kwanza katika wingi imedhihirika kupitia kiambishi au mofu 'tu' katika maneno kama vile 'tunywapo na 'tujue'. Mshairi kupitia nafsi ya kwanza amejiweka miongoni mwa wengine ambao anawasihi wajitahadhari kuhusu yale ambayo huenda yakawapata ama kutokea baadaye.

Mfano mwingine:

**Shairi la Kichwa na Mwili**

*Ningekuwa askari ningeoga damu na maji,*
*Ningepasua vichwa na kuchana matumbo,*
*Ningekanyaga kicwa cha msaliti au mhaini*
*Ili kuitwa mume wa wanaume*
*Ningekuwa wa kwanza kutimiza malalamiko ya watu,*
*Wa kwanza kuona hatari ingawa wa mwisho kuiogopa*
*Ningekuwa askari wa haki, ama, na mapenzi duniani.*

(Kezilahabi; *Kichomi* Uk. 16)

Katika ubeti wa shairi hili, mtunzi ametumia nafsi ya kwanza umoja kwa kuzingatia mofu 'ni' katika maneno "ningekuwa na ningepasua" kuashiria kuwa msemaji wa maneno haya yuko katika nafsi ya kwanza umoja. Vilevile, nafsi ya kwanza katika wingi inabainika kupitia mfano wa ubeti ufuatao:

**Shairi la Kuchambua Mchele**

*Chenga na mchango vikawa vingi sana*
*Tukapika baada ya muda mrefuwa kazi:*
*Tukaanza kula,*
*Tukakuta bado mchanga na chenga!*

*Lini tutaula bila mchanga, bila chenga?*
(Kezilahabi; *Kichomi* Uk. 63)

Katika ubeti huu wa shairi, mtunzi yeye pamoja na wengine wanajirejelea wakati wanopolalamika kuhusu mchele waloula ambao ulikuwa umejaa mchanga na chenga. Nafsi hii inajidhihirisha kupitia mofu 'tu' katika maneno kama vile "tukapika, tukaanza na tukakuta". Hii inaonyesha nafsi ya kwanza katika wingi.

### 3.3.2 Nafsi ya Pili

Aghalabu tunaporejelea nafsi ya pili, tunatumia mofu 'u' na 'm' katika umoja na wingi mtawalia au viwakilishi 'wewe' katika umoja na 'nyinyi' katika wingi kurejeleo njeo. Nafsi ya pili katika ushairi ina athari kubwa kwa wasomaji kwa kuwa inanuia kuwaleta wasomaji hao karibu kwa kuwahusisha na matukio yanayorejelewa.

Tazama mfano ufuatao:

**Shairi la Hadija**

*Hadija*
***U**mekata mti mtima*
*Umeangukia nyumba yao.*
*Umeziba mto hasira*
*Nyumba yako sasa mafurikoni*
*Na utahama*
(Kezilahabi; *Kichomi* Uk. 22)

Katika shairi hili mtunzi anamrejelea Hadija ambaye ndiye mrejelewa yani nafsi nenewa. Wakati anapokejeli Hadija kwa kukata miti na kusababisha mafuriko na maafa mengine tunaona mshairi anarejelea viambishi viwakilishi vya nafsi ya pili kupitia kauli zifuatazo: 'umekata', 'umeziba', 'utahama' n.k. ametumia mofu 'u' kumrejelea Hadija ambaye alijisababishia majanga yanayomkumba leo hii.

Mfano mwingine:

**Shairi la Mzee na Mzigo**

*Haya piteni! Piteni haraka! Heei!*
*Mwafikiri mwaniacha nyuma!*
*Njia ya Maisha ni moja tu.*
*Huko mwendako ndiko nilikotoka*
*Na nilipopafika wengi wengi hawatafika*
(Kezilahabi; *Kichomi* Uk. 38)

Hili ni kundi la watu lililo katika nafsi ya pili wingi, wanaonywa dhidi ya kwenda wanakokwenda, nafsi ya pili katika wingi imebainishwa kupitia maneno "mwafikiri, mwendako, wengi wenu, hii inabainisha wazi kuwa kundi linalorejelewa ni watu wengi ambao wanashauriwa wapite kwenda ambako msimulizi alikofika tayari. Watu hawa wamerejelewa katika nafsi ya pili wingi kuonyesha kuwa sio mtu mmoja bali wengi.

Mfano mwingine:

**Shairi la Karibu Ndani**

*Karibu ndani asema, hapa hujawa mgeni*
*Tumekuwa tukisubiri, umefika mapema*
*Umo ndani ya duara, ukinaswa nasika*
*Ulipo umezingirwa, kumbukumbu zilokufinyanga*
*Hapa ulisafisha zako, fizi, kwenye titi la mama*
*Na huyu ndiye mbwa, aliyekulamba kidevu*
*Ingia sasa ngomani, ufunge fundo la kitali.*
(Kezilahabi; *Karibu Ndani* uk. 36)

Ubeti wa shairi hili unaohusu mgeni ambaye anashawishiwa aingie ndani na wenyeji wake haswa baada ya kusubiriwa kwa muda mwingi hatimaye amewasili. Nafsi ya pili inabainika kupitia mofu 'u' kwenye maneno kama vile "umo, ulipo, ulipoingia miongoni mwa mengine" hii inaonyesha kuwa mtunzi amewasilisha ujumbe wake kupia nafsi ya pili ya msemaji.

Mfano mwingine:

**Shairi la Mbegu**

*Wavina nudhumu imewapwaya*
*Waiteni wa jadi waje kitali waone.*
*Zana zenu mikuki na mawe!*
*Bunduki mwaziona bado mwataka shambulia!*
*Mtazikwa kwenye majumba ya makumbusho!*
*Na juu ya yenu makaburi, tutaandika*
*Wasahairi wa mapokeo!*
(Kezilahabi; *Karibu Ndani* Uk. 23)

Kupitia kifungu hiki, mtunzi ametumia nafsi ya pili katika wingi kupitia mofu ‘m’ katika maneno kama “zenu, mwaziona, mtazikwa”

### 3.3.3 Nafsi ya Tatu

Katika nafsi ya tatu, mtunzi anatumia mofu ‘a’ au “yeye” ambayo inaonyesha kwamba mrejelewa ni mtu ni mmjoja wala sio kundi la watu. Katika wingi, mofu ‘wa’ au “wao” kuonyesha wingi yaani kundi la watu ambao wanarejelewa.

Shairi la Matumaini

*Akiyumbayumba*
*Na sarawili zee mawinguni*
*Kama mlevi mwenye mguu mmoja, nilimwona*
*Akitoka magharibi Kwenda mashariki*
*Kisha, akaanguka baharini kwa kishindo.*
*Binadamu tukasubiri. Tukasubiri*
*Alafu baharini ndege katoka*
*Karuka ju mawinguni*
*Wengine wakasema: Ndiye!*
*Wengine: Siye!*
*Tukasubiri.*

(Kezilahabi; *Karibu Ndani* Uk. 7)

Nafsi ya usimulizi katika shairi hili ni nafsi ya tatu katika umoja pale mshairi anaporejelea mrejelewa huyu kwa kutumia mofu ‘a’ katika maneno yafuatayo: ‘akiyumbayumba’, ‘akitoka’, wakati msomaji anapopatana na mofu hizi kama viambishi vya viwakilishi anatambua kuwa nafsi inayorelewa ni ile ya tatu yani ‘yeye’.

Mfano mwingine:

**Shairi la Moshi Ukizidi Pangoni**

*Moshi ukizidi pangoni, wakaidi hujujumuka*
*Wakabanana mlangoni, nyoyo zikawapapatika*
*Moshi ukizidi pangoni, wakaidi nje hutoka*
*Wakaona yam wanga fani, wakakubali kufunzika*
*Wakakubali kubaini, mambo yanayowazunguka,*
*Lakini (*E. Kezilahabi; *Karibu Ndani uk 11)*

Katika ubeti huu, nafsi ya tatu katika wingi imejitokeza kupitia maneno kama “wakabanana, wakaona, wakakubali” kupitia maneno haya, mofu ‘wa’ imetumika kuashiria kuwa maneno haya yametumika kurejelea nafsi ya tatu ya wasemaji.

Mfano mwingine

**Shairi la Mto wa Haki**

*Alipepea hewani! Kama kidefu cha kabaila.*
*Alinepanepa kama kiboko cha mjerumani.*
*Alijipepea kama bendera ya mwingereza:*
*Suti ju yake, elimu kichwani na pesa mfukoni.*
(Kezilahabi; *Kichomi* Uk. 17)

Huu ni ubeti wa shairi ambao unazungumzia kuhusu mtu katika nafsi ya tatu aliyepepea hewani kwa malengo ya kupata elimu, ubeti umetungwa kwa nafsi ya tatu katika umoja ili

kuwasilia maudhui ya mtunzi kupitia mtu mwingine. Mofu ‘a’ imetumika katika maneno kama vile “alipepea, alinepanepa,” kubainisha nafsi ya tatu umoja au kuonyesha msemaji.

Mfano mwingine:

**Dakika 15 za Uzalendo**

*Lakini kwa nini, waliweza fanya hivyo!*
*Walitoka ujijini? Hapana na wala sivyo*
*Je, walizuka majini? Hapana na sivyo!*
*Je, labda mbinguni? Hata sura zao hovyo!*
(Kezilahabi; *Kichomi* Uk. 51)

Katika ubeti huu, mtunzi amewasilisha dhamira na maudhui yake kupitia nafsi ya tatu katika wingi pale ambapo wanenaji wamerejelewa kwa mofu ‘wa’ katika maneno kama “walitoka, walizuka na waliweza” matumizi ya mofu “wa” katika maneno haya yanawasilisha nafsi ya warejelewa. Hii inaonyesha kuwa walikuwa watu zaidi ya mmoja kwa sababu ya matumizi ya mofu “wa”. Kwa jumla, mtafiti amegundua kuwa mtunzi wa mashairi tuliyoyachambua amezingatia usarufi au isimu katika kurejelea kipengele cha nafsi katika umoja na wingi kama ilivyo katika sarufi ya lugha.

## 3.4 Hitimisho

Katika sura hii mtafiti amebainisha vipengele vya kiisimu katika mashairi huru ya Kiswahili kutoka katika diwani teule za Kezilahabi. Aidha, kwa kubainisha vipengele hivi vya kiisimu, tuliweza kuonyesha jinsi vipengele vyenyewe vinatumika katika kuendeleza kazi ya mashairi huru ya Kiswahili. Vipengele vya kiisimu vilivyobainishwa ni: Aina za sentensi, uakifishaji na kipengele cha nafsi. Ni bayana kuwa kazi za mashairi huru na isimu vinategemeana, vinashabihiana na kuathiriana kwa kiwango kikubwa. Sura inayofuata itashughulikia umuhimu wa vipengele vya kiisimu katika kuendeleza kazi ya ushairi huru wa Kiswahili.

## SURA YA NNE

## UMUHIMU WA VIPENGELE VYA KIISIMU KATIKA KUENDELEZA KAZI YA MASHAIRI HURU

### 4.0 Utangulizi

Katika sura iliyotangulia, tulibainisha vipengele vya vya kiisimu na kuonyesha jinsi vilivyotumika katika mashairi huru ya Kezilahabi. Sura hii imeshughulikia umuhimu wa vipengele vya kiisimu katika kuendeleza kazi ya mashairi huru teule ya Kithaka wa Mberia na ya Kezilahabi. Vipengele ambavyo vimeshughulikiwa ni: Aina za sentensi, uakifishaji na kipengele cha nafsi. Katika kipengele cha aina ya sentensi, tumejikita kwenye aina tatu za sentensi ambazo ni: sentensi za mishata, sentensi ndefu na sentensi zenye mishororo isiyolingana katika ubeti.

Pia, utafiti umeshughulikia umuhimu wa kipengele cha uakifishaji kwa kuangalia viakifishi mbalimbali kama vile: alama za mtajo, kitone, koma, alama za nukuu, matumizi ya koloni, nusu koloni, matumizi ya herufi kubwa na vingine. Aidha, tumeangazia kipengele cha nafsi na kuonyesha umuhimu wa nafsi tatu za kisarufi tukihusisha nafsi hizo kwa kurejelea diwani teule. Nafsi zilizoangaziwa ni nafsi ya kwanza, nafsi ya pili na nafsi ya tatu.

Uchunguzi katika kuonyesha umuhimu wa vipengele vya kiisimu katika kuendeleza kazi ya mashairi huru ya Kiswahili umeongozwa na mhimili mmoja wa nadharia ya Fonolojia Mizani unaosema kuwa uhusiano wa ndani wa silabi huonyeshwa kwa kutumia mizani.

Aidha, Liberman na Prince (1977) walisistiza kauli hii kwa kuonyesha uhusiano wa ndani wa silabi mbalimbali zilizomo katika neno au kirai.

### 4.1 Umuhimu wa Aina za Sentensi katika Ushairi wa Kiswahili

Aina za sentensi zimeangaziwa kwa kueleza umuhimu wa sentensi za mishata, sentensi ndefu na sentensi zenye urefu usiolingana katika beti mbalimbali za mashairi kama ifuatavyo:

#### 4.1.1 Umuhimu wa Sentensi za Mishata katika Ushairi Huru

Katika diwani teule za Kithaka wa Mberia na za Kezilahabi, mistari mishata imetumika kimakusudi wala sio kiholela. Inapotumika katika shairi inaonyesha hali iliyo halisi ya mawasiliano japo kwa njia ya mkato na inayonata makini ya wasomaji. Watunzi hawa teule wameipanga kazi yao kwa jinsi ambayo inakuwa rahisi kwa hadhira katika kuufasiri ujumbe ambao wanakusudia kuwasilisha kwa hadhira yao.

Mfano wa kwanza:

**Shairi la 20**

*Katika mitaa walimoishi watu kwa amani*
*Jirani alisaka Jirani wa miaka na mikaka*
*Na kwa upanga kumkatakata bila huruma*
*Wanawake walivamiwa na watu waliowajua*
*Waliteswa kwa jinsi isiyoelezeka kwa lugha*
*(*Kithaka wa Mberia; *Doa* Uk. 80)

Mshairi anaangazia vita vilivyozuka baada ya uchaguzi na kufanya kutangazwa kwa ambaye alikuwa mshindi katika uchaguzi huo. Kuna baadhi ya watu ambao hawakuridhika na matokeo hayo na kwa hivyo, wakazua vita na ghasia zilizowatesa na kuwaua wengi.

Katika ubeti huu, mtunzi ametumia mistari mishata kwa mfano sentensi ya kwanza inakamilika katika sentensi ya pili, ameonyesha namna majirani waliokuwa wameishi kwa

amani kabla ya uchaguzi wa kiongozi waliyemchagua, mshairi ametumia mishata kuondoa uchovu wa kusoma kauli ndefu mfululizo kama ilivyo katika lugha ya nathari na kwa jinsi hiyo, ujumbe aliouanza katika sentensi ya kwanza unakamilika katika sentensi zinazofuata.

Mfano wa pili:

**Shairi la Ardhi yenye Siha na Uchangamfu wa Rutuba**

*Ardhi yenye siha na uchangamfu wa rutuba*
*Imelala usingizi katika kitanda cha maumbile*
*Tukinongenezana. 'Anga linaonea nchi'*
*Tambarare zenye uwezo wa kuhimili mamilioni*
*Zimeachiwa nguchiro, panya, mchwa na nyenze*
*Katika taifa linalotapatapa katika dimbwi la njaa*
*(*Kithaka wa Mberia; *Msimu wa Tisa* Uk. 3)

Mshairi anaangazia ardhi iliyo na rutuba ambayo ndiyo raslimali muhimu kwa binadamu lakini haitumiki vilivyo ili kupigana vita na janga la njaa katika nchi hiyo. Kwa mfano, wazo katika sentensi ya kwanza linakamilika katika sentensi ya pili na hata ya tatu. Mtunzi ametumia mishata katika ubeti huu ili kuleta maana anayaokusudia kuiwasilisha kwa hadhira ili kumfanya msomaji aendelee kuusoma ubeti mzima ndipo apate maana. Mishata imetumika kuwasilisha ujumbe katika akili ya mshairi badala ya kutumia lugha nathari.

Mfano mwingine:

**Shairi la Mawimbi ya Upweke**

*Jana*
*Alipopanda ulingo kwa uwezo wa ngazi ya ufisadi*
*Mshahara na marupurupu yalipokwea na kuelea angani*
*Alipoona sura yake ikipamba magazeti na viwambo*
*Manafiki walipompaka mafuta kwa mgongo wa chupa*
*Alipopata sagingi, dereva na mlinzi mwenye bastola*

*Aliposalimiana kwa mikono na wenye majina mateule*
*Alipokula Pamoja na vizito katika hoteli zenye mazulia*
*Akiwa juu, alipoangalia chini, hakuona aliokuwa nao*
*Aliona vidubwana vya kuhurumiwa na waliokamilika*
(Kithaka wa Mberia; *Mvumo wa Helikopta* Uk. 44)

Katika ubeti wa shairi hili, sentensi ya kwanza, ya pili, ya tatu, ya nne, ya tano, ya sita na ya saba ni mishata. Mtunzi amedokeza tu mistari hiyo kwa kuanza na kauli "alipo.". Sentensi ya kwanza haijakamilika kimaana hadi pale inapoambatanishwa na sentensi ya tisa amabayo ndiyo ya mwisho. Kwa mfano: "Alipopanda ulingo kwa uwezo wa ngazi ya ufisadi, Aliona vidubwana vya kuhurumiwa na waliokamilika".

Aidha, sentensi ya pili, ya tatu, ya nne, ya tano, ya sita, ya saba na hata ya nane ni mishata kwa kukosa kuleta maana ila tu zinapounganishwa na sentensi ya mwisho ndipo zinaleta maana kamilifu. Kwa mfano sentensi ya tatu: "alipoona sura yake ikipamba magazeti na vikwambo, aliona vidubwana vya kuhurumiwa na waliokamilika". Sentensi hizi za mishata zinaweza kuunganishwa na sentensi ya mwisho kwa kutumia viakifishi kama koma au kistari kifupi kama vipumuo ili kuleta maana ya kisarufi.

Mfano mwingine:

**Shairi la Nimechoka**

*Sauti ya baba inasema kwa msistizo*
*"Najua utafika wakati itakulazimu kudondoka,*
*Lakini endelea kushikilia hiyo waya*
*Kama unazo nguvu bado, na usikate tamaa,*
*Ila usitegemee kusifiwa au kusaidiwa;*
*Vichwa vyote hivi vilidondoka kutoka umbali huo,*
*Nawe kudondoka, utadondoka!"*
(Kezilahabi; *Kichomi* Uk. 35)

Katika ubeti huu, sentensi ya kwanza ni mshata kwa sababu imedokeza tu kauli kwa kuwa "sauti ya baba inasema kwa msisitizo." Sentensi hii haina maana hadi pale inapounganishwa na sentensi ya pili, ya tatu au hata kifungu kizima ndipo iweze kuleta maana inayokusudiwa na mtunzi. Maneno yaliyosemwa na baba yanapatikana kuanzia sentensi ya pili hadi ya mwisho na kwa hivyo sentensi hizi zinatusaidia kujua kauli zilizotolewa na baba baada ya kudokezwa katika sentensi ya kwanza.

Kwa kutumia mifano ya beti hizi nne za mashairi, sentensi za mishata zimetumiwa kimakusudi ili kuwasilisha ujumbe kwa kauli fupi zenye taharuki ya kutaka kujua yaliyofuata badala ya kutumia lugha ya kinathari ambayo ina maelezo mengi na marefu yenye uchovu kama zilivyo tanzu nyingine za kifasihi kama vile riwaya na tamthilia. Mishata inatumika katika kuwasilisha ujumbe kwenye akili ya mshairi badala ya kutumia lugha ya kawaida kama ilivyo katika tanzu zingine za fasihi.

### 4.1.2 Umuhimu wa Sentensi zenye Urefu Usiolingana katika Ushairi Huru

Kama tulivyosema awali, haya ni mashairi yenye sentensi au mishororo isiolingana katika ubeti yaani kila mshororo kwenye ubeti teule unatofautiana na mwingine kwa urefu kwa kuzingatia idadi ya silabi au mizani. Kwa mfano, kuna mistari mirefu na mifupi katika beti za shairi.

Katika mashairi huru ya Kiswahili, hakuna ulinganifu wa idadi ya mistari katika beti. Mashairi haya huwa hayazingatii ulinganifu na urari wa mizani. Hii ni sawa na kusema kuwa kila mshororo katika ubeti huwa na idadi yake ya silabi. Mchanganyiko wa sentensi ndefu na fupi zina umuhimu wa kipekee katika kuwasilisha ujumbe uliokusudiwa na mtunzi.

Katika beti za mashairi teule ya Kithaka wa Mberia, kuna matumizi mengi ya mishororo isiolingana yaani mchanganyiko wa sentensi ndefu na fupi katika ubeti mmoja wa shairi. Sentensi ndefu na fupi zinapotumika, mtunzi huwa na makusudi mahususi kwa kufanya hivyo kama ifuatavyo katika mifano ambayo imeshughulikiwa hapa chini.

Mfano wa kwanza:

**Shairi la Kifo cha Mende Wekundu**
*Na ujenge yako nyumba, jingi jasho likuoshe (silabi 16)*
*Ufyeke, upime na uweke nguzo (silabi 12)*
*Kisha paa uweke na ukandike (silabi 12)*
*Siku nyingi bila kuingiliwa na mgeni hutakaa (silabi 19)*
*(*Kezilahabi; *Karibu Ndani* Uk. 33)

Kupitia ubeti wa shairi hili, mtunzi ametumia sentensi zenye urefu usiotoshana kuzingatia idadi ya silabi kama ilivyobainishwa katika ubeti. Kwa mfano, mtunzi ametumia sentensi ya kwanza iliyo na silabi kumi na sita (16) ikilinganishwa na sentensi ya pili na tatu ambayo ni fupi kwa sababu amekusudia kuwasilisha hisia zenye uzito kwa mapana katika kuwasilisha maudhui ya kazi yake kuhusu ujenzi wa nyumba ya mrejewa, hii inaonyesha mtiririko wa mawazo katika fikra za mshairi na ana kusudia kuwasilisha ujumbe wake bila kujifunga kwenye matumizi ya sentensi za mkato.

Aidha, katika sentensi ya pili na ya tatu mshairi ametumia sentensi fupi fupi zenye silabi kumi na mbili (12). Amefanya hivyo ili kudokeza kauli inayofuata katika mstari unaofuata na vilevile, amefanya hivi ili kuorodhesha baadhi ya shughuli ambazo mnenewa anatarajiwa kuzifanya katika kuwaua mende wekundu.

Mfano mwingine:

***Shairi la 25:***

*Wanaofichwa nyumbani kwa jitihada thabiti (silabi 16)*

*Wazazi wakigugunwa na haya kuwazaa, (silabi 15)*

*Wamaozuiliwa kushikana mikono na mwangaza, (silabi 18)*

*Jamaa zao wakihofia macho ya ulimwengu, (silabi 17)*

*Hao si wachache wa kutoshea katika kiganja (silabi 17)*

*Ni idadi ya kujaza kumbi kadhaa hadi pomoni (silabi 18)*

*(*Kithaka wa Mberia*; Doa uk 101)*

Mtunzi wa shairi hili ametumia sentensi zenye urefu usiotoshana kwa kuzingatia utofauti katika idadi ya silabi katika kila mshororo kwa sababu hakutaka kujifunga kwenye sheria za utunzi. Kwa mfano: mtunzi ametumia sentensi fupi katika mshororo wa pili ambao una silabi kumi na tano (15), amefanya hivi kimakusudi ili kudokeza wazo ambalo linapatikana katika sentensi zinazofuata.

Hii inamsaidia msomaji wa kazi hii katika kutua na kumkumbusha kuwa kuna haja ya kuendelea kulisoma shairi au ubeti wote ndipo apate maana iliyokusudiwa. Sentensi au mstari wa tatu ni mrefu kuliko mistari mingine ambao una silabi kumi na nane (18), mshairi ametumia sentensi hii ndefu ili kuwasilisha hisia nzito kuhusu wale wahusika wanaozuiliwa kuungana mikono na wenzake kwa kuleta mwangaza ili wasitokee kujiunga na wenzao katika kupigania nchi yao.

Urefu tofauti wa sentensi katika ubeti wa shairi hili na pia katika mashairi yenye miundo ya sentensi kama hii unaweza kudumisha wizani katika shairi zima na kulifanya shairi liimbike ama likaririwe katika kuleta mdundo na mtiririko maalum katika mashairi. Katika kuchanganya mistari mirefu na mifupi husaidia kubadilisha kasi ya shairi na kujenga hisia mahususi katika hatua mbalimbali za kuwasilisha ujumbe (Arege, 2016).

Mfano mwingine:

***Shairi la mafahali wapigana***

*Mafahali wenye matumbo wanapigana, (silabi14)*
*Chini, chini, chini zaidi (silabi 9)*
*Mpaka vichwa vyao vinagusana, (silabi 11)*
*Alafu watazamaji wakondefu (silabi 12)*
*Wanaazna kupiga kelele. (silabi 10)*
*Haya! Haya! Machakulo haya! (silabi 10)*
*Polepole hawaoni kitu. (silabi 10)*
*Vumbi hewani, vumbi machoni (silabi 10)*
*Vumbi kuisha, mshindwa amekwisha kimbia. (silabi 15)*
*Mshindi juu ya kichuguu amekaa, (silabi 13)*
*Akionyesha kidole kimoja sasa (silabi 13)*
*Mchwa ndo askari (silabi 7)*
(Kezilahabi; *Kichomi* Uk. 5)

Katika ubeti wa shairi hili, mtunzi ametumia sentensi zenye urefu usiolingani kwa kuzingatia mizani katika kila mshororo. Kwa mfano, katika sentensi ya tisa inayosema "vumbi kuisha, mshindwa amekwisha kimbia" mshairi ametumia sentensi hii ndefu kwa kipumuo ili kuwasilisha maudhui ya kazi yake kuhusu mafahali wawili ambao wanapigana ambapo aliyeshindwa anakimbilia usalama wake. Katika kufanya hivi, mtunzi amejipa uhuru wa kujieleza kwa kina kusudi kazi yake ieleweka vyema na msomaji.

Aidha, mtunzi vilevile ametumia sentensi fupi zaidi katika ubeti huu kwa mfano, katika sentensi ya mwisho anaposema "mchwa ndio askari", sentensi hii ina silabi saba (7), mtunzi amekusudia kutamatisha ujumbe wake kuhusu ushindi wa aliyeshinda mapigano na sasa ameketi juu ya kichuguu akilindwa na mchwa kama askari. Mtunzi huyu amefanya

hivi kimakusudi ili kuwafanya wasomaji wa kazi hii wahisi uwepo wa maisha na jinsi yalivyo katika uhalisia wake.

Mfano mwingine:

**Shairi la Mkesha**

*Usiku wa manane bwana na bibi wanakumbatiana*
*Kujisahaulisha mateso na ahadi walizopewa.*
*Kwa muda mfupi waota ndoto,*
*Ndoto za ajabu na wastukastuka kwa hofu*
*Midomo yao ikiwa wazi, meno nje*
*Na nyuso zilizokunjamana. Lazima wakeshe.*
*Watoto wanacheka usingizini, na waandishi*
*Wayumbayumba, kalamu zao mikononi,*
*Macho mazito, na wanastukastuka*
*Kama mbwa vichaa wakali*
*Waliohisi kitu kitembeacho gizani.*
*(*E. Kezilahabi; *Karibu Ndani uk 4)*

Kezilahabi ametumia sentensi ndefu katika mstari wa pili ambayo ni ndefu sana ikilinganishwa na sentensi zingine, amefanya hivi kwa lengo la kuwasilisha ujumbe ambao umedokezwa na sentensi ya kwanza kuhusu bwana na bibi ambao sentensi ya pili inaeleza namna wapenzi hawa wanavyojisahaulisha na mateso na ahadi walizopewa. Matumizi ya sentensi hii ndefu inasaidia msomaji wa kazi hii kuelewa haraka ujumbe wa mshairi na kile alichoangazia kukiwasilisha kwa hadhira yake bila kutatizika.

Aidha, mtunzi ametumia sentensi fupi kwa mfano katika mstari wa kumi (10) ambao unasema “kama mbwa wenye vichaa wakali”, ametumia sentensi hii fupi katika kulinganisha namna waandishi walivyoyumbayumba kama mbwa wenye vichaa

huyumbayumba. Hii inasaidia kupunguza kasi ya usomaji wa kazi hii katika kuleta muwala na mshikamano.

Mfano mwingine:

**Shairi la Mwashi**

*Ulikuwa mwashi aliyekolea ujuzi: (silabi 15)*
*Kiswahili na usawa wa makabila (silabi 13)*
*Ulizifanya mawe adimu ya ujenzi (silabi 14)*
*Matamshi yaliyochujua kwa kichungi (15)*
*Na Maisha yaliyometameta maadili (silabi 15)*
*Yalikuwa saruji ya chapa ya kutajika (silabi 15)*
*Sasa tuna msingi imara wa taifa (silabi 14)*

*Mwalimu, kuwemo ndani ya udongo (silabi 12)*
*Hakutazuia kuinuka kutoka pumziko (silabi 17)*
*Na kupanda jukwaa la marmar na mvuli (silabi 16)*
*Kupokea hili koja la mawaridi adimu (silabi 16)*
*Kutoka kitalu cha maua moyoni mwangu (15)*
*(*Kithaka wa Mberia; *Msimu wa Tisa uk 40)*

Mawazo katika akili ya Kithaka wa Mberia yanadhibiti urefu wa sentensi zisizotoshana katika beti hizi mbili kwa mfano katika ubeti wa pili sentensi ya kwanza ina silabi kumi na mbili (12) ikilinganishwa na sentensi ya pili ambayo ina silabi kumi na saba ambazo ni nyingi.

Kwa jumla tumeona kwamba idadi ya silabi inatofautiana toka katika sentensi moja hadi nyingine. Hii inaashiria mtiririko wa mawazo katika akili ya mtunzi kwa hivyo ameweza kuwasilisha ujumbe kwa njia iliyo huru bila kujifunga kwenye kanuni za utunzi.

### 4.1.3 Umuhimu wa Matumizi ya Sentensi Ndefu katika Mashair Huru

Matumizi ya sentensi ndefu katika beti za shairi hutumika kwa kusudi la kuzitoa hisia zenye mawazo mapana na ili kumwezesha msomaji kuelewa kile mtunzi wa shairi husika anachokizungumzia kwa undani zaidi bila kutatizika.

Mfano wa kwanza:

**Shairi la Sombombi**

*Si mchache wa kusengenya, ni mwingi wa kuchongea na kukashifu*
*Kwa wivu, anabuni kuwapaka majirani na wenza chuoni*
*Machoni mwa watu, anajitia tabasamu, anavalia joho la ulimbwende*
*Kumbe ndani ya kinywa ana ulimi wenye panda kama wa mamba*
*Nyuma ya meno yanayoiga ya binadamu, kuna tezi za sumu ya swila*
*(*Kithaka wa Mberia; *Mvumo wa Helikopta* Uk. 43)

Mtunzi ametumia sentensi ndefu ndefu katika ubeti huu ili kuwasilisha ujumbe mzito na wenye mawazo mapana yanayohusu mrejelewa ambaye ana tabia za kusenganya wenzake lakini anapowakuta anajitia tabasamu la uongo. Kwa mfano: katika sentensi ya kwanza mtunzi ametumia sentensi ndefu kuelezea kuhusu mrejelewa ambaye ni mwingi wa kusengenya na kuchochea. Mshairi ametumia sentensi hizi ndefu kwa sababu amekusudia kuzitoa hisia zenye mawazo mapana kwa kuwezesha msomaji kuelewa kile anachozungumzia wazi bila kutatizika. Mashairi ya aina hii mara nyingi huwa ni ya toni ya huzuni na msiba.

Mfano mwingine:

**Shairi la 26**

*Husuni iliyokuwaje jamii bila tone la hatia*
*Kushuhudia kutiwa kufuli shule za wanao,*
*Uwi uliokuwaje dhidi ys wakazi wa msitu:*
*Afisa wa msitu na askari tawala wenye hamaki*
*Kushambulia nyumba za wenyewe kwa moto*

*Makazi yam situ yakawa sio mastakimu tena*
*Bali masazo yaliyotemwa na kinywa cha moto!*
*(*Kithaka wa Mberia; *Doa* Uk. 106)

Katika ubeti huu, sentensi ndefu zimetumika katika ubeti mzima haswa kupitia mstari wa kwanza na wa pili pale ambapo wazo linakamilikia, mtunzi anaposema "huzuni iliyokuwaje jamii bila tone, kushuhudia kutiwa kufuli shule za wanao" sentensi hii ndefu imetumika bila kikomo kwa vile mshairi alikusudia kuwasilisha fikra zake nzito kwa mapana kuhusu jinsi watu walioishi msituni kama makao wakati walivyoshambuliwa na askari tawala wenye hamaki kwa kuchoma nyumba zao kwa moto. Mtunzi alifanya hivyo kimakusudi ili kuwasilisha maudhui yake bila kujifunga kwenye sentensi za mkato.

Mfano mwingine:

**Shairi la Nimechoka**

*Wanadamu wameinama. Wanasali kwa haraka sasa.*
*Utafikiri wanahesabu mchanga utakaojaza kaburi langu.*
*Vichwa vyeupe vinacheka. Kingine kinasema tena:*
*"Mnaliona Hilo Joka!" vichwa vinacheka. Wanasali.*
*"Nyinyi nyote hamna akili! Mnaniudhi!*
*Hamwoni hali yangu!" Napiga kelele. Lakini vichwa*
*Havitishiki, na wanadamu hawatingishiki.*
(Kezilahabi*; Kichomi* Uk. 35)

Katika ubeti huu mtunzi ametumia sentensi ndefu ndefu katika ubeti mzima, kwa mfano sentensi ya kwanza inayosema "wanadamu wameinama. Wanasali kwa haraka sasa", mshairi ametumia ndefu kwa kipumuo ambacho ni kitone (.) ili amuwezeshe msomaji kutua kabla ya kuendelea kuisoma sentensi au kishazi kinachofuata katika sentensi hii ndefu.

Kezilahabi ametumia sentensi ndefu katika ubeti huu ili kutoa hisia nzito kwa utondoti kuhusu binadamu walioinama wakisali kwa kukejeliwa na sauti inayosema: “mnakiona hilo joka”. Hii inamwezesha msomaji kuelewa kwa urahisi kile mshairi anakusudia kuwasilisha.

### 4.2 Umuhimu wa Uakifishaji katika Mashairi ya Kiswahili

Wamitila (2008) anasema kwamba, uakifishaji huweza kutumika katika kuelekeza kwenye mantiki. Hii ina maana kuwa matumizi ya viakifishi mbalimbali katika utunzi wowote ule unatumika ili kuwaelekeza wasomaji wa kazi husika katika kuleta mantiki yaani wanafahamu maudhui na dhamira mbalimbali za watunzi.

Kwa hivyo, mashairi huru mara nyingi hutumia viakifishi mbalimbali kwa madhumni ya kusisitiza mambo fulani kimaudhui na katika kuunganisha fikra moja na nyingine ili kuwezesha kupatikana kwa muwala na mtiririko mzuri wa usomaji wa mashairi teule.

Katika sehemu hii, tumeangalia umuhimu wa viakifishi mbalimbali huku tukidondoa mifano mahususi ya mashairi kutoka katika diwani teule za Kezilahabi na Kithaka wa Mberia, katika kila diwani, tumechambua shairi mojamoja kama ifuatavyo:

#### 4.2.1 Uakifishaji kama Mbinu ya kujenga Uhuru katika Usarifu wa Lugha

Mfano wa kwanza:

**Shairi la Mwashi:**

*Leo labda, Uchumi wa ukanda*
*Ungelikuwa imara kama kigongo*
*Kama ndoto yako ya kuvuta pamoja*
*Haingeuliwa na wauaji wa Nairobi-*
*Ole wao wazungu weusi kama makaa*

*Na suti zao za milia na mikufu ya saa*
*Mazuu wakioachwa nyuma na malkia*
*Viumbe vya kuhurumiwa kwa huzuni.*
*Wagonjwa wenye virusi vya akili!*
*(*Kithaka wa Mberia; *Msimu wa Tisa uk 40)*

Kwa kuzingatia viakifishi vilivyotumika na mshairi mathalani: herufi kubwa, koma (,), kitone (.), kistari kifupi (-) na alama ya hisi (!). Kwa mfano, mshairi ametumia koma katika sentensi ya kwanza baada ya kusema "leo labda", ametumia kiakifishi hiki ili kumpa msomaji uwezo wa kutua ili aendelee kusoma sehemu nyingine ya sentensi kwa kuleta maana iliyokusudiwa.

Aidha, mtunzi ametumia kistari kifupi (-) mwishoni mwa sentensi ya nne katika kuwatambulisha wauaji wa Nairobi walioua uchumi wa ukanda ambao huenda leo hii ungefaidi wananchi. Kistari kifupi kimetumika kuonyesha kuwa sentensi hiyo ya nne haijamilika na kwamba itaendelezwa katika sentensi inayofuata.

Kithaka wa Mberia vilevile ametumia alama ya hisi (!) baada ya sentensi ya mwisho katika kukamilisha kifungu ili kuonyesha huzuni ya mhusika. Amefanya hivi kimakusudi ili kuvuta makini ya hadhira ili watambue jinsi waafrika walivyobadilisha hali zao za Maisha.

Kwa jumla tumebaini kuwa mshairi huyu ameweza kutumia hivi viakifishi ili kujipa uhuru wa kisarifu pamoja na kuweza kudhibiti miundo ya lugha kwa malengo ya kumtumikia msomaji wa kazi hii namna apendavyo katika uwasilishaji wake.

### 4.2.2 Uakifishaji kama Mbinu ya kuwasilisha Mawazo

Mfano mwingine:

**Shairi la Sisi kwa Sisi**
*Jangwani!*
*Katika mchanga, vumbi na joto kali tulisafiri*
*Tulisafiri mwendo wa kinyonga na kobe.*
*Hapakuwa na maji, hapakuwa na chakula*
*Wanyama hawakuwa, manyani ya Mbotela hayakuwa.*
*Nyuma yetu kuzima zetu nyayo ilinyesha*
*Mchanga na mguu, vumbi na macho. Kiwi!*
*Kama ngamia vipofu tulijikokota*
*Mizigo kichwani, mizigo mabegani.*
*Shingo ziliuma, midomo ikakauka. Kiu!*
*Miguu, mikono, nguvu ikawa haina. Mavune!*
*Lakini mbele tulikwenda, bila maji, bila chakula,*
*Tukihesabu vichwa vya Mfalme na Malkia.*
*Sisi kwa sisi tukilana, safari lazima iendelee.*
(Kezilahabi; *Karibu Ndani* Uk. 9)

Katika kuzingatia matumizi ya viakifishi vilivyotumiwa katika ubeti huu, mathalani: herufi kubwa, koma (,), kitone (.) na alama za hisi (!). Kwa mfano, mtunzi ametumia herufi kubwa mwanzoni mwa kila sentensi kupitia maneno kama vile; “Tulisafiri, Miguu, Lakini, Tukihesabu na Sisi”. Kwa kufanya hivi, mtunzi ameonyesha mtiririko wa mawazo katika akili ya yake na kuanzisha sentensi.

Aidha, mtunzi wa kazi hii ametumia koma (,) kimakusudi katika kifungu hiki kuashiria kipumuo kifupi baada ya kusoma sentensi ya pili na ya kumi na mbili (12), hii inambidi msomaji atue baada ya kufululiza mawazo yake marefu kisha aendelee na sentensi

zinazofuata.hii ni kusema kuwa koma imetumika kugawa mawazo katika sentensi. Kitone (.) kimetumika baada ya sentensi “Tukihesabu vichwa vya mfalme na malkia”, matumizi ya kiakifishi hiki ni kuonyesha mwisho wa wazo katika sentensi hiyo.

Ujumbe ambao umewasilishwa unakusudiwa kuwafikia wasomaji na huchukuliwa kuwa muhimu sana pale ambapo msomaji anasoma akizingatia viakifishi hivi. Mshairi ametumia viakifishi hivi katika ujenzi wa mawazo yake. Matumizi mwafaka ya viakifishi hivi humfaidi sana mtunzi wa kazi husika kwa vile ndiyo dira katika uwasilishaji wa mawazo. Aidha, matumizi ya alama za uakifishaji hizi zinasaidia msomaji na mtunzi kuingia katika kiini cha ujumbe wke kwa ndani bila kupoteza mada ya kazi yake.

### 4.2.3 Uakifishaji kama Chombo cha kuchochea Usaili wa Utafakari wa Ujumbe

Mfano mwingine:

**Shairi la 8**

*Baridi iliyoje katika mishipa ya damu*
*Ziwadiapo nyakati za Kwenda haja:*
*Nyayo za mfungwa zilizotamauka*
*Zinakanyaga kinamasi kwenye sakafu*
*Zikilakiwa na vijasumu vya aina nyingi?*
(Kithaka wa Mberia; *Doa* Uk. 38)

Mtunzi wa shairi hili ametumia viakifishi vifuatavyo kati ubeti wa shairi hili kama vile kitone (.), koloni (:) na kiulizi (?). Koloni (:) imetumika katika ubeti huu kuonyesha kile kinachofuata, hii ina maana kuwa koloni imetumika kuelezea sababu na kuonyesha matokeo ya sentensi tangulizi ambayo matokeo yake yanakamilika katika sentensi inayofuata. Katika ubeti huu, mshairi ametumia koloni baada ya sentensi “Ziwadiapo nyakati za Kwenda haja” katika kudokeza kuwa sentensi hii haijakamilika kimaana na kuna

haja ya kuendelea kusoma sentensi inayofuata ndipo upate maana iliyokusudiwa na mtunzi. Koloni ni muhimu sana kwa kuwa imetumika kudhibiti mahadhi ya usomaji na wizani katika ubeti wa shairi hii.

Aidha, mtunzi huyu ametumia alama ya kiulizi (?) ili kuonyesha swali la balagha katika sentensi. Kwa mfano: “zikilakiwa na vijasumu vya aina nyingi?”, kiakifishi hiki kimetumika kumfanya msomaji atafakari kuhusu ujumbe unaotolewa na mshairi. Katika kifungu hiki, mtunzi anaeleza kuhusu mateso ambayo mfungwa huyu anayapitia katika gereza na anatamatisha ubeti wenyewe kwa kauli ya huzuni ya hamaki kupitia kiakifishi hiki mwishoni mwa sentensi ya mwisho.

Viakifishi hivi katika mashairi huru ya Kiswahili hutumika kama chombo cha kujengea muktadha kufumbia mafumbo ambapo mtunzi anatumia katika kuwasilisha kazi yake. Viakifishi hivi ni vipengele vya kuleta uchochezi katika usaili na utafakari. Ujumbe unaowasilishwa aghalabu sio wa hoja moja kwa moja kwa msomaji isipokuwa pale inapokusudiwa na mshairi wa kazi husika.

### 4.2.4 Uakifishaji kama Njia ya Kuelekeza Toni katika Mashairi na Kudhibiti Mwendo wa Usomaji

*Mfano mwingine:*

**Shairi la Kilabuni**

*Tulipokutana kilabuni mara ya mwisho*
*Nilipotoa kauli ya kirafiki, “pewa kinywaji!”*
*Alipofunua kinywa, alitangaza, “chivas!”*
*Akapata agizo, akashukuru kwa tabasamu*
*Bili ilipokuja, bila huruma, ikanichoma-*

*Bei haikuwa bei, ilikuwa mkuki kifuani!*
(Kithaka wa Mberia; *Mvumo wa Helikopta* Uk. 58)

Toni na hali vinategemea matukio katika uwasilishaji wa mashairi huru, toni ni mapigo ya yanayosaidia kuainisha ukasi wa shairi. Viakifishi vinaweza kutumika katika matukio ya furaha, starehe na mapenzi ama ya huzuni na machozi. Kwa mfano, katika ubeti wa shairi hili, mshairi ametummia viakifishi vifuatavyo kudhihirisha toni za huzuni na starehe katika miktadha waliyokuwemo wahusika. Kwa mfano, kiakifishi (!) katika sentensi "pewa kinywaji" kimetumika kuonyesha toni ya furaha na starehe ya hawa wahusika wakiwa katika burudani za unywaji kwenye kilabu, nacho kiakifishi kistari kifupi na koma (, na -) vimetumika pamoja na mshairi kuonyesha toni ya huzuni na majuto haswa baada ya maneno "bila huruma ikanichoma!" na "…ilikuwa mkuki kifuani!", maneno haya yanaonyesha toni ya huzuni haswa baada ya msimulizi kugundua kuwa alifaa kulipi vinywaji hivyo apende asipende.

Viakifishi hivi vimetumika kuonyesha hali ya toni mbalimbali. Vinamsaidia msomaji kujitia katika toni inayowakilishwa wakati anaposoma ubeti huu. Aidha, mshairi ametumia viakifishi hivi hasa baada ya maneno haya: "Nilipotoa kauli ya kirafiki," na "bili ilipokuja," kuashiria kupunguza kwa kasi ya usomaji wa shairi hilo, yaani kumwezesha msomaji wa kazi hii kutua kidogo kabla ya kuendelea na usomaji.

### 4.2.5 Viakifishi katika Kusaidia Kuifanya Matini Kueleweka Kisarufi

Watunzi hawa Kithaka na Kezilahabi wa mashairi huru ya Kiswahili wametumia viakifishi mbalimbali ili kushirikisha katika kubainisha ujumbe kwa malengo ya kuwasiliana na hadhira au wasomaji wa kazi yao kama ifuatavyo katika ubeti wa shairi lifuatalo:

Mfano wa shairi:

***Shairi la Nimechoka***

*Mikono inaniuma, na waya imekwishanikata vidole.*
*Damu imetiririka hadi kwapani; kujipangusa siwezi.*
*Nimechoka. Kadri niendeleavyo kuning'inia, ndivyo*
*Sura yangu ionyeshavyo vizuri alama za uchovu.*
*Ninatazama huku na huko kuwatafuta wenye huruma,*
*Lakini wanadamu wote wazima wanainamisha vichwa*
*Chini kana kwamba hawanijui; hata jamaa zangu!*
(Kezilahabi; *Kichomi* Uk. 34)

Katika ubeti wa shairi hili, mtunzi ametumia viakifishi mbalimbali kama vile: kitone (.), koma (,), nusu koloni (;), herufi kubwa na alama ya hisi (!). Ametumia viakifishi hivi kimakusudi kwa sababu analenga kuwasilisha maudhui ya kazi yake kikamilifu. Matumizi ya viakifishi hivi yamebainishwa kama ifuatavyo:

1. Herufi kubwa zimetumika katika kila mwanzo wa sentensi kuonyesha mianzo ya sentensi au mishororo kama ilivyo katika sarufi ya lugha kwa mfano katika maneno kama vile "Mikono, Damu, Nimechoka na Nitazama".
2. Koma zimetumika kuonyesha kutua au kutenganisha mfululizo wa matukio katika usomaji. Kwa mfano, katika sentensi ya kwanza kuna koma baada ya sentensi "mikono inauma". Imetumika kuwezesha msomaji kutua kidogo ndipo aendelee kusoma sentensi inayofuata. Aidha, koma imetumika katika sentensi hii ya kwanza ili kugawanya mawazo na kutoa maelezo zaidi katika sentensi.
3. Nusu koloni imetumika katika sentensi ya pili na ya mwisho katika kuunganisha vishazi huru viwili au kuonyesha mawazo mawili katika sentensi. Kwa mfano, kishazi cha kwanza katika sentensi ya pili "damu inatiririka hadi kwapani", imeweza

kuunganishwa na kishazi cha pili katika sentensi hiyo ambacho ni: “kujipangusa siwezi” kwa kutumia nusu koloni. kuonyesha hoja nzito au kuu inahusiana na ile iliyotangulia.

4. Alama za hisi zimetumika kuashiria kauli au toni ya huzuni na masikitiko ya msemaji hasa baada ya kukosa msaada kutoka kwa wale alidhani wangemuhurumia kupitia kauli zake “Chini kana kwamba hawanijui; hata jamaa zangu!”
5. Kitone kimetumiwa na mshairi katika ubeti huu mwishoni mwa sentensi ya pili na ya nne, kwa mfano: “sura yangu ionyeshayo vizuri alama za uchovu.”, imetumika kuashiria mwisho wa wazo hasa baada ya sentensi zilizokamilika kisarufi na kimantiki.

### 4.3 Umuhimu wa Kipengele cha Nafsi katika Kuendeleza Ushairi Huru

Katika sehemu hii, tumegawa data katika nafsi tatu zilizo katika Kiswahili sanifu ambazo ni nafsi ya kwanza, nafsi ya pili na nafsi ya tatu. Kipengele cha nafsi huchunguza majukumu ya wahusika katika matukio ya mawasiliano (Marmaridour, 2000). Majukumu haya kwa kawaida huwa ni ya mnenaji na anayerejelewa katika kazi husika hasa nafsineni katika ushairi.

#### 4.3.1 Umuhimu wa Nafsi ya Kwanza katika Ushairi Huru

Nafsi ya kwanza katika ushairi huru wa Kiswahili husheheni masuala wanayofanya wahusika na visa vyenyewe. Tumeangazia umuhimu wa nafsi ya kwanza katika umoja na wingi. Nafsi ya kwanza katika umoja huwa inaasharia mnenaji wa tamko kama inavyojitokeza katika ubeti ufuatao wa shari hili:

**Shairi la Mkimbizi**

*Nilikuwa na bahati kama mtende*
*Mbio za usiku wa kelele gizani*
*Zilinitema kutoka kinywa cha mauti*

*Kama mbarika kutoka ganda la mboni*
*Sas, katika mandhari, mikono mitupu*
*Jina langu limefunikwa kwa ukungu*
*Nimebakia an bandiko: mkimbizi*
(Kithaka wa Mberia; *Msimu wa Tisa* Uk. 57)

Katika ubei huu, kiambishi 'ni' cha nafsi ya kwanza katika umoja kimetumiwa na mtunzi kumrejelea msemaji kuptia maneno haya: "Nilikuwa, nimebakia". Kwa hivyo akilini mwa msomaji ufasiri wa 'ni' unawakilisha msemaji mmoja katika nafsi ya kwanza umoja. Kwa hivyo, umuhimu wa matumizi ya nafsi ya kwanza umoja unatumika kuonyesha ushahidi wa matukio yanayosimuliwa na mshairi kwa wasomaji wake kwa ukina. Hii ndiyo inayoitwa mbinu ya uchopekeji ambayo mtunzi anajinasibisha na wahusika wengine katika kazi teule. Aidha, nafsi ya kwanza katika wingi inajitokeza kupitia ubeti wa shairi lifuatao:

Mfano wa kwanza:

**Shairi la Sisi kwa Sisi**

*Nyikani!*
*Wakati huo umepita, safari inaendelea.*
*Tumepumzika chini ya mti mkavu. Inanyesha.*
*Hatutasimama hapa kusubiri tone la mwisho!*
*Mti huu wenye jani moja lipepealo*
*Hauwezi kutukinga sote. Jani linavuja,*
*Na mvua inazidi kunyesha. Nasi tumesimama*
*Tukihesa bu watawala wa Maisha barani*
(Kezilahabi; *Karibu Ndani* Uk. 9)

Utaratibu wa kusimba viambishi vya viwakilishi "sisi na tu" ni kutambua kile kinarejelewa kwa kumtambua msemaji. Kwa hivyo, matumizi ya nafsi ya kwanza katika wingi yanatumika kuonyesha uhusika wa nafsi ya kwanza wingi. Umihimu wa nafsi ya kwanza

katika wingi imetumika katika ubeti wa shairi hili ili kuonyesha ushahidi wa matukio yanayosimuliwa na mtunzi kwa hadhira yake kwa ukina.

### 4.3.2 Umuhimu wa Nafsi ya Pili katika Ushairi Huru

Nafsi ya pili katika mashairi huru hutambuliwa kupitia viambishi vya viwakilishi "nyinyi na m" katika wingi na "wewe na u" katika umoja. Tazama mfano ufuatao:

**Shairi la Hadithi ya Kitoto**

*Kainama mwana Wesema*
*Ulisifika tangu kale*
*Lakini sasa tazama*
*Mke duni umekuwa*
*Kanana mwana Wesema*
*(*E. Kezilahabi; *Kichomi uk 45)*

Kwa kurejelea ubeti huu, mshairi ametumia mofu 'u' katika maneno: "ulisifika…na umesema" kurejea nafsi ya pili ya mrejelewa ambaye ni mwanamke aliyekuwa mwema mwenye sifa nzuri lakini baadaye akaja kuwa mke duni.

Mfano mwingine:

**Shairi la Firimbi**

*Kwa ujasiri kama tumba la jua*
*Mlipanda kilimani mkapiga mbiu*
*Kwa maneno wazi kama firimbi*
*Mkaarifu umma kwa angani*
*Kunapepea bendera nyekundu*
*Kitambaa chenye nembo ya fuvu*
*Ishara ya mamlaka ya virusi sugu*
(Kithaka wa Mberia; *msimu wa Tisa* Uk. 83)

Mtunzi wa kazi hii ametumia mofu 'm' kwenye maneno kama "mlipanda, mkaarifu" ili kurejelewa wanenaji au wanenewa kama watu walio katika nafsi ya pili wingi. Umuhimu

wa matumizi ya nafsi ya pili kwa jumla hutumika kumfanya msomaji au wasomaji wa kazi husika wajione kuwa wao ndio walengwa wakuu wa kazi husika na kuonyesha matamko yenye maagizo pale mrejelewa hubainika wazi.

### 4.3.4 Umuhimu wa Matumizi ya Nafsi ya Tatu katika Ushairi Huru

Nafsi ya tatu hutumika kuwarejelea watu ambao sio wanenaji ama wanenewa katika matukio ya mawasiliano. Wanaweza kuwa warejelewa au hadhira isiyokuwa wasemewa (Levison, 1983). Nafsi hii huonyeshwa kwa kutumi mofu ‘a’ na ‘wa’ katika umoja na wingi mtawalia ama kupitia viwakilishi “yeye na wao” kwenye umoja na wingi mtawalia. Nafsi ya tatu katika umoja imedhihishwa kupitia ubeti ufuatao:

**Shairi la Kimbuga cha Misiba**
*Kijana aliyepigana mieleka na vitabu akafaulu*
*Hatimaye akachuna shahada na kuitia mfukoni*
*Jicho la Benki ya Taifa lilimwona anapendeza*
*Akapata kivuli cha kumstiri joto la jua la uhitaji*
*Maisha yakatulia katika pepezi za kujikidhia*
(Kithaka wa Mberia; *Mvumo wa Helikopta* Uk. 38)

Kwa kurejelea ubeti wa shairi hili, mtunzi ametumia nafsi ya tatu umoja kumrejelea mrejelewa ambaye ni kijana aliyepata mafanikio mema baada ya kuhitimu na kupata shahada kisha baadaye akajinyakulia kazi nzuri kwenye benki ya taifa. Nafsi ya tatu imedhihirika kupitia kiambishi cha kiwakilishi ‘a’ katika maneno: “aliyepigana…akapata”. Kwa ufupi tuseme kuwa nafsi ya tatu katika umoja huonyesha mtu ambaye ndiye mrejelewa katika shairi. Halikadhalika nafsi ya tatu katika wingi pia inadhihirika kupitia mfano ufuatao:

**Shairi la Kifo cha Mende Wekundu**

*Wataanza kutalii mipaka mende usiku,*
*Nje na ndani ya nyumba watazunguka*
*Bila woga, bila ruhusa ulichonacho watakula,*
*Masalio yatakuwa yako, ijara ya kaziyo.*
(Kezilahabi; *Karibu Ndani* Uk. 33)

Nafsi ya warejelewa inabainika kupia mofu ‘wa’ katika maneno haya: “wataanza…watakula”. Kama tulivyotanguliza nafsi ya tatu katika wingi inatumika kuonyesha warejelewa katika kifungu cha shairi kwa mfano katika ubeti huu warejelewa ni mende ambao wanasemekana kula vyakula vya binadamu bila woga.

Umuhimu wa nafsi ya tatu katika mashairi huru ya Kiswahili kwa jumla hutumika kuwaweka karibu wasomaji wa kazi husika wa mashairi huru husika.

**Tanbihi:** tumegundua kwamba matumizi ya nafsi katika ushairi huru ni mtindo ambao hutumika kwa malengo ya kuifanya kazi ya ushairi kuwa hai na kuwachora wahusika wake na kuonyesha upekee wa kazi ya mtunzi ili kufikisha ujumbe kwa hadhira yake.

### 4.4 Hitimisho

Katika sura hii, tumeelezea umuhimu wa kila kipengele cha isimu katika kuendeleza kazi ya ushairi huru wa Kiswahili kwa kudondoa mifano mahususi kutoka katika diwani teule za Kezilahabi na Kithaka wa Mberia. Kwa kufanya hivyo, tumebaini kuwa isimu inachangia pakubwa sana na ina mchango mkubwa katika kuendeleza utunzi wa mashairi huru ili kuimarisha usomaji wa mashairi huru ya Kiswahili kwa sababu hakuna kazi yoyote ile ya kifasihi inayoweza kuendelezwa bila kuzingatia isimu au usanifu wa sarufi ya lugha. Sura inayofuata imeshughulikia, muhtasari wa utafiti, matokeo ya utafiti, na mapendekezo kwa tafiti zaidi za b

# SURA YA TANO

# MUHUTASARI, MATOKEO NA MAPENDEKEZO YA UTAFITI

## 5.0 Utangulizi

Sura hii imeshughulikia muhtasari wa utafiti na matokeo ya utafiti kwa kuongozwa na malengo ya utafiti pamoja na nadharia ya Fonolojia Mizani. Aidha, matatizo ya utafiti yameelezwa. Isitoshe, sura hii imetoa mapendekezo ya utafiti wa baadaye katika kazi zinazohusiana na isimu na tanzu nyingine.

## 5.1 Muhtasari wa Utafiti

Utafiti huu ulilenga kuchanganua ushairi huru wa Kiswahili kwa kuzingatia mbinu za kiisimu katika dwani teule za Kithaka wa Mberia na za Kezilahabi ambazo ni *Doa*, *Msimu wa Tisa, Mvumo wa Helikopta, Kichomi* na *Karibu Ndani*. Malengo makuu ya utafiti huu yalikuwa ni: Kubainisha vipengele vya kiisimu katika mshairi huru na kuonyesha namna vipengele vya kiisimu vinavyotumika katika kuendeleza kazi ya mashairi huru ya Kiswahili ya Kithaka wa Mberia na ya Kezilahabi na mwisho kuonyesha umuhimu wa vipengele vya kiisimu katika kuendeleza kazi ya mashairi huru ya Kiswahili.

Aidha, vipengele vya kiisimu vilivyobainishwa ni: kwanza, aina za sentensi, pili, uakifishaji na tatu ni kipengele cha nafsi. Katika kuangalia aina za sentensi, aina tatu za sentensi zifuatazo zilishughulikiwa: sentensi za mishata, sentensi ndefu na sentensi zenye urefu usiolingana. Viakifishi mbalimbali kama vile; matumizi ya herufi kubwa, koma, kitone, alama za hisi, matumizi ya koloni na nusu koloni viliweza kubainishwa na kuonyesha jinsi vinavyotumika na umuhimu wake katika kuendeleza kazi ya mashairi huru ya Kiswahili.

Mwisho, utafiti uliweza kuangalia kipengele cha nafsi katika utatu yaani nafsi ya kwanza, nafsi ya pili na nafsi ya tatu katika umoja na wingi. Baada ya kufanya hivi tuliweza kuonyesha jinsi nafsi zinavyotumika katika mashairi teule katika kuendeleza kazi ya mashairi huru ya Kiswahili kwa kurejelea diwani teule za Kithaka wa Mberia na za Kezilahabi.

Utafiti huu uliongozwa na nadharia ya Fonolojia Mizani (FM) iliyoasiwa na Liberman (1975) kisha ikaendelezwa na Liberman na Prince (1977). Nadharia ya Fonolojia Mizani imetumika katika ushairi huu kwa sababu ilifaa sana kwa kuwezesha kuchanganua mashairi huru teule kwa kutumia mbinu za kiisimu.

Fonolojia Mizani ni nadharia ya mtazamo wa uchanganuzi wa mfumo wa sauti za lugha ambao umejikita katika mfumo sauti kama kitu ambacho kimejengeka kimsonge kwa kufuata misingi ya silabi, maneno, virai na sentensi. Hivyo basi, nadharia hii imetumika kuibua na kubainisha vipengele mbalimbali vya kiisimu katika ushairi huru wa Kiswahili.

Katika sura ya kwanza tumeshughukia vipengele vifuatavyo: Usuli wa mada, suala la utafiti, maswala ya utafiti, malengo ya utafiti, umuhimu wa utafiti, sababu za kuchagua mada, upeo na mipaka ya utafiti, yaliyoandikwa kuhusu mada, misingi na mihimili ya kinadharia na mbinu za utafiti.

Sura ya pili imeweza kubainisha vipengele vya kiisimu ambavyo ni aina za sentensi, uakifishaji na kipengele cha nafsi. Aidha, sura hii imeonyesha jinsi vipengele vya kiisimu vilivyotajwa vinatumika katika kuendeleza kazi ya mashairi huru teule kwa kurejelea diwani teule za Kithaka wa Mberia.

Sura ya tatu imeweza kubainisha vipengele vya kiisimu katika mashairi huru ya Kiswahili na kuonyesha jinsi yanavyotumika katika kuendeleza kazi ya mashairi huru katika diwani teule za Kezilahabi.

Sura ya nne imeshughulikia umuhimu wa vipengele vya kiisimu katika kuendeleza kazi ya mashairi huru teule ya Kiswahili. Utafiti uliweza kuangalia umuhimu wa kila kipengele cha isimu katika mashairi mbalimbali kutoka katika diwani teule. Kwa mfano, imebainika kuwa matumizi ya sentensi za mishata inasaidia mtunzi wa kazi husika kuwasilisha kazi yake kwa njia iliyo huru na huondoa uchovu wa kusoma kazi zilizoandikwa katika lugha ya kinathari ambazo aghalabu huwa ndefu. Pili, sentensi zenye urefu usiolingama katika ubeti husaidia kubadilisha kasi ya shairi na kujenga hisia muhimu katika hatua mbalimbali. Aidha, sentensi ndefu zimetumika ili kumpa mtunzi wa kazi husika kutoa hisia nzito zenye mawazo mapana ili kuwezesha msomaji kuelewa malengo ya mshairi wa kazi husika kwa undani bila kutatizika. Vilevile katika sura ya nne tuliangazia umuhimu wa viakifishi mbalimbali vya lugha na tukagundua kuwa viakifishi vinatumika ili kudhibiti mwendo wa usomaji, kudokeza kauli mbalimbali na vingine vimetumika kama mbinu za kuwasilisha ujumbe.

Mwisho, sura hii pia imeangazia umuhimu wa nafsi mbalimbali kama vile nafsi ya kwanza, ya pili na ya tatu na kubaini kuwa matumizi ya nafsi mbalimbali katika ushairi huru husaidia msomaji wa kazi husika kufahamu sauti ya mnenaji au mrejelewa katika shairi. Nayo sura ya tano tumeshughulikia; muhtasari wa utafiti, matatizo ya utafiti, matokeo na mapendekezo ya utafiti za baadaye.

## 5.2 Matokeo ya Utafiti

Utafiti huu ulilenga kutimiza malengo matatu: La kwanza ni kubainisha vipengele vya kiisimu katika mashairi huru teule ya Kithaka wa Mberia na kuonyesha jinsi vinavyotumika katika kuendeleza kazi ya mashairi huru ya Kiswahili, pili ni kubainisha vipengele vya kiisimu katika mashairi huru na kuonyesha jinsi yanavyotumika katika kuendeleza kazi ya mashairi huru ya Kiswahili katika diwani za Kezilahabi na tatu ni kuonyesha, umuhimu wa vipengele vya kiisimu katika kuendeleza kazi ya mashairi huru teule.

Malengo ya kwanza na ya pili yameafikiwa kutokana na kubainisha vipengele vya kiisimu na kueleza kwa kina jinsi vipengele hivyo vinavyotumika katika kuendeleza kazi ya mashairi huru teule. Mihimili ya nadharia ya Fonolojia Mizani ilifaa kwa kuwa ilisaidia kubainisha vipengele vya kiisimu na kuonyesha jinsi vipengele hivyo vinatumika katika kuendeleza kazi ya mashairi huru teule hasa kupitia mhimili wa kwanza wa nadharia hii unaosema kuwa, mpangilio msonge ambapo vipengele vya kiisimu vya kifonolojia huakilishwa katika ruzu zilizo katika uhusika wa kimsonge yaani kuanzia vipengele vikubwa zaidi hadi vidogo zaidi (Massamba, 2009). Kwa kuzingatia mhimili huu tuliweza kubainisha usarufi katika kazi ya ushairi huru mathalani kipengele cha aina za sentensi, tuliweza kutofautisha aina za sentensi kama vile sentensi za mishata, sentensi ndefu na sentensi zenye urefu usiolingana katika beti kwa kutumia mhimili huu na kuangalia jinsi zilivyotumika katika kuendeleza kazi ya mashairi huru teule.

Mhimili wa pili wa nadharia hii unaosema kuwa, kubainisha uwakilishi mkazo katika lugha kwenye viwango vya neno na katika viwango vya tungo ambapo uchanganuzi wa sauti

umejikita katika kigezo cha nguvu msikiko kinachoweza kutofautisha silabi zenye mkazo dhidi ya silabi zisizo na mkazo kwa mawimbi ya sauti wakati wa utamkaji. Hii husaidia kujua pale ambapo silabi huanzia na pale zinapokamilikia katika kiwango cha neno na kirai.

Kwa kuzingatia mhimili huu wa pili, utafiti uliweza kubainisha umuhimu wa viakifishi mbalimbali viliyotumika katika mashairi teule yaliyochunguzwa. Kwa mfano, tuliweza kujua kuwa mshairi anakusudia kutumia viakifishi mbalimbali kwa sababu zifuatazo: kwanza, matumizi ya viakifishi katika kujenga uhuru wa usarifu wa lugha, pili, matumizi ya viakifishi kama mbinu ya kuwasilisha mawazo, tatu, viakifishi kama chombo cha kuchochea usaili wa utafakari wa ujumbe na mwisho, matumizi ya viakifishi katika kuifanya matini kueleweka.

Aidha, mhimili huu wa pili ulituwezesha kutambua nafsi mbalimbali za Kiswahili sanifu zilizotumika katika mashairi yaliyochanganuliwa kwa kuonyesha mofu inayofaa kutiwa mkazo katika kuonyesha nafsi ya msemaji kama vile nafsi ya kwanza inabainishwa kwa kutumia mofu ‘ni’ na ‘tu’ nayo ya pili inabainishwa kwa kutumia mofu ‘u’ na ‘m’ kuashiria mrejelewa kisha katika nafsi ya tatu inawasilishwa kwa mofu ‘a’ na ‘wa’. Kwa kufanya hivi, utafiti ulisaidia kugundua kuwa matumizi ya nafsi mbalimbali katika mashairi huru ya Kiswahili yana umuhimu kama vile: kutumika kuwaweka karibu wasomaji wa kazi husika, pili, hutumika kumfanya msomaji wa kazi husika ajione kuwa ndiye mlengwa mkuu wa kazi husika na vilevile nafsi inatumika kuonyesha ushahidi wa matukio yanayosimuliwa na mtunzi kwa hadhira kwa undani zaidi. Kwa kuzingatia haya, msomaji wa kazi husika anatambua sauti ya nafsi haraka. Mhimili wa tatu uliwezesha utafiti kuafiki

malengo ya tatu ya utafiti huu kwa kutathmini umuhimu wa vipengele vya kisimu katika kuendeleza kazi ya mashairi huru teule. Utafiti huu umebaini kuwa katika mashairi huru ya Kithaka wa Mberia na Kezilahabi, kuna uhusiano mkubwa sana wa matumizi ya vipengele vya isimu katika kuendeleza kazi ya mashairi huru ya Kiswahili.

Lengo la kuchunguza vipengele vya kiisimu katika mashairi huru ya Kiswahili limetimizwa kwa kuwa utafiti huu umebainisha kuwa isimu na fasihi vinahusiana na kutegemeana kwa kiwango kikubwa na haviwezi kutenganishwa na kuwa vipengele vya kiisimu vina umuhimu mkubwa katika kuendeleza kazi ya mashairi huru ya Kiswahili.

### 5.3 Changamoto za Utafiti

Utafiti huu umekumbwa na changamoto kadha wa kadha. Kwanza, ukosefu wa fedha za kutosha ili kushughulikia baadhi ya mahitaji ya utafiti huu. Pili, utafiti huu ulikumbwa na janga la korona (covid 19) ambalo lilichukua kipindi kirefu cha watahiniwa kukaa nyumbani bila kusoma wala kukutana na msimamizi ili kushughulikia kazi hii. Pia, mtafiti alikumbwa na changamoto za kusafiri hapa na pale hasa chuoni kumtafuta msimamizi lakini yote tisa kumi utafiti ulikamilika kama ilivyotarajiwa.

### 5.4 Hitimisho

licha ya changamoto zilizoathiri utafiti huu, utafiti ulibainisha ya kwamba mbinu za kiisimu zinaweza kutumika kkatika uhakiki wa ushairi huru. Kimsingi, huwezi kutenganisha kazi za kiisimu na kifasihi kwa vile zinategemeana katika kuwasilisha ujumbe unaokusudiwa. Na hivyo maswali ya utafiti yalijibiwa na malengo yametimizwa.

## 5.5Mapendekezo

Utafiti huu umechunguza namna mashairi huru ya Kiswahili yanavyoweza kuchanganuliwa kiisimu katika diwani teule za Kithaka wa Mberia na Kezilahabi ambazo ni: *Msimu wa Tisa, Mvumo wa Helikopta, Doa, Kichomi* na *Karibu Ndani*. Uchanganuzi huu umeshughulikia vipengele vitatu vya kiisimu ambavyo ni: Aina za sentensi, uakifishaji na kipengele cha nafsi. Utafiti umeongozwa na nadharia ya Fonolojia Mizani iliyoasisiwa na Liberman (1975) na kuendelezwa na Liberman na Prince (1977).

Hivyo basi, tunapendekeza tafiti za baadaye zifanywe kuhusu; uhakiki wa kiisimu katika ushairi wa kiarudhi au kimapokeo kwa kuzingatia vipengele vingine vya kiisimu kama vile mpangilio wa maneno katika sentensi au hata kuboronga sarufi. Aidha, tunapendekeza watafiti wa baadaye watafiti kuhusu uchanganuzi wa kiisimu lakini ujikite katika tanzu nyingine za fasihi kama vile; riwaya na hadithi fupi kwa kuzingatia mtazamo wa nadharia nyingine za isimu.

## MAREJELEO


Arege, T. (2016). *Fani Katika Ushairi*. Nairobi: Oxford University Press.

Chacha, N. C. (1980). *Ushairi wa* Abdilatif: *utenzi wa Maisha ya Adamu na Hawa*. Tasnifu ya M.A, Nairobi: Nairobi University Press.

Crystal, D. and Davy, D. (1969). *Investigating English style.* London and New York, NY: Roatlegde.

Halle, M. and Vergnaud, J. R. (1987*). Linquitic Inquiry*. Cambridge: The MIT Press Publication.

Hayes, B. (1980). *Ametrical Theory of Stress Rules*. Doctoral Dissertation, MIT, Cambridge, Massachusetts. Indiana University.

Kahigi, K. K. (1975). Ushair*i:* Mtazamo wa Kisayansi. *Poetry: A Scientific Perspective, Kiswahili*, 45(1), 35-50.

Kezilahabi, E. (1974). *Kichomi.* Nairobi: Heinmann Educational Books Ltd.

Kezilahabi, E. (1988). *Karibu Ndani*: Dar es Salaam:  DUP.

Kitsao, J. (1975). *A Stylistic Approach Adopted ForThe Study of Swahili Prose Texts*.' Tasnifu ya uzamili. Nairobi: University of Nairobi.

Kombo, K. D. and Tromp, L. A. D. (2006). *Proposal and Thesis Writing: An Introduction. Paulines Publishers*, Nairobi, Kenya.

Kothari, C. R. (2008). *Research Methodology, methods and Techniques.* New Delhi: New Age International Ltd.

Leech, G. (2008). *Language in Literature:  Styles and foregrounding*. Harlow: Pearson Longman.

Leech, G. na Short, M. (1998). *Style in Fiction: A Linguistic Inroduction to English Fictional Prose*. London: Longhorn.

Levison, S. C. (1983*). Pragmatics*. Cambridge:  Cambridge University Press.

Liberman, M. (1975). *The Intonation System of English. PHD dissertation MIT.* Bloomington: Indiana University Linguistic Club.

Liberman, M. na Prince, A. (1977). '*On the Stress and Linguistic Rhythm'* Katika Linguistics Inquiry 8: 249-336.

Maitaria, J. N. (2012). Uandishi wa Ushairi wa Kiswahili: Dhima ya Methali. Tasnifu ya Uzamili: Chuo kikuu cha Kenyatta, Nairobi. (Haijachapishwa).

Makanga, A. M. (2008). *Uchanganuzi wa Kiisimu katika Matini ya Fasihi*. Nairobi: University of Nairobi

Massamba, D. P. (2004*). Kamusi ya Isimu na Falsafa ya Lugha.* Taasisi ya uchunguzi wa Kiswahili, Chuo Kikuu cha Dar'es Salaam Publisher.

Mberia, K. (2000). *Msimu wa Tisa.* Nairobi: Marimba publishers.

Mberia, K. (2018). *Mvumo wa Helikopta:* Marimba Publications.

Mberia, K. (2019). *Doa.:* Marimba Publications.

Milroy, L. (1987). *Observing and Analyising natural Language*. Oxford: Blackwell.

Murray, M. (2003). Narrative psychology and narrative analysis.

Mwai, W. (1988). *New Trends in Ushairi* (Doctoral dissertation).

Nofal, K. H. (2011). *Syntactic Aspects of Poetry: Apragmatic Perspective*. University of Buckingham press.

Nzuki, P. (2003). *Fani katika mchezo wa Karata na Bara Jingine:* Tasnifu ya Uzamili, Chuo Kikuu Cha Nairobi.

Ogula, P.A. (2005). *Research methods*. Nairobi: CUEA Publication.

Okuku, W. M. (2010). *Uchanganuzi wa Kiisimu wa baadhi ya Matini za Kiswahili. Mtazamo wa Pragmantiki Leksia.: University of Nairobi Kenya.*

Osore, M. (1994). *Uhakiki wa Kiisimu wa Fasihi Katika Riwaya za Suleiman Mohamed:* Tasnifu ya uzamili, Chuo Kikuu Cha Kenyatta.

Prince, A. (1983). *Relating to the Grid, 'Linquistic Inquiry*.' The MIT Press Publisher.

Shavinya, M. L. (2015). *Uchanganuzi wa Kiisimu wa baadhi ya semi katika Matini ya Kidini: Mtazamo wa Kipragmatiki.* Nairobi University Press.

Traugott, E. C. and Pratt, M. L. (1980*). Linguistic for students of literature* (p.275). New York: Harcourt Brace Jovanovich.

Wamitila, K. W. (2002). *Uhakiki wa fasihi: Misingi na vipengele vyake*. Nairobi: Phoenix Publishers Ltd.

Wamitila, K. W. (2008). *Misingi ya Uchanganuzi wa Fasihi:* Vide Muwa publishers, Kenya.